# Maarifa ya Jamii

## Kitabu cha Mwanafunzi

### Darasa la 5



Taasisi ya Elimu Tanzania

Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Maarifa ya Jamii

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Tano



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 554

Jina la Chapisho: Maarifa ya Jamii Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Tano

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-332-8

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 12 Julai, 2021 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Darasa la Tano katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa Mwaka 2016.

**Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa**
Kamishna wa Elimu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 1 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la Kwanza, 2018

Toleo la Pili, 2021

ISBN 978 - 9987 - 09 - 332 - 8

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 170/+255 735 041 168
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 2 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Yaliyomo

**Utangulizi** ........................................................................................v

**Shukurani** ........................................................................................vi

**Sura ya Kwanza**

Mazingira ........................................................................................1

**Sura ya Pili**

Utunzaji wa kumbukumbu za matukio ya kihistoria ..............................16

**Sura ya Tatu**

Hali ya hewa - Upepo ........................................................................22

**Sura ya Nne**

Utamaduni ........................................................................................ 29

**Sura ya Tano**

Uhusiano wa Tanzania na nchi za Ulaya na Asia kabla ya ukoloni .....40

**Sura ya Sita**

Jinsi wakoloni walivyogawana Afrika ................................................ 51

**Sura ya Saba**

Mashujaa wa Afrika waliopinga uvamizi wa kikoloni ............................59

**Sura ya Nane**

Utawala wa kikoloni ........................................................................67

**Sura ya Tisa**

Mashujaa wa Afrika dhidi ya uvamizi mpya ........................................88

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 3 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Sura ya Kumi**

Ramani ....................................................................................99

**Sura ya Kumi na Moja**

Mfumo wa jua ........................................................................104

**Sura ya Kumi na Mbili**

Rasilimali zetu .......................................................................111

**Sura ya Kumi na Tatu**

Uzalishaji mali ........................................................................120

**Sura ya Kumi na Nne**

Ujasiriamali ............................................................................129

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 4 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Utangulizi

Kitabu cha Maarifa ya Jamii Darasa la Tano ni kitabu cha tatu cha mwanafunzi katika mfululizo wa vitabu vya somo hili. Uandishi wa kitabu hiki umezingatia mahitaji ya mwanafunzi katika kukuza na kuendeleza umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK). Kitabu hiki kimeandikwa ili kumwezesha mwanafunzi kujifunza namna ya kutunza mazingira, kutunza kumbukumbu za matukio ya kihistoria, kubaini hali ya hewa ya upepo ya mahali fulani na kutambua utamaduni wa Mtanzania.

Pia, mwanafunzi atajifunza kutambua uhusiano wa Tanzania na nchi za Ulaya na Asia kabla ya ukoloni na jinsi wakoloni walivyogawana Afrika. Aidha, atajifunza mashujaa wa Afrika waliopinga uvamizi wa kikoloni, utawala wa kikoloni pamoja na mashujaa wa Afrika dhidi ya uvamizi mpya. Vilevile, atajifunza namna ya kusoma ramani, mfumo wa jua, kutambua rasilimali zetu, shughuli za uzalishaji mali pamoja na kupata stadi za ujasiriamali. Kitabu hiki kitamsaidia mwanafunzi kupata umahiri uliokusudiwa kwa somo hili kwa Darasa la Tano.

Mwisho, kitabu hiki kinawasilisha maudhui kwa njia ya matini, kazi za vitendo, kisa mafunzo, picha zenye mvuto pamoja na mazoezi yenye lengo la kupima uelewa wa mwanafunzi katika kila sura.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 5 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao walioshiriki kutayarisha kitabu hiki:

**Waandishi:** Anjela Moshy, Aikande Urasa, Karani Hemed Mdee, Lightness Kombe, Joan Mdanya, Merina Yohana, Charles Manyama na Theodora Silayo.

**Wahariri:** Prof. Gaudens Mpangala (Historia), Dkt. Lydia Kimaryo (Jiografia), Dkt. Donath Olomi (Ujasiriamali) na Musa Kaoneka (BAKITA).

**Msanifu:** Katalambula Faraji

**Wachoraji:** Alama Art and Media Production Limited

**Mratibu:** Anjela Moshy

Pia, TET inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa karibu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.



**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 6 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kwanza

## Mazingira

Ulipokuwa darasa la nne, ulijifunza kuhusu mazingira ya kijijini na mjini na vitendo vinavyochangia uharibifu wa mazingira ya kijiji au mtaa. Pia, ulijifunza shughuli za utunzaji wa mazingira. Katika sura hii utajifunza kuhusu shughuli zinazofanywa na binadamu kama vile kilimo, ufugaji, uchimbaji madini, uvuvi, ukataji miti ovyo na shughuli za viwandani zinavyoweza kuharibu mazingira. Vilevile, utajifunza kuhusu utunzaji wa vyanzo vya maji, vitendo vinavyoharibu vyanzo vya maji na athari zinazotokana na uharibifu wa vyanzo vya maji. Mwisho utajifunza njia za kutunza vyanzo hivyo.

### Maana ya mazingira

Neno mazingira linajumuisha vitu vyote vinavyotuzunguka vikiwemo viumbe hai na visivyo hai. Hivyo, mazingira yanaundwa na vitu vya asili na vitu vya kutengenezwa na binadamu. Mazingira ni mjumuisho wa hali ya hewa, wanyama, mimea, udongo, milima, mabonde, bahari na miundombinu.

### Uharibifu wa mazingira

Shughuli zote za binadamu hutegemea uwepo wa mazingira mazuri. Baadhi ya shughuli za binadamu huchangia uharibifu wa mazingira. Matumizi yasiyo sahihi ya mazingira hufanya mazingira kupoteza thamani yake, jambo ambalo husababisha binadamu kushindwa kufaidika nayo. Mazingira yanapoharibika husababisha athari mbalimbali. Kwa mfano, uharibifu wa ardhi husababisha ardhi kupoteza rutuba na kusababisha mavuno kupungua. Kuchafuliwa kwa hewa kutokana na moshi na vumbi kutoka viwandani husababisha kuongezeka kwa magonjwa ya binadamu kama vile kikohozi na mafua. Aidha, sumu za viwandani hufanya maji yanayotumika kwa shughuli mbalimbali kuchafuka.

### Shughuli za binadamu zinazochangia uharibifu wa mazingira

Baadhi ya shughuli za binadamu zinazoweza kuchangia uharibifu wa mazingira iwapo hazitafanyika kwa uangalifu ni pamoja na kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda na uchimbaji wa madini.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Kilimo

Kilimo ni shughuli ya uzalishaji mali inayohusisha uzalishaji wa mazao mbalimbali. Binadamu huzalisha mazao ya chakula na biashara. Baadhi ya mazao ya chakula ni mahindi, mpunga, mihogo, mtama, uwele, ndizi na karanga. Mazao ya biashara ni kama vile pamba, kahawa, katani, korosho na chai. Mazao hayo hulimwa sehemu mbalimbali nchini kutegemeana na hali ya hewa. Jedwali lifuatalo linaonesha mikoa inayolima mazao ya biashara na chakula kwa wingi nchini Tanzania.

**Jedwali namba 1:** *Baadhi ya mikoa inayolima mazao ya chakula na biashara kwa wingi nchini Tanzania*

| Mazao | Mkoa |
|---|---|
| Mahindi | Mbeya, Iringa, Ruvuma, Morogoro, Rukwa, Dodoma, Kilimanjaro, Njombe, Katavi na Songwe |
| Mpunga | Mbeya, Rukwa, Morogoro, Pwani, Tabora, Mwanza na Shinyanga |
| Ndizi | Kagera, Arusha, Kilimanjaro na Mbeya |
| Mihogo | Tanga, Mtwara, Lindi, Mwanza, Ruvuma, Pwani, Morogoro, Kigoma na Mara |
| Chai | Njombe, Tanga, Iringa na Mbeya |
| Kahawa | Kagera, Kilimanjaro, Arusha, Mbeya, Ruvuma na Songwe |
| Katani | Tanga na Morogoro |
| Pamba | Mwanza, Shinyanga, Simiyu na Tabora |
| Korosho | Lindi, Mtwara na Pwani |
| Tumbaku | Tabora, Ruvuma, Katavi na Iringa |

## Faida za kilimo

Kilimo hutupatia chakula na malighafi ambazo hupelekwa viwandani kwa ajili ya kuchakata. Halikadhalika, hutupatia fedha za ndani na za kigeni ambazo hupatikana kwa kuuza mazao ya biashara na chakula. Kwa ujumla, kilimo hutoa ajira na kuitambulisha nchi katika sura ya dunia, mfano kilimo cha pamba Mwanza na korosho Mtwara.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 2 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Athari zitokanazo na shughuli za kilimo kisichofaa katika mazingira

Pamoja na faida zitokanazo na kilimo, shughuli hii huweza kuharibu mazingira isipofanyika kwa uangalifu. Kwa mfano, kilimo katika miteremko ya milima husababisha mmomonyoko wa udongo. Kutokana na kilimo cha kuhamahama, watu hufyeka misitu ovyo na kuichoma moto hivyo husababisha ukame. Vilevile, matumizi ya dawa na mbolea za viwandani yasiyokuwa sahihi husababisha ardhi kupoteza rutuba yake ya asili na kuua viumbe hai vinavyoishi ardhini.

Kutokana na vitendo hivi, ardhi hupoteza uoto wake wa asili na kusababisha mmomonyoko wa udongo. Aidha, vyanzo vya maji hukauka na ardhi hupoteza rutuba. Madhara yanayotokana na vitendo hivyo kwa viumbe hai kama binadamu, wanyama na wadudu ni kukosa makazi, kupata magonjwa na vifo.



**Kielelezo namba 1:** Athari ya kulima katika eneo la mteremko

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 3 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Njia za kukabiliana na athari za shughuli za kilimo kisichofaa katika mazingira

Zipo njia mbalimbali zinazoweza kutumika katika kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira unaotokana na kilimo kisichofaa. Njia hizo ni kulima matuta ya kukingama na mteremko ili kuzuia mmomonyoko wa udongo. Njia nyingine ni kilimo mseto ambacho zao zaidi ya moja hulimwa katika eneo au shamba moja. Aina hii ya kilimo husaidia kuongeza rutuba katika ardhi. Pia, kulima kilimo cha kubadilisha mazao, mfano, mwaka huu mkulima akilima mahindi, mwakani analima mazao ya mikunde ambayo hurutubisha ardhi. Kupunguza matumizi ya dawa za kuulia wadudu na mbolea za viwandani ili kulinda rutuba ya asili ya udongo. Mbolea ya mboji au samadi inaweza kutumika badala ya mbolea za viwandani.

Aidha, kupanda miti katika maeneo yaliyoachwa wazi katika sehemu ambazo watu hufanya kilimo cha kuhamahama huzuia mmomonyoko wa udongo. Ni muhimu pia kupanda miti katika miteremko ya milima kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo.

## Ufugaji

Ufugaji ni shughuli inayohusu kutunza mifugo kama ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na bata. Kuna aina tatu za ufugaji nazo ni ufugaji wa ndani, ufugaji wa jadi au asili na ufugaji wa kuhamahama. Katika ufugaji wa ndani sehemu maalumu hutengwa kwa ajili ya kufugia. Ufugaji huu huweza kufanywa kwa mifugo michache. Aidha, mifugo mingi kama vile ng'ombe, mbuzi na kondoo hufugwa katika mashamba makubwa yanayomilikiwa na serikali, makampuni au watu binafsi, mashamba hayo huitwa ranchi. Aina nyingine ya ufugaji ni ule wa jadi au asili. Katika aina hii wafugaji hupeleka mifugo yao malishoni asubuhi na kuwarudisha mazizini jioni. Halikadhalika kuna ufugaji wa kuhamahama. Katika aina hii ya ufugaji, mfugaji hulazimika kuhama na mifugo yake kwa ajili ya kutafuta malisho na maji. Wakati mwingine mifugo hutembea umbali mrefu kabla ya kufika mahali penye malisho na maji.

Ufugaji wa ng'ombe hufanyika zaidi katika mikoa ya Mwanza, Mara, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Kilimanjaro na Arusha. Baadhi ya makabila yanayojihusisha na ufugaji huo ni Wamasai, Wabarbaig,

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 4 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wasukuma, Wanyamwezi, Wameru na Wagogo. Wafugaji kama vile Wamasai, Wabarbaig na Wasukuma hufuga kwa kuhamahama kutoka eneo moja hadi jingine wakitafuta maji na malisho kwa ajili ya mifugo yao.

## Faida za ufugaji

Ufugaji una faida nyingi. Baadhi ya faida hizo ni kutupatia nyama, maziwa, ngozi, kwato na mbolea. Ngozi hutumika kutengeneza vitu mbalimbali kama vile viatu, mabegi, mikanda na ngoma. Kwato hutumika kutengeneza gundi. Pia, mifugo hutupatia samadi kwa ajili ya kutumia kwenye kilimo kuzalisha mazao mbalimbali. Mazao hayo huzalishwa kwa ajili ya chakula na biashara. Vilevile, mifugo inapouzwa hutupatia fedha.

## Athari zitokanazo na ufugaji usiofaa

Wanyama wengi wanapochungwa kwenye eneo moja, humaliza nyasi zote na uoto mwingine na kuacha ardhi wazi. Makundi makubwa ya mifugo yanapopita mahali katika eneo kwa muda mrefu huondoa uoto katika ardhi. Pia, wanyama hao hufanya ardhi kuwa tifutifu na kusababisha upepo au mvua kuimomonyoa na kusafirisha udongo wake kwa urahisi. Udongo uliomomonyolewa huweza kusababisha mabwawa kujaa na kukauka. Hatimaye kusababisha ukosefu wa maji na malisho kwa mifugo, watu na viumbe wengine.

Aidha ufugaji wa kuhamahama husababisha ukataji miti ovyo pale ambapo wafugaji hutengeneza mazizi ya kuhifadhi mifugo yao na kupata kuni za kupikia. Baada ya muda wafugaji hao huondoka mahali hapo na kwenda sehemu nyingine ambako huendelea kufanya uharibifu wa mazingira.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 5 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 2:** Wafugaji wakichunga mifugo yao

## Njia za kudhibiti athari za ufugaji usiofaa

Njia ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaotokana na ufugaji usiofaa ni kuepuka kufuga mifugo mingi katika eneo dogo. Kupunguza idadi ya mifugo kutasaidia kuepuka athari zitokanazo na shughuli za ufugaji. Hivyo, ni muhimu kutoa elimu ya ufugaji bora kwa wafugaji ili wafuge mifugo michache itakayotoa mazao bora na mengi mfano maziwa ya kutosha, nyama na ngozi bora.

### Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Ufugaji ni nini?
2. Orodhesha aina tatu za ufugaji.
3. Taja faida za mifugo katika jamii unayoishi.
4. Eleza madhara ya kufuga mifugo mingi katika eneo dogo.
5. Eleza madhara yatokanayo na mmomonyoko wa udongo kutokana na kilimo kisichofaa.
6. Taja faida za kilimo katika kuchangia uchumi wa Taifa.



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 6 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Viwanda

Kiwanda ni mahali panapofanyika shughuli ya kiuchumi inayohusisha uchakataji wa malighafi na kuzalisha bidhaa kwa kutumia mashine. Bidhaa hizo zinaweza kuwa nguo, magodoro, magari, bati, pikipiki, vyakula na vinywaji mbalimbali. Kuna aina mbili za viwanda ambazo ni viwanda vinavyochakata malighafi na viwanda vinavyozalisha bidhaa. Mifano ya viwanda vinavyochakata malighafi ni viwanda vya uchakataji wa pamba na kutengeneza nyuzi. Aina ya pili ya viwanda ni vile vinavyotengeneza bidhaa zinazotokana na malighafi au bidhaa za viwanda vya uchakataji. Kwa mfano kiwanda cha kutengeneza nguo kutokana na nyuzi za pamba, kiwanda cha kutengeneza mazulia kutokana na nyuzi za mkonge na kiwanda cha kutengeneza sukari kutokana na zao la miwa.

## Faida zitokanazo na shughuli za viwanda

Viwanda husaidia kuongeza ubora na thamani ya malighafi inayozalishwa na kupata bidhaa kwa matumizi mbalimbali. Viwanda husaidia kuinua pato la taifa kwa kuingiza fedha za kigeni baada ya kuuza bidhaa hizo nje ya nchi. Aidha, viwanda hutoa ajira kwa kuwa watu wengi huajiriwa viwandani. Pia, viwanda hutoa fursa ya watu kujiajiri kwa kuanzisha shughuli za ujasiriamali katika maeneo yenye viwanda.

## Athari zitokanazo na shughuli za viwanda katika mazingira

Viwanda husababisha uchafuzi wa aina mbalimbali wa mazingira kama vile kutoa hewa chafu yenye sumu, moshi, vumbi, taka ngumu, majitaka na kelele. Aina mbalimbali za gesi zinazotoka viwandani huwa ni sumu. Sumu hiyo hudhuru viumbe hai akiwemo binadamu. Uchafuzi wa hewa kutokana na shughuli za viwandani husababisha magonjwa mbalimbali kwa mfano magonjwa ya ngozi na magonjwa ya mfumo wa hewa. Pia uchafuzi wa hewa kutokana na viwanda, huchangia katika kusababisha mabadiliko ya tabia ya nchi kama vile ongezeko la joto, mafuriko na ukame.

Majitaka kutoka viwandani yakitiririshwa kwenye ardhi, mito na maziwa hudhuru viumbe hai wa nchi kavu na majini. Taka ngumu kama vile mifuko au chupa za plastiki zikitupwa ovyo katika mazingira kuchafua mazingira.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 7 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Njia za kudhibiti athari zitokanazo na shughuli za viwanda

Uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za viwandani unaweza kudhibitiwa kwa kujenga viwanda mbali na makazi ya watu. Kuweka utaratibu wa kusafisha maji taka yanayotoka viwandani ili yaweze kutumika kwa shughuli nyingine. Viwanda vijengewe mashine yenye mitambo ya kupunguza moshi na kusafisha hewa yenye sumu na vumbi linalotoka viwandani.

Viwanda viweke utaratibu wa urejelezaji takataka ambazo huweza kutumiwa tena kwa matumizi mengine au kutumiwa kama malighafi. Kwa mfano, karatasi zilizotumika kama vile magazeti huweza kurudishwa kiwandani na kuchakatwa ili kupata karatasi tena. Pia, karatasi huweza kubadilishwa kuwa nishati ya mkaa. Takataka nyingine zinaweza kubadilishwa kuwa mbolea. Aidha, vizuia sauti viwekwe viwandani ili kupunguza kelele za mashine.

**Kazi ya kufanya**

Tembelea kiwanda kilicho karibu ili kubaini taka zinazozalishwa na kuona namna urejelezaji wa takataka hizo unavyofanyika.

## Uchimbaji wa madini

Madini ni mkusanyiko wa maliasili zinazopatikana katika ardhi. Madini huchimbwa ardhini. Mifano ya madini ni dhahabu, almasi, chuma, makaa ya mawe, shaba na chumvi. Madini chumvi hupatikana kwa kuvukiza maji ya bahari na kubaki chumvi. Aidha chumvi inaweza kupatikana kwa kuvukiza majichumvi yaliyopo chini ya ardhi.

Uchimbaji wa madini ardhini hufanyika kwa mashine au mikono kwa kutumia vifaa rahisi kwa mfano majembe na sururu. Njia ya mikono hutumiwa na wachimbaji wadogo. Wachimbaji wakubwa hutumia mitambo mikubwa kuchimba madini ardhini.

Jedwali lifuatalo linaonesha baadhi ya madini na mahali yanapopatikana nchini Tanzania.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 8 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Jedwali namba 2:** *Baadhi ya madini na mahali yanapopatikana nchini Tanzania*

| Aina ya Madini | Mahali yanapopatikana |
|---|---|
| Dhahabu | Geita, Kahama mkoani Shinyanga, Chunya mkoani Mbeya, Mpanda mkoani Katavi, Amani mkoani Tanga, Sekenke na Manyoni mkoani Singida |
| Bati | Karagwe mkoani Kagera |
| Almasi | Mwadui mkoani Shinyanga |
| Tanzanite | Mererani mkoani Manyara |
| Makaa ya mawe | Songwe, Kiwira mkoani Mbeya na Mchuchuma mkoani Njombe |
| Rubi | Mahenge na Kilosa mkoani Morogoro |
| Chumvi | Uvinza mkoani Kigoma na mwambao wa Bahari ya Hindi |
| Chuma | Liganga mkoani Njombe, Mbeya, Milima ya Uluguru mkoani Morogoro na Mbabara karibu na ziwa Tanganyika |
| Chokaa | Chunya mkoani Mbeya, Kilwa mkoani Lindi na Tanga |
| Shaba | Mpanda mkoani Katavi |
| Ulanga | Ulanga mkoani Morogoro |
| Urani | Manyoni mkoani Singida, Bahi mkoani Dodoma na Namtumbo mkoani Ruvuma |

## Faida za madini

Uchimbaji wa madini husaidia watu kupata ajira na malighafi kwa ajili ya viwanda mbalimbali. Aidha, madini kama vile dhahabu, fedha na almasi huweza kutumika kama mapambo. Madini ya chumvi hutumika kama kiungo cha chakula na dawa. Aidha, chumvi hutumika kuhifadhi vyakula kama nyama na samaki visiharibike. Madini kama almasi hutumika kutengeneza mashine za kukata vitu vigumu viwandani, kukatia vioo na kutoboa au kuvunja miamba. Baadhi ya madini huuzwa nchi za nje na hivyo nchi hupata fedha za kigeni. Madini hutambulisha nchi. Kwa mfano,

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 9 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

madini ya Tanzanite ambayo hupatikana Tanzania peke yake, hufanya Tanzania itambulike na nchi mbalimbali.

## Athari zitokanazo na uchimbaji wa madini katika mazingira

Uchimbaji wa madini huharibu mazingira iwapo njia bora za uchimbaji hazitatumika. Uchimbaji madini huweza kusababisha mmomonyoko wa udongo na kuacha mashimo makubwa. Mahali palipochimbwa madini hapawezi kutumika kwa shughuli nyingine za uzalishaji mali mfano kilimo. Vumbi na moshi kutoka migodini husambaa na huweza kusababisha magonjwa kwa binadamu. Magonjwa hayo ni kama vile kifua, ugonjwa wa macho na magonjwa mengine yanayosababishwa na mzio wa vumbi. Aidha, kemikali zinazotumika katika kusafishia madini kama vile zebaki zikiingia katika vyanzo vya maji huathiri viumbe vya majini pamoja na binadamu.

Maeneo ya migodi mara nyingi hukumbwa na mafuriko. Kwa mfano, Mererani mkoani Manyara na Geita. Maeneo hayo hukumbwa na mafuriko kwa sababu uoto wa asili huondolewa na kusababisha maji kutiririka kwa kasi na kusomba udongo mwingi. Udongo huu huweza kuingia katika mito au mabwawa ambayo hujaa na kusababisha mafuriko. Maeneo ya migodi pia hukumbwa na ukame unaosababishwa na ukataji miti ovyo.

## Njia za kudhibiti athari za uchimbaji wa madini

Athari zinazosababishwa na uchimbaji wa madini zinaweza kudhibitiwa kwa kusawazisha sehemu za machimbo kwa kufukia mashimo makubwa na madogo. Pia, kupanda miti na nyasi katika maeneo yaliyoharibiwa na uchimbaji madini ili kurejesha uoto wake. Vilevile, kuweka mashine za kuchuja hewa chafu na maji machafu yanayotoka migodini. Njia nyingine ni kutunga sheria ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo ya machimbo.

### Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja aina za viwanda.
2. Eleza faida zinazotokana na viwanda.
3. Eleza madhara ya shughuli za viwanda katika mazingira.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 10 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

4. Moshi utokao viwandani una madhara gani kwa binadamu?
5. Eleza maana ya neno madini.
6. Orodhesha faida za uchimbaji wa madini.
7. Fafanua athari tatu zinazosababishwa na uchimbaji wa madini.
8. Kwa nini maeneo ya migodi hukumbwa na mafuriko?
9. Nini kifanyike kwenye maeneo yaliyoharibiwa na uchimbaji wa madini?

## Uvuvi

Uvuvi ni shughuli ya kiuchumi inayohusisha uvunaji wa bidhaa za majini wakiwemo samaki. Uvuvi hufanyika katika maziwa, mito, mabwawa na bahari. Baadhi ya aina ya samaki wanaopatikana baharini ni changu, pweza, kibua, kolekole na papa. Samaki hawa ni wa maji chumvi. Samaki wa maji baridi hupatikana kwenye maziwa, mito na mabwawa. Mfano wa samaki wa maji baridi ni sato, kambale na sangara.

### Faida za uvuvi

Shughuli ya uvuvi hutupatia faida nyingi. Baadhi ya faida hizo ni upatikanaji wa ajira kwa jamii zinazozunguka maeneo ya uvuvi mfano uchuuzi na ununuzi wa samaki. Vilevile, hutoa malighafi kwa ajili ya viwanda kama vile viwanda vya kusindika samaki. Samaki wanapouzwa huchangia kuongeza pato la taifa. Samaki wanapouzwa nje ya nchi hutupatia fedha za kigeni. Pia, uvuvi hutupatia chakula.

### Athari zitokanazo na shughuli ya uvuvi usiofaa katika mazingira

Kuna njia mbalimbali zinazotumika katika kuvua samaki. Njia hizo zinaweza kuwa bora au njia zisizo bora. Njia bora ni zile ambazo wavuvi hutumia nyavu sahihi zenye viwango vinavyokubalika katika kuvua. Njia zisizo bora ni zile ambazo huleta uharibifu wa samaki na mazalia yake. Mifano ya njia zisizo bora ni pamoja na matumizi ya sumu na baruti. Njia hizi huharibu mazingira ya baharini au ziwani na kuharibu mazalia ya samaki. Matumizi ya kokoro ni mojawapo ya njia zisizo bora za uvuvi kwani hukamata samaki wadogo na mayai. Samaki hao wangeachwa wakue wangekuwa na manufaa zaidi kwa jamii na nchi kwa ujumla.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 11 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mvuvi anapotumia sumu au baruti huua viumbe wengi wa majini, kwa hiyo husababisha viumbe hao kutoweka. Samaki waliovuliwa kwa kutumia sumu huweza kuleta madhara kwa afya ya binadamu kama vile saratani.

## Njia za kudhibiti uvuvi haramu

Uvuvi usio bora huitwa uvuvi haramu. Madhara yanayotokana na uvuvi haramu yanaweza kudhibitiwa kwa kuelimisha wavuvi kuhusu madhara ya kutumia baruti, sumu na kokoro. Vilevile, sheria za kuzuia uvuvi haramu zisimamiwe vizuri ili kuboresha shughuli za uvuvi. Aidha, wavuvi wajengewe uwezo wa kutumia vifaa bora vya uvuvi kwa kupewa mikopo yenye riba nafuu.

### Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja vifaa vinavyotumika katika uvuvi haramu.
2. Eleza madhara ya uvuvi haramu.
3. Nini kifanyike ili kuepukana na uvuvi haramu?

## Vyanzo vya maji

Maji ni rasilimali muhimu sana kwa maisha ya kila siku kwa viumbe hai. Kuna vyanzo vikuu vitatu vya maji:

(a) Maji yaliyopo chini ya ardhi mfano chemchemi na visima

(b) Maji yaliyopo juu ya ardhi mfano maziwa, mito na bahari

(c) Maji ya mvua

Mvua inaponyesha maji huingia ardhini mpaka kwenye miamba. Maji hayo hujitokeza tena juu ya ardhi kama chemchemi au mto.

Maji hutumika nyumbani kwa kupikia, kunywa, kufulia, kuoga na kufanya usafi. Maji hutumika pia viwandani ili kupooza mashine na kuchakata malighafi. Vilevile, maji hutumika kwa shughuli za umwagiliaji na kufua umeme. Umeme unaotokana na nguvu za maji huzalishwa kwa nguvu ya maporomoko ya maji. Mifano ya mabwawa ya kufua umeme hapa Tanzania ni Bwawa la Nyumba ya Mungu mkoani Kilimanjaro, Mtera mkoani Iringa na Kidatu mkoani Morogoro.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 12 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 4**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja vyanzo vitatu vya maji.
2. Taja matumizi manne ya maji nyumbani kwenu.
3. Tofauti na matumizi ya nyumbani, maji hutumika kwa shughuli gani nyingine?

**Kazi ya kufanya**

Tembelea chanzo cha maji kilichopo katika mazingira yako, kisha orodhesha vitendo vya utunzaji na uharibifu wa chanzo hicho.

## Vitendo vya uharibifu wa vyanzo vya maji

Shughuli za uzalishaji mali zinazofanywa na binadamu huhitaji matumizi makubwa ya maji. Binadamu anapofanya shughuli za uzalishaji mali huweza kuharibu vyanzo vya maji. Vitendo vinavyoweza kuharibu vyanzo vya maji ni pamoja na kulima na kulisha mifugo kwenye vyanzo vya maji, kukata miti na kuchoma misitu. Halikadhalika, kutupa taka na kutiririsha majitaka yanayotoka majumbani, viwandani na maeneo ya biashara karibu na vyanzo vya maji huchafua na kuharibu vyanzo vya maji.

## Athari zinazotokana na uharibifu wa vyanzo vya maji

Vyanzo vya maji vinapoharibiwa huleta athari kwa maisha ya viumbe hai. Athari mojawapo ni kusababisha upungufu wa maji kwa matumizi ya nyumbani na viwandani. Uharibifu huo pia huathiri shughuli za kilimo na uvuvi. Pia, uharibifu wa vyanzo vya maji husababisha magonjwa kama homa ya matumbo, kipindupindu, kuhara na kuhara damu. Vilevile, kuweka makazi ya watu karibu na vyanzo vya maji, husababisha maji kukauka hivyo kuleta usumbufu kwa watu.

## Njia zinazotumika kutunza vyanzo vya maji

Kwa kuzingatia umuhimu wa maji ni vema kutunza vyanzo vya maji kwa kupanda miti inayohifadhi maji kama vile mkuyu, kutokulima au kujenga

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 13 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

karibu na vyanzo vya maji na kutokutupa takataka za majumbani na zile za viwandani katika vyanzo hivyo. Pia, kuepuka kukata miti hasa ya asili na kuchoma moto katika maeneo ya vyanzo vya maji. Vilevile, kuweka sheria inayozuia kufanya shughuli za kiuchumi katika maeneo ya vyanzo vya maji. Aidha, jamii ielimishwe kuhusu umuhimu wa maji na njia za kutunza vyanzo hivyo.

## Zoezi la 5

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja vitendo vinavyoharibu vyanzo vya maji.
2. Madhara gani hutokea unapotumia maji machafu?
3. Taja athari zitokanazo na uharibifu wa vyanzo vya maji.
4. Eleza njia zinazotumika kutunza vyanzo vya maji.

## Zoezi la 6

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja shughuli tano za uzalishaji mali zinazofanywa na binadamu zinazoweza kuharibu mazingira.
2. Eleza kwa kifupi namna shughuli hizo za uzalishaji mali zinavyoweza kuharibu mazingira.
3. Eleza mbinu nne za kukabiliana na uharibifu wa mazingira utokanao na shughuli za uchimbaji madini.

**Chagua herufi ya jibu sahihi katika sentensi zifuatazo:**

4. ___________ ni jumla ya mambo yote yanayomzunguka binadamu.
   (a) Misitu
   (b) Mazingira ( )
   (c) Makazi
   (d) Milima
5. Mojawapo ya shughuli zinazofanywa na binadamu zinazoweza kuharibu mazingira ni ___________.
   (a) uchimbaji wa madini
   (b) ufugaji wa ndani ( )
   (c) ukusanyaji takataka
   (d) urejelezaji



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 14 30/07/2021 09:33
FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

6. Kufuga mifugo mingi katika eneo dogo husababisha __________.
   (a) mifugo kunenepa
   (b) wachungaji kuchoka ( )
   (c) mmomonyoko wa udongo
   (d) majani kuongezeka
7. Uvuvi haramu ni hatari kwa vile huharibu __________.
   (a) miundombinu
   (b) mazalia ya samaki ( )
   (c) chakula
   (d) mali asili
8. Ni muhimu __________ takataka za viwandani ili kutunza mazingira.
   (a) kurejeleza
   (b) kutupa ovyo ( )
   (c) kuficha
   (d) kufukia

**Andika Ndiyo kwa sentensi sahihi na Hapana kwa sentensi zisizo sahihi.**

9. Mito, maziwa na bahari ni vyanzo vya maji. __________
10. Kitendo cha kupanda miti ni hali ya kutokutunza mazingira. __________
11. Kilimo mseto huharibu rutuba ya udongo. __________
12. Kukata miti ovyo husababisha ukame. __________
13. Ili kutunza vyanzo vya maji inatupasa kufuata kanuni za utunzaji wa mazingira. __________

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Madini | ni mkusanyiko wa maliasili zinazopatikana ardhini |
| Migodi | ni mahali panapochimbwa madini |
| Ukame | ukosefu wa mvua kwa muda mrefu |
| Urejelezaji | kukusanya takataka na kuzichakata ili kupata malighafi ambayo inaweza kutumika tena kutengeneza bidhaa nyingine |



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 15 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Pili

## Utunzaji wa kumbukumbu za matukio ya kihistoria

Ulipokuwa darasa la nne, ulijifunza matukio yaliyotokea katika familia yako na shuleni, njia za kupata taarifa za matukio ya kihistoria, vifaa vinavyotumika kuchukua taarifa za matukio na njia za kutunza taarifa za matukio hayo. Katika sura hii utachambua matukio ya kihistoria yaliyowahi kutokea Tanzania, vyanzo vya taarifa za matukio ya kihistoria na namna ya kukusanya na kuandika taarifa za matukio katika mazingira yanayokuzunguka. Pia, utajifunza maeneo ambayo kumbukumbu za kihistoria zinatunzwa.

### Matukio ya kihistoria Tanzania

Yapo matukio mbalimbali ya kihistoria yaliyowahi kutokea nchini Tanzania. Baadhi ya matukio hayo yameorodheshwa katika jedwali lifuatalo.

**Jedwali namba 1:** *Mwaka na matukio ya kihistoria Tanzania*

| Mwaka | Matukio ya Kihistoria |
|---|---|
| 1961 | Tanganyika ilipata uhuru |
| 1964 | Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar |
| 1967 | Azimio la Arusha |
| 1972 | Kifo cha Rais wa kwanza wa Zanzibar hayati Sheikh Abeid Amani Karume |
| 1974 | Azimio la Musoma |
| 1978 – 1979 | Vita vya Kagera |
| 1984 | Kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania hayati Edward Moringe Sokoine |
| 1996 | Ajali ya meli ya M.V. Bukoba |
| 1997 – 1998 | Mvua ya Elinino |
| 1999 | Kifo cha Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere ambaye pia alikuwa Rais wa kwanza wa Tanganyika |
| 2002 | Ajali ya garimoshi Dodoma |

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 16 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Tanganyika ilipata uhuru mwaka gani?
2. Tanganyika na Zanzibar ziliungana mwaka gani?
3. Vita vya Kagera vilitokea mwaka gani?
4. Edward Moringe Sokoine alikuwa nani?
5. Taja jina la Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Kazi ya kufanya**

Andika habari yoyote inayohusu tukio lililowahi kukutokea au ulilowahi kulishuhudia, kisha wasimulie wenzako darasani.

## Vyanzo vya taarifa za matukio ya kihistoria

Katika ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu, wanahistoria hutumia vyanzo mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) Akiolojia ni njia ambayo mwanaakiolojia hufukua ardhini kutafuta mabaki ya kale ya binadamu, majengo, na zana zilizotumika enzi za kale. Mwanahistoria hutumia mambo hayo yaliyogunduliwa na wanaakiolojia katika kuandika historia ya maisha ya watu, matukio na muda.

(b) Anthropolojia ni njia anayotumia mwanahistoria kupata taarifa zinazohusu historia na utamaduni wa maisha na maendeleo ya binadamu. Vitu vinavyochunguzwa ni pamoja na mila, desturi na lugha.

(c) Lugha ni njia mojawapo inayotumika kukusanya taarifa mbalimbali za kihistoria kutoka katika jamii. Lugha inabeba taarifa za kihistoria na husaidia kufuatilia asili ya watu husika. Mfano baadhi ya maneno katika lugha ya Kingoni yanafanana na maneno ya lugha ya Kizulu. Hii inaonesha uhusiano wa karibu kati ya Wangoni wa Tanzania na Wazulu wa Afrika ya Kusini.

(d) Masimulizi ya mdomo ni njia ya kurithisha taarifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kupitia masimulizi tunapata taarifa za kihistoria zilizohifadhiwa vichwani mwa watu kwa njia ya sanaa, muziki, michezo au kwa kusimulia hadithi au habari za matukio mbalimbali.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 17 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(e) Machapisho ni maandiko yanayotunza taarifa mbalimbali za kihistoria mfano, majarida, vitabu na magazeti.

(f) Makumbusho ya Taifa ni mahali ambako kumbukumbu za matukio ya kihistoria zimehifadhiwa au zinapatikana, mfano jengo la Makumbusho ya Taifa Dar es Salaam na jengo la kumbukumbu ya hayati Mwalimu Nyerere Butiama. Jengo hili hutumika kuhifadhi kumbukumbu za kihistoria za Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## Njia za kukusanya taarifa za matukio ya kihistoria katika mazingira

Taarifa za matukio ya kihistoria katika mazingira huweza kukusanywa kwa kutumia njia mbalimbali. Njia hizo ni pamoja na:

(a) Mahojiano

(b) Kutumia dodoso

(c) Kusoma maandiko mbalimbali

(d) Kufanya uchunguzi kwenye maeneo ya kihistoria

Taarifa za matukio ya kihistoria zinaweza kupatikana katika maktaba, Makumbusho ya Taifa na kwa watu mbalimbali katika jamii walioshuhudia matukio husika.

Baadhi ya vifaa vinavyoweza kutumika katika kukusanya taarifa za kihistoria ni:

(a) Kinasa sauti

(b) Daftari

(c) Kamera

### Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja vifaa vinavyoweza kutumika katika kukusanya taarifa za kihistoria.
2. Orodhesha njia za kukusanya taarifa za kihistoria.
3. Taja vyanzo vya taarifa za matukio ya kihistoria.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 18 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vyanzo na maeneo yenye kumbukumbu za matukio ya kihistoria Tanzania

Wanahistoria hupata taarifa za kumbukumbu za matukio ya kihistoria kwa kutumia vyanzo na maeneo mbalimbali. Vyanzo na maeneo hayo ni Makumbusho ya Taifa, Nyaraka za Taifa, Maktaba mbalimbali, Kijiji cha Makumbusho Dar es Salaam, Kijiji cha Kaole kilichoko Bagamoyo na maeneo ya Ujiji huko Kigoma. Jumba kuu la makumbusho ya Taifa lipo Dar es Salaam, na mengine madogo yapo Kalenga - Iringa, Bujora - Mwanza, Halwego Handebezyo Ukerewe - Mwanza na Butiama - Mara kunakotunzwa kumbukumbu za hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere. Vyanzo na maeneo mengine ni Mji Mkongwe Zanzibar, Kilwa, Isimila, Bonde la Olduvai, Kondoa Irangi, Engaruka, Makumbusho ya Mashujaa wa vita vya Maji Maji eneo la Mahenge mjini Songea na makumbusho ya kumbukumbu za Azimio la Arusha. Katika Makumbusho na nyaraka za Taifa tunapata taarifa za kihistoria zinazohusu masuala ya kiutamaduni, kijamii, kiuchumi, kisiasa na maendeleo ya teknolojia kuanzia zama za kale hadi sasa.

Taarifa za kihistoria zinazohusu shughuli mbalimbali za binadamu wa kale hadi sasa huhifadhiwa katika maktaba mbalimbali. Taarifa hizo ziko kwenye vitabu, majarida yaliyoandikwa na wamisionari na wapelelezi wa kwanza, barua za kibiashara na machapisho mengine. Pia, katika maktaba kunahifadhiwa taarifa mbalimbali za kiserikali, taasisi na vyama. Taarifa hizi zinatusaidia kujua vipindi mbalimbali vya maisha ya binadamu na jinsi walivyoishi.

### Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi.**

1. Makumbusho ni sehemu inayotumika:
   (a) kutunza kumbukumbu za vizazi na vifo
   (b) kutunza kumbukumbu za kihistoria ( )
   (c) kutunza kumbukumbu za masomo
   (d) kutunza kumbukumbu za kiteknolojia tu

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 19 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Utunzaji wa kumbukumbu za kihistoria husaidia:
   (a) kufahamu mambo yaliyopita, yaliyopo na yajayo
   (b) kufahamu mambo yaliyopo ( )
   (c) kuboresha mambo ya kale
   (d) kufahamu mambo yajayo
3. Baadhi ya sehemu zinazotumika kutunza kumbukumbu za kihistoria katika Tanzania ni:
   (a) msikitini na kanisani
   (b) hekaluni na makumbusho ( )
   (c) makumbusho na maktaba
   (d) gulioni na shuleni
4. Ni maeneo gani ya kihistoria yaliyopo Tanzania ambako taarifa za kumbukumbu za kihistoria hupatikana?
   (a) Bonde la Olduvai Gorge, Engaruka, Kondoa Irangi na Isimila
   (b) Lushoto, Bagamoyo, Kilwa na Rusinga ( )
   (c) Rusinga, Isimila , Nsogenzi na Engaruka
   (d) Uvinza, Ugweno, Kilwa na Chekereni
5. Kumbukumbu za maandishi kama vitabu, barua na ripoti mbalimbali hutunzwa kwenye:
   (a) makumbusho na mapango
   (b) maktaba na nyaraka za taifa ( )
   (c) mapango na maktaba
   (d) nyumba na mahakama

**Kazi ya kufanya**

Tembelea sehemu yoyote yenye kumbukumbu za kihistoria iliyokaribu na shule ili kupata taarifa za matukio ya kihistoria, kisha wasimulie wenzako darasani.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza maana ya maneno yafuatayo:
   (a) Anthropolojia (b) Akiolojia
2. Eleza matumizi ya Makumbusho ya Taifa.
3. Bainisha umuhimu wa taarifa zinazopatikana katika maeneo mbalimbali ya kihistoria.

**Andika Ndiyo kwa sentensi sahihi na Hapana kwa sentensi zisizo sahihi.**

4. Masimulizi ni maelezo yanayotolewa na mtu kwa njia ya mdomo. ___________
5. Katika Tanzania jumba kuu la Makumbusho ya Taifa lipo katika jiji la Arusha. ___________
6. Uchunguzi unaofanywa katika maeneo mbalimbali ya kihistoria husaidia kupata taarifa za matukio ya kihistoria. ___________

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Azimio | ni tamko au tangazo linaloelezea jambo fulani |
| Hekalu | ni nyumba ya kuabudia |

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 21 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tatu

## Hali ya hewa – Upepo

Ulipokuwa darasa la nne, ulijifunza kuhusu dhana ya hali ya hewa, vipengele vya hali ya hewa na vifaa vinavyotumika kupima vipengele vya hali ya hewa. Vilevile, ulijifunza mabadiliko ya hali ya hewa. Katika sura hii, utajifunza maana ya upepo, sababu za kutokea kwa upepo, faida zinazotokana na upepo na hasara zake. Mwisho, utajifunza upimaji wa upepo.

### Maana ya upepo

Upepo ni hewa inayokwenda kwa kasi. Upepo huvuma kutoka sehemu yenye mgandamizo mkubwa wa hewa kwenda sehemu yenye mgandamizo mdogo wa hewa. Mfano, ukichukua mpira uliojazwa hewa, kisha ukautoboa kwa sindano utaona kuwa hewa iliyomo ndani ya mpira inatoka nje ya mpira kwa kasi. Hali hii hutokea kwa sababu kwenye mpira kuna mgandamizo mkubwa wa hewa kuliko nje ya mpira huo.

### Sababu za kutokea kwa upepo

Upepo hutokea kutokana na tofauti ya mgandamizo wa hewa kati ya sehemu moja na nyingine. Ongezeko la joto husababisha hewa kutanuka, kuwa nyepesi na kupaa juu. Kwa hiyo mgandamizo huwa mdogo. Hali hiyo husababisha hewa ya baridi kuingia kuchukua nafasi iliyoachwa na hewa ya joto. Hali ya ubaridi inaifanya hewa kusinyaa na kusababisha mgandamizo mkubwa wa hewa. Tofauti ya joto inapokuwa kubwa kati ya maeneo mawili upepo huwa mkali.

**Kazi ya kufanya**

Chukua puto, kisha puliza ili kulijaza upepo. Likijaa, lifunge mdomo wake. Toboa puto kwa kutumia sindano au pini ili kuona namna hewa inavyotoka sehemu yenye mgandamizo mkubwa wa hewa kwenda sehemu yenye mgandamizo mdogo wa hewa.



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Faida zinazotokana na upepo

Upepo una faida zifuatazo katika maisha ya kila siku.

(a) Kuendesha mashine za kuvuta maji kutoka ardhini. Katika sehemu zenye upepo mwingi kinuupepo hutumika kuendesha mashine zinazovuta maji kutoka kwenye kisima.



**Kielelezo namba 1:** Kinuupepo kikivuta maji kutoka ardhini

(b) Kuendesha mitambo ya kufua umeme. Kinuupepo kinaweza kutumika kuendesha mashine za kufua umeme. Mkoa wa Singida ni sehemu mojawapo ambapo upepo hutumika kufua umeme. Kwa hiyo ni muhimu kuwekeza kwenye matumizi ya nguvu ya upepo katika kuvuta maji au kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme. Hii itasaidia kupunguza matumizi ya nishati nyingine kama vile mafuta, gesi na umeme.

(c) Kuchavusha maua ya mimea ili itengeneze matunda na kutoa mbegu. Hivyo, upepo ni moja ya wakala wa uchavushaji.



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 23 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Kukausha vitu mfano nguo na mazao. Upepo mkavu unapovuma huchukua unyevu kutoka kwenye nguo au mazao yaliyoanikwa na kuyakausha.

(e) Kupooza joto. Kwa mfano, nyakati za joto watu hupenda kukaa katika fukwe za bahari ili kupunga upepo. Vilevile, wakati wa joto watu hutumia pangaboi ambalo hupuliza upepo unaopooza mwili. Aidha, pangaboi katika injini ya gari hupuliza upepo unaopooza maji yanayozunguka kupooza joto la injini.

(f) Kusababisha mvua kunyesha. Upepo unapovuma sehemu yenye unyevu huchukua unyevunyevu huo na kupandisha juu hatimaye kutengeneza mawingu. Mawingu hayo husababisha mvua kunyesha.

## Hasara zinazotokana na upepo

Pamoja na faida za upepo ulizojifunza, upepo unasababisha hasara zifuatazo:

(a) Kuharibu majengo. Upepo mkali huwa na nguvu ya kuezua mapaa na kuangusha nyumba na kusababisha hasara na hata vifo kwa watu na wanyama.



**Kielelezo namba 2:** Athari za upepo

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Kusababisha kuenea kwa magonjwa kwa kusambaza vimelea vya magonjwa mbalimbali mfano kifua kikuu, mafua na macho. Upepo mkali hutimua vumbi ambalo husambaza vimelea vya magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya hewa.

(c) Kuharibu uoto wa asili. Kwa mfano kimbunga huweza kung'oa miti na hivyo kuharibu uoto wa asili wa sehemu husika.

(d) Husababisha mafuriko. Kwa mfano, kimbunga kinachotokea baharini husababisha mafuriko katika visiwa na maeneo ya pwani ambayo kimbunga hupita.

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Upepo ni nini?
2. Eleza sababu za kutokea kwa upepo.
3. Taja faida mbili za kinuupepo.
4. Taja faida za upepo.
5. Eleza madhara ya upepo mkali.

## Upimaji wa upepo

Upepo unapovuma kuna vitu viwili ambavyo tunaviona. Vitu hivyo ni mwelekeo wa upepo na kasi ya upepo. Unaweza kutambua upepo unakoelekea kwa kuangalia upande miti au majani yanakoinamia. Kasi ya upepo unaweza kuitambua kwa kuangalia kiwango cha kuyumba kwa miti, majani au kupeperushwa kwa vitu mbalimbali. Kwa uhakika zaidi, ili kujua uelekeo na kasi ya upepo vipo vifaa maalumu vya kupimia kasi na mwelekeo wa upepo. Kifaa kinachotumika kupima mwelekeo wa upepo kinaitwa kipimaupepo. Sehemu ya juu ya kifaa hiki kuna mshale unaoonesha uelekeo wa upepo. Mshale huo umepachikwa katika bomba, chini ya mshale zimewekwa mbao au vipande vya chuma vinavyoonesha pande kuu nne za dira ambazo ni Kaskazini, Mashariki, Kusini na Magharibi. Upepo unapovuma, mshale huelekea upande upepo unapotokea. Tazama kielelezo namba 3.

Jina la upepo hutegemea upande unakotokea. Kwa mfano, kama upepo

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 25 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

unavuma kutoka Kusini kuelekea Kaskazini hujulikana kama upepo wa kusi. Upepo unaovuma kutoka Kaskazini kuelekea Kusini hujulikana kama upepo wa kaskazi. Upepo unaovuma kutoka Mashariki kuelekea Magharibi hujulikana kama upepo wa Mashariki, na upepo unaotoka Magharibi kuelekea Mashariki hujulikana kama upepo wa Magharibi.




**Kielelezo namba 3:** Kipimaupepo

Kasi ya upepo hupimwa kwa kifaa maalumu kinachoitwa Anemomita. Anemomita ni kifaa ambacho kimeundwa mfano wa vikombe vitatu au vinne vilivyoshikiliwa na chuma ambacho huzunguka. Upepo unapovuma vikombe hujizungusha. Upepo unapokuwa mkali vikombe hujizungusha kwa kasi zaidi. Idadi ya mizunguko hurekodiwa kwenye mita iliyoko katika chombo hicho. Idadi hii huonesha kasi ya upepo kwa kilomita kwa saa. Kwa mfano katika kielelezo namba 4 kasi ya upepo inasomeka kilomita 28.3 kwa saa.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 26 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 4:** Anemomita

## Namna ya kujikinga na madhara ya upepo

Mara nyingi tunasikia kwenye vyombo vya habari kuwa upepo mkali umetokea na nyumba nyingi zimeezuliwa au kuta zimeanguka. Madhara yote haya yanatokana na upepo kuwa na kasi kubwa. Jamii ambayo iko kwenye maeneo hayo ni vema ikachukua tahadhari ya kujikinga na madhara hayo yaletwayo na upepo mkali. Namna ya kujikinga na madhara hayo ni kupanda miti katika maeneo yote yaliyo wazi. Miti ina uwezo mkubwa wa kupunguza kasi ya upepo, hatimaye kupunguza madhara yake. Pia, nyumba zinazojengwa kwenye maeneo yenye upepo mkali ziwekwe mapaa imara.

### Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja mambo matatu yatakayokuonesha kuwa upepo mkali unavuma.



FOR ONLINE USE ONLY

MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 27 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

2. Kwa nini madhara ya upepo huwa makubwa katika maeneo yasiyo na miti?
3. Nini kifanyike katika maeneo yenye upepo mkali ili kupunguza madhara yake?
4. Nini kinasababisha upepo kutokea?
5. Kwa nini eneo moja linaweza kupata madhara makubwa kutokana na upepo mkali kuliko eneo jingine?

**Oanisha maneno kutoka Safu A na sentensi kutoka safu B, kisha andika majibu yako kwa kujaza herufi sehemu ya majibu.**

| Na | Safu A | Majibu | Safu B |
|---|---|---|---|
| 6. | Anemomita | ( ) | (a) Hupima mwelekeo wa upepo |
| 7. | Upepo | ( ) | (b) Mojawapo ya faida za upepo |
| 8. | Kuezua mapaa | ( ) | (c) Hupima mgandamizo wa upepo |
| 9. | Kuchavusha mimea | ( ) | (d) Hupima joto la mahali |
| 10. | Kipimaupepo | ( ) | (e) Hurutubisha mimea |
| | | | (f) Hupima kasi ya upepo |
| | | | (g) Hewa inayokwenda kwa kasi |
| | | | (h) Upepo uvumao kwa kasi |
| | | | (i) Mojawapo ya hasara za upepo |

## Msamiati

Kimbunga — upepo unaovuma kwa kasi

Kinuupepo — ni mtambo unaotumia nguvu ya upepo kuzalisha umeme au kusukuma maji



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 28 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nne

## Utamaduni

Ulipokuwa darasa la nne, ulijifunza mambo yanayojenga ushirikiano baina ya watu katika jamii. Katika sura hii utajifunza utamaduni wa Mtanzania, dhana ya utamaduni, vielelezo vya utamaduni na umuhimu wa mila, michezo na desturi. Pia, utajifunza mambo yanayoathiri utamaduni na namna ya kudumisha mila na desturi nzuri.

### Maana ya utamaduni

Utamaduni ni mfumo mzima wa maisha ya watu fulani, jamii au nchi, mila na desturi zao za asili, jadi au imani. Utamaduni hutambulisha na kuwaunganisha watu wa jamii husika kwa njia ya lugha, chakula, mavazi, nyimbo, michezo, mila na desturi.

Utamaduni wa Mtanzania ni mfumo wa maisha ya Watanzania jinsi wanavyoishi kwa kufuata mila, desturi, jadi, imani, michezo na maendeleo yao kijamii, kiuchumi na kisiasa. Tanzania ina makabila yasiyopungua 120, yote yana mila na desturi zao za namna tofautitofauti. Aidha, utamaduni wa Mtanzania umeunganishwa na lugha moja ya Kiswahili ambayo ni lugha ya taifa. Pia, Kiswahili ni lugha ya mawasiliano katika nchi za Afrika Mashariki.

### Umuhimu wa utamaduni kwa Mtanzania

Utamaduni ni muhimu kwa Mtanzania kwa sababu zifuatazo:

(a) Ni alama ya umoja wa kitaifa na utambulisho wa kijamii.

(b) Hudumisha uhusiano katika jamii kwa kutunza heshima iliyopo miongoni mwa wanajamii.

(c) Husaidia jamii kuthamini rasilimali za Taifa letu.

(d) Hutunza maadili ya malezi ya watoto, vijana na wazee.

(e) Husisitiza uvaaji wa mavazi ya heshima.

(f) Husisitiza uwajibikaji miongoni mwa wanajamii ili kukuza uchumi wa nchi.

(g) Huepusha kudharau tamaduni zetu na kuiga za kigeni.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 29 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vielelezo vya utamaduni wa Mtanzania

Utamaduni wa Mtanzania unajitokeza katika mambo mbalimbali kama vile lugha, mila, desturi, michezo, sanaa na mavazi.

**Lugha:** Ni mfumo wa mawasiliano kati ya watu wa jamii au taifa fulani. Utamaduni wa Mtanzania umeunganishwa kwa lugha ya Kiswahili inayotumika katika kuwasiliana.

Lugha ni chombo cha mawasiliano ambacho hutumika kama utambulisho wa jamii katika kuelimisha, kupashana habari na kubadilishana mawazo. Aidha, lugha hutumiwa na jamii kurithisha mila na tamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hadithi, vitendawili, methali na nyimbo ni mifano ya namna lugha inavyoweza kutumika kurithisha tamaduni za jamii.

**Mila:** Ni jumla ya mambo yanayofanywa na jamii husika kulingana na asili, mazingira na mienendo ya jamii hiyo. Endapo mwanajamii atakiuka mila hizo, atapewa adhabu au onyo na viongozi wa jamii husika kulingana na taratibu zao. Taratibu za kuoa au kuolewa, ibada, urithi na matambiko ni miongoni mwa mila ambazo hutambulisha watu katika mazingira tofautitofauti ya kitanzania. Miongoni mwa mila kongwe za makabila ya Tanzania zenye athari kubwa kwa baadhi ya makabila ni jando na unyago. Katika jamii nyingi za kitanzania, jando na unyago zilikuwa sehemu kubwa ya kutoa malezi bora kwa vijana wa kike na kiume.

Mafunzo katika jando na unyago yalikuwa na nia ya kumuandaa kijana kuingia katika hatua ya utu uzima. Wasichana na wavulana walifundishwa jinsi ya kutunza nyumba, watoto na kuishi vizuri na familia. Elimu hii ilisaidia kudumisha upendo na uelewano katika jamii. Mafunzo ya jando kwa wavulana yalihusisha kutahiriwa. Baadhi ya makabila kama ya Wagogo, Wanyaturu, Wakurya, Wambulu na Wamasai walitahiri vijana wa kiume. Vilevile, kipindi cha jando kilihusisha kuwapatia vijana elimu na stadi mbalimbali za maisha. Mila nyingi za makabila ni nzuri na zinafaa kwa malezi na stadi za maisha kwa wanajamii. Hata hivyo, baadhi ya mila kama vile tohara kwa wasichana, kukataza kina mama kula vyakula kama mayai, maini na maziwa ni baadhi ya mila potofu ambazo jamii huzipinga.

**Desturi:** Ni mambo ya kawaida yanayofanywa mara kwa mara na wanajamii. Pia, huweza kubadilika kulingana na mahali na wakati. Kila jamiii ina utambulisho wake wa desturi kama vile tiba, mavazi vinywaji na vyakula. Mfano, jamii nyingi zina aina fulani za vinywaji ambavyo vinawatambulisha kama vile mbege kwa jamii ya Wachaga, kimpumu

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 30 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwa jamii ya Wanyakyusa, dengelua kwa jamii ya Wapare, kangara kwa jamii ya Wagogo, obhulandi kwa jamii ya Wajita, khangaa kwa jamii ya Wanyaturu, kayoga kwa jamii ya Waha na myakaya kwa jamii ya Wangoni.

Aidha, vyakula ni mtori kwa jamii ya Wachaga, mbaragha kwa jamii ya Wanyakyusa, kishumba kwa jamii ya Wapare, jinumbu kwa jamii Wajita, ugali na mlenda kwa jamii ya Wanyaturu, ugali kwa jamii ya Waha na mfusulela kwa jamii ya Wangoni.

**Michezo:** Ni mambo yafanywayo kwa ajili ya kujifurahisha, kujichangamsha au kupitisha wakati. Vilevile, ni kati ya mambo muhimu katika utamaduni wa Mtanzania na nchi nyingine. Kwa Tanzania kuna aina mbili za michezo nazo ni michezo ya jadi na michezo ya kisasa. Michezo ya jadi ni kama vile kurusha mkuki, kucheza bao, kukimbia, kubembea na kuruka kamba. Michezo ya kisasa ni kama vile mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa wavu, mpira wa pete, mchezo wa ngumi na mchezo wa kuogelea.

**Sanaa:** Ni ufundi anaoutumia mtu ili kuwasilisha fikra au mawazo yake katika namna inayoburudisha na kufikirisha. Tunaweza kuona kazi za sanaa kupitia fasihi, uchoraji, ususi, ufumaji, udarizi, uchongaji na ufinyanzi. Sanaa hizi zimegawanyika katika makundi matatu kama ifuatavyo:

(a) Sanaa za maonesho ambazo mara nyingi huonekana kwa umbo maalumu zinaweza kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye. Mfano wa sanaa hizo ni udarizi, uchoraji, uchongaji na ufinyanzi. Tazama kielelezo namba 1 hadi 3.

(b) Sanaa za ghibu ni zile zisizoonekana katika umbo maalumu au kushikika bali hugusa hisia. Mfano ushairi, uimbaji na muziki.

(c) Sanaa za vitendo huonekana katika uzuri wa umbo na hufanyika kwa vitendo. Mfano ni mwanasanaa aigizapo kwa njia ya vichekesho, majigambo na nyimbo.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 31 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 1:** Maumbo ya sanaa katika uchongaji



**Kielelezo namba 2:** Sanaa ya ususi



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 32 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 3:** Sanaa ya ufinyanzi

## Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Vielelezo namba 1, 2 na 3 vinaonesha matendo gani ya sanaa?
2. Kati ya matendo ya kielelezo namba 1, 2 na 3 ni tendo lipi unaweza kulifanya?
3. Eleza maana ya utamaduni.
4. Taja umuhimu wa utamaduni kwa Mtanzania.
5. Toa mifano miwili ya utamaduni katika jamii yako.
6. Kiswahili kina umuhimu gani kwa utamaduni wa Mtanzania?

### Kazi ya kufanya

Jadili na wenzako kuhusu mila na desturi zinazofaa katika jamii unayoishi, kisha, ziandike kwenye daftari lako.



FOR ONLINE USE ONLY

MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 33 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Umuhimu wa mila na desturi

Utamaduni ni nyenzo muhimu sana katika jamii. Kila jamii hulinda mila na desturi zake kulingana na umuhimu wake ambao ni:

(a) Kusisitiza kushiriki katika kufanya kazi kwa juhudi na maarifa. Kila mtu katika jamii mwenye uwezo wa kufanya kazi anasisitizwa kufanya hivyo.

(b) Kudumisha na kuimarisha ushirikiano, kuthaminiana, kupendana na kuheshimiana katika jamii.

(c) Kusaidiana katika mambo mbalimbali kama vile harusi, jando na unyago, misiba na shughuli za uzalishaji mali.



**Kielelezo namba 4:** Wanajamii wakilima kwa kushirikiana

(d) Kusaidiana na kutatua migogoro ya jamii, mfano migogoro ya mali kama ardhi na mirathi. Hata hivyo, ukosefu wa nidhamu kwa vijana wenye rika tofautitofauti katika jamii huweza kusababisha migogoro mbalimbali. Hivyo wanajamii (hususani vijana) ambao huenda kinyume na mila na desturi zinazowazunguka hurekebishwa na wazazi wao au viongozi wa jamii hiyo.



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 34 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 5:** Kijana akionywa na mama yake

(e) Kukemea kuiga tamaduni za kigeni zinazokwenda kinyume na tamaduni zetu.

(f) Kusaidia kuendeleza mila na desturi nzuri kwa taifa. Kwa mfano kufanya kazi kwa bidii, weledi, utii na usikivu, kubisha hodi unapokwenda nyumbani kwa mtu, kushukuru unapopewa kitu na kusema pole kwa mtu aliyepatwa na shida au maumivu.

(g) Kujenga ari ya kujitegemea.

**Kazi ya kufanya**

Waombe wazazi au walezi wako wakufundishe kuimba na kucheza ngoma ya utamaduni wa kabila lako, kisha waimbie wenzako darasani.

Jadiliana na wenzako kuhusu umuhimu wa mila na desturi katika jamii, kisha uandike kwenye daftari lako.

## Mambo yanayoathiri utamaduni

(a) Maendeleo ya sayansi na teknolojia yanaweza kuathiri utamaduni. Mila huweza kubadilika kwa kuiga na kukuza utamaduni wa kigeni. Hali hii husababisha jamii kuacha mila na desturi zao nzuri. Mfano lugha, mavazi, vyakula, sherehe na desturi za mazishi.

(b) Mabadiliko ya mazingira kama vile ukame huathiri uzalishaji wa



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mazao hasa ya chakula. Mabadiliko haya hulazimisha kubadilika kwa utamaduni wa uzalishaji mazao ya chakula na ulaji wake katika jamii.

(c) Kukua kwa lugha ya Kiswahili kumechangia katika kuathiri lugha za makabila mengi. Lugha za makabila mengi zinafifishwa kutokana na kukua kwa lugha ya taifa.

(d) Mwingiliano baina ya nchi yetu na mataifa ya kigeni, umechangia kuleta maendeleo na vilevile kuathiri jamii yetu. Kwa mfano mapokeo ya mavazi ya kigeni, vyakula, michezo na kuiga tamaduni za mataifa mengine.

(e) Kushamiri kwa vipindi vingi visivyokuwa na maadili ya kitanzania katika televisheni, redio, magazeti na mitandao ya kijamii. Baadhi ya vyombo hivi hufanya kazi bila kufuata maadili ya utoaji wa habari kuhusu mavazi, vyakula na lugha ambavyo hupotosha utamaduni wa Mtanzania. Aidha baadhi ya vyombo vya habari hasa vya kigeni hupigia chapuo mila za kigeni kama mavazi na lugha hivyo huchangia kufifisha utamaduni wa kitanzania.

## Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Toa maana ya maneno yafuatayo:
   (a) Utamaduni
   (b) Sanaa
   (c) Mila
   (d) Desturi
   (e) Michezo
2. Taja aina za sanaa na mifano yake.
3. ___________ ni kielelezo cha utamaduni wa Mtanzania kwani kimefanikiwa kuunganisha makabila yote.
4. Taja makabila ambayo hujitambulisha kupitia mavazi yake.
5. Sanaa za maonesho ni kama vile ___________, ___________ na ___________.

**Andika Ndiyo kwa sentensi sahihi na Hapana kwa sentensi zisizo sahihi.**

6. Mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanaweza kuathiri utamaduni. ___________
7. Mila na desturi hutambulisha jamii fulani. ___________
8. Lugha ni kitambulisho cha jamii yoyote. ___________
9. Kufanya kazi ni kipimo cha utu katika jamii. ___________

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 36 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Namna ya kudumisha mila na desturi nzuri

Lugha za asili zinayatambulisha makabila zaidi ya 120 yenye mila, desturi na tamaduni tofauti. Lugha na utamaduni wa asili ni urithi usioshikika na una thamani kubwa kwa taifa. Hivyo, wazazi wasipuuze lugha zao za asili kwa kisingizio cha kuepuka ukabila. Ni wazi kuwa vijana wengi tangu kuzaliwa hutumia lugha ya Kiswahili, lakini ni muhimu pia kujifunza na kuthamini lugha za makabila yao.

Maendeleo ya sayansi na teknolojia pia yanaathiri utamaduni. Ili tusipoteze utamaduni wetu, wazee wanapaswa kutumiwa kikamilifu kukusanya taarifa za jamii husika. Taarifa hizo ziwekwe katika maandishi, michoro au vitu vya kutengeneza. Aidha, wazee wanapaswa kuweka mikakati ya kutangaza mila na desturi zao za zamani ili Watanzania wengine wazitambue.

Namna nyingine ya kudumisha mila na desturi nzuri ni kuweka mikakati ya kuanzisha vituo vya kuhifadhi taarifa mbalimbali kuhusu mila na desturi za kila kabila. Taratibu hizo ni pamoja na kuwafundisha watoto lugha, mila na desturi nzuri za makabila yao.

**Kazi ya kufanya**

Kwa kushirikiana na wanafunzi wenzako jadili namna utamaduni wa Mtanzania unavyopotoshwa na mila na desturi za kigeni. Kisha andika katika daftari lako.

**Zoezi la 3**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Tunawezaje kudumisha mila na desturi zetu?
2. Orodhesha umuhimu wa mila unazozijua.
3. Taja namna tatu za kudumisha mila na desturi nzuri.

**Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua jibu sahihi.**

4. Lugha inayowaunganisha Watanzania wote ni:
   (a) Kihehe
   (b) Kiswahili ( )
   (c) Kiingereza
   (d) Kisukuma

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 37 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Ufundi wa kuwasilisha hisia na mawazo yaliyomo katika fikra huitwa:
   (a) mila
   (b) desturi ( )
   (c) sanaa
   (d) utamaduni
6. Mambo yanayofanywa na jamii fulani kulingana na asili, mazingira na mienendo ya jamii hiyo huitwa:
   (a) mila
   (b) desturi ( )
   (c) utamaduni
   (d) sanaa
7. __________ ni asili, mila, jadi, imani na desturi za jamii fulani:
   (a) Utamaduni
   (b) Desturi ( )
   (c) Sanaa
   (d) Mila
8. Jambo la kawaida linalotendwa kila siku na jamii fulani huitwa:
   (a) lugha
   (b) sanaa ( )
   (c) desturi
   (d) mila

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi.**

9. Lugha ni kitambulisho kikubwa cha __________.
10. __________ ni namna mtu au kikundi cha watu kinavyoweza kuwasilisha hisia, mawazo au fikra zao.
11. Mafunzo waliyokuwa wakipatiwa vijana katika jamii kwa lengo la kuwaandaa kuingia hatua ya utu uzima yaliitwa __________ kwa wavulana na __________ kwa wasichana.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 38 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Oanisha maswali kutoka Safu A na majibu kutoka Safu B, kisha andika jibu kwa kujaza herufi kwenye sehemu ya majibu.**

<table>
<tr><th>Na</th><th>Fungu A</th><th>Majibu</th><th>Fungu B</th></tr>
<tr><td>12.</td><td>Mashairi, ngonjera na uchongaji</td><td>( )</td><td rowspan="5">(a) Kiswahili<br>(b) Utamaduni<br>(c) Desturi<br>(d) Mambo yanayotambulisha mila za jamii<br>(e) Ni sehemu ya sanaa<br>(f) Ni matokeo ya kulima wakati wa mvua nyingi<br>(g) Kiingereza</td></tr>
<tr><td>13.</td><td>Kielelezo cha uhai na utashi wa jamii</td><td>( )</td></tr>
<tr><td>14.</td><td>Matambiko</td><td>( )</td></tr>
<tr><td>15.</td><td>Lugha inayotumiwa na watu wa Afrika Mashariki</td><td>( )</td></tr>
<tr><td>16.</td><td>Mambo yanayofanywa na jamii mara kwa mara</td><td>( )</td></tr>
</table>

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Faini | tozo anayolipishwa mtu baada ya kubainika katenda kosa fulani |
| Fasihi | sanaa ya lugha inayotumia maneno ili kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa |
| Ghibu | isiyoonekana kwa macho |
| Hadhara | mkusanyiko wa watu wengi |
| Sanifu | kuondoa kasoro katika lugha na kuifanya iwe rasmi na hivyo kukubalika na walio wengi |
| Weledi | ni hali ya kuwa na maarifa makubwa kuhusiana na kitu au jambo fulani |
| Chapuo | tangaza sifa za mtu au kitu |
| Jandoni | mahali ambapo watoto wa kiume hukaa na kutahiriwa ambapo hupata pia mafunzo kuhusu maisha |
| Unyago | mafunzo ya nadharia na vitendo yanayohusu malezi kwa wasichana kuhusu mila na desturi za jamii zao |



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 39 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tano

## Uhusiano wa Tanzania na nchi za Ulaya na Asia kabla ya ukoloni

Ulipokuwa darasa la nne, ulijifunza dhana ya uhusiano na chimbuko la ukoo. Pia, ulijifunza jamii za kale za ujima na ukabaila. Katika sura hii utajifunza sababu za uhusiano wa Tanzania na nchi za Ulaya na Asia kabla ya ukoloni. Kabla ya ukoloni jamii za kale za Tanzania zilijulikana kama jamii za Pwani ya Afrika Mashariki. Vilevile, utajifunza athari za uhusiano katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

### Sababu za ujio wa watu kutoka Asia

Katika karne ya 9, Pwani ya Afrika ya Mashariki ilitembelewa na watu kutoka bara la Asia. Wengi wa wageni hao walikuwa ni wafanyabiashara kutoka India, China na nchi za Kiarabu hasa Omani na Ghuba ya Uajemi. Ujio wa wageni kutoka nchi hizo ndio ulikuwa ni mwanzo wa uhusiano kati ya jamii za Pwani ya Afrika Mashariki na zile za bara la Asia. Sababu kuu ya uhusiano huu ilikuwa ni ya kiuchumi. Wafanyabiashara walifuata dhahabu na pembe za ndovu. Biashara ya dhahabu ilifanyika katika mji wa Kilwa. Pembe za ndovu zilipatikana kutoka sehemu mbalimbali karibu na pwani. Bidhaa nyingine zilizopatikana sehemu hizo ni nta, watumwa, mpira, ngozi ya chui na mikoko. Wafanyabiashara hawa walileta nguo, shanga, vikombe, visu, sabuni na vyombo vya nyumbani.

### Sababu za ujio wa watu kutoka Ulaya

Jamii za Pwani ya Afrika Mashariki zilihusiana na nchi za Ulaya katika biashara mbalimbali. Watu wa kwanza kutoka Ulaya kuja kufanya biashara Pwani ya Afrika Mashariki walikuwa Wagiriki na Warumi enzi za kale. Baada ya hapo walifuata Wareno. Wareno walifika maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki mwaka 1498 wakiongozwa na kiongozi wao Vasco da Gama. Wareno walifika katika mji wa Kilwa mnamo karne ya 16. Baada ya kufika, walieneza utawala wao sehemu yote ya Pwani ya Afrika ya Mashariki. Makao yao makuu yalikuwa Mombasa. Katika mji huo walijenga ngome kuu iliyoitwa Ngome ya Yesu (Fort Jesus).



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 40 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE



**Kielelezo namba 1:**Vasco da Gama

Wareno walitaka kumiliki biashara kati ya Pwani ya Afrika ya Mashariki na Asia, hasa biashara ya dhahabu na pembe za ndovu. Himaya ya Wareno katika Pwani ya Afrika ya Mashariki ilidumu hadi mwishoni mwa karne ya 17. Mwanzoni mwa karne ya 18, Waarabu wa Omani wakisaidiana na Waswahili wa pwani, walifanikiwa kuwafukuza Wareno. Lengo la Waarabu wa Omani lilikuwa kumiliki biashara katikati ya Pwani ya Afrika ya Mashariki, Asia na Ulaya. Wareno walikimbilia Msumbiji Kusini mwa mto Ruvuma.

Uhusiano wa kibiashara baina ya nchi za Ulaya na Pwani ya Afrika Mashariki uliimarika zaidi katika karne ya 19. Kipindi hicho nchi za Ulaya zilikuwa zimeingia katika mapinduzi ya viwanda; kwa hiyo walihitaji malighafi na masoko ya bidhaa zao. Hali hii ilisababisha ujio wa Wajerumani, Wafaransa na Waingereza. Aidha, mafanikio ya biashara kati ya pande hizi mbili yalifanywa kupitia mikataba baina yao na Sultani wa Zanzibar. Sultani huyu aliwapa fursa ya kuendesha biashara katika himaya yake. Sultani alikuwa kiunganishi cha biashara baina ya nchi za Ulaya na watawala wa bara hadi kufikia Kusini mwa Tanzania. Sultani wa Zanzibar alikuwa na uhusiano mkubwa wa kibiashara sehemu nyingi za jamii za bara. Sehemu hizo ni kama vile sehemu za kandokando ya mto Pangani hadi mlima Kilimanjaro. Sehemu nyingine ambazo Sultani wa Zanzibar alikuwa na uhusiano nazo kibiashara ni kama vile Ujiji na Karagwe. Uhusiano kati ya Sultani na jamii za bara uliwanufaisha wafanyabiashara wa Ulaya. Wafanyabiashara hao walitumia miundombinu ileile iliyotumiwa na wafanyabiashara wa Kiafrika na Kiarabu katika shughuli zao.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 41 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Bidhaa za biashara kati ya jamii za Pwani ya Afrika Mashariki, Ulaya na Asia

Wafanyabiashara walileta bidhaa mbalimbali kama vile nguo, bunduki, risasi, vinywaji na vyombo vya nyumbani kama bilauri, sahani, bakuli na vikombe. Vilevile, bidhaa za urembo kama pete na bangili.




**Kielelezo namba 2:** Baadhi ya bidhaa kutoka Ulaya na Asia

Aidha, kutoka Pwani ya Afrika Mashariki walichukua pembe za ndovu na dhahabu. Bidhaa kutoka kwa Wareno zilikuwa na thamani ndogo ukilinganisha na zilizotoka Pwani ya Afrika Mashariki. Wafanyabiashara wa kireno walipata faida kubwa kwa hivyo makundi ya wafanyabiashara yalivutiwa kuja katika eneo la Afrika Mashariki.




**Kielelezo namba 3:** Baadhi ya bidhaa kutoka jamii za Pwani ya Afrika Mashariki

## Njia walizopitia wafanyabiashara

Wafanyabiashara kutoka Ulaya na Asia walitumia usafiri wa meli kupitia Bahari ya Atlantiki na Bahari ya Hindi. Njia hii ilifanikisha shughuli zao za kibiashara. Wakiwa Pwani ya Afrika Mashariki walitumia njia zilizotumiwa na misafara ya watumwa, kufikia bidhaa mbalimbali walizokuwa wanazihitaji na masoko ya bidhaa walizoleta. Ili kufanikisha biashara yao, waliwatumia Wahindi na Waarabu.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 42 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 4:** Ramani ya Dunia kuonesha njia walizopita Wareno kwenda India



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 43
30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Kufikia karne ya 16 njia za bahari kuelekea maeneo ya Asia Mashariki zilitumika kwa ajili ya biashara. Njia za kupitia Kusini mwa Afrika na Amerika Kusini zilikuwa zikidhibitiwa na Wareno na Wahispania. Meli kubwa zilibeba bidhaa kutoka Afrika na kwenda Ulaya.

## Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua jibu sahihi.**

1. ____________ ni lengo la Waarabu wa Omani kuja Pwani ya Afrika Mashariki.

   (a) Kilimo (b) Uvuvi ( )

   (c) Biashara (d) Upagazi

2. Wareno walifika Pwani ya Afrika Mashariki mwaka:

   (a) 1540 (b) 1498 ( )

   (c) 1497 (d) 1690

3. Wareno walifika katika mji wa Kilwa mnamo karne ya:

   (a) 15 (b) 16 ( )

   (c) 18 (d) 19

4. Mreno wa kwanza kufika Pwani ya Afrika Mashariki alijulikana kwa jina la:

   (a) William Mackinnon ( )

   (b) Charles Stokes

   (c) Vasco da Gama

   (d) Karl Peters

5. Wafaransa walipanua wigo wa biashara zao katika Pwani ya Afrika Mashariki karne ya:

   (a) 19 (b) 17 ( )

   (c) 18 (d) 16

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 44 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Athari za biashara kabla ya Ukoloni

Zifuatazo ni baadhi ya faida na hasara za biashara kabla ya kipindi cha ukoloni:

**Faida**

(a) Ujio wa Waarabu na Wareno ulisaidia kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili, dini ya kiislamu na mila za Kiarabu kama vile kuvaa baibui.

(b) Kuingia kwa mazao mapya ya chakula na matunda katika jamii za Pwani ya Afrika Mashariki mfano mahindi, mananasi, mapapai na mapera.

(c) Kupata bidhaa muhimu kama vile nguo na vyombo vya nyumbani.

**Hasara**

(a) Kudhoofisha tamaduni za asili na kuthamini za wageni.

(b) Kuporomoka kwa tawala za jadi.

(c) Kukua kwa biashara isiyokuwa na usawa kati ya jamii za Tanzania, Asia na Ulaya. Bidhaa kutoka Ulaya zilikuwa na thamani ndogo ukilinganisha na bidhaa walizochukua kutoka jamii za Tanzania.

(d) Baadhi ya wafanyabiashara wa kigeni walivamia vijiji na kuwachukua watu kama watumwa. Wakati mwingine viongozi au watawala wa jamii fulani walishiriki kwenye biashara ya utumwa. Watawala hao walianzisha vita dhidi ya jirani zao kwa minajili ya kuteka watu wa kuwauza utumwani. Katika vita hivyo, baadhi ya wanajamii walikufa kwa kupigwa risasi, njaa na kiu.

(e) Kupoteza mamilioni ya watu wenye nguvu kutokana na kukamatwa kwa vijana na wanaume wenye nguvu. Vilevile, vifo vya wenyeji vilivyotokana na vita baina ya Waarabu na Wareno.

## Uhusiano wa kisiasa kabla ya ukoloni

Kabla ya ukoloni, uhusiano kati ya jamii za Ulaya na Asia na jamii za Pwani ya Afrika Mashariki ulikuwa zaidi kibiashara kuliko kisiasa. Hata hivyo, wafanyabiashara wa Ulaya walilazimika kuingia mikataba na makubaliano ya kisiasa na watawala wa jadi, ili kufanya biashara katika maeneo yao kwa kigezo cha kulipa kodi au hongo waliyokubaliana. Viongozi wa jadi walihusika kutoa ruhusa kwa wafanyabiashara kutoka Ulaya na Asia ili waweze kupita na misafara yao katika maeneo waliyokuwa wakitawala.



FOR ONLINE USE ONLY

MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 45 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Vitangulizi vya mwanzo vya ukoloni

Katika kufanikisha adhma ya wakoloni kuingia Afrika, mataifa ya Ulaya yalitanguliza vitangulizi vya ukoloni. Hii ilitumika kama mbinu ya kurahisisha ujio wao. Vitangulizi vya ukoloni vilikuwa ni pamoja na:

### (a) Wapelelezi

Wapelelezi ni miongoni mwa watangulizi wa mwanzo wa ukoloni. Wapelelezi hawa walifika Afrika Mashariki katika karne ya 19. Mwanzoni wapelelezi hao walitumiwa na vyama au makampuni ya Ulaya. Kuanzia katikati ya karne ya 19 Waingereza, Wafaransa, Wabelgiji na Wajerumani waliingia kwa wingi Pwani ya Afrika Mashariki. Wapelelezi hao walikuja kwa malengo yafuatayo:

(i) Kutafuta ardhi kwa ajili ya kilimo cha mazao ya biashara kama vile pamba na kahawa.

(ii) Kutafuta maeneo yenye hali nzuri ya hewa kwa ajili ya makazi ya wazungu na sehemu zenye madini, maziwa na mito.

(iii) Kuchunguza tamaduni za wenyeji na uimara wa tawala zao za jadi.

(iv) Kuchunguza bidhaa zilizopatikana Afrika Mashariki na zilizohitajika Ulaya.

(v) Kutafiti na kujua sehemu zilizokuwa na idadi kubwa ya watu.

Miongoni mwa wapelelezi waliofika Tanganyika walikuwa Richard Burton, John Hanning Speke, Daktari David Livingstone, Henry Morton Stanley na Joseph Thompson.

Safari za Wapelelezi zilianzia Zanzibar ambapo Sultani Seyyid Said aliwapa vibali na maelekezo muhimu kuhusu sehemu walizokusudia kutembelea. Wapelelezi hawa walitumia njia za misafara ya biashara ya watumwa kufika maeneo mbalimbali katika nchi yetu. Walipokuwa wanapita walikutana na watawala mbalimbali. Watawala hao walikuwa Mtemi Mirambo wa Unyamwezi, Mangi Horombo wa Uchaga, na Mkama Rumanyika wa Karagwe. Wapelelezi waliyaandika yote waliyoyaona na kutuma kwao. Kwa hiyo, wakoloni walipokutana na kuamua kugawana Afrika kati yao walikuwa wameshaijua Afrika kupitia ripoti walizokuwa wamezipata.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 46 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 5:** Ramani kuonesha njia walizopita wapelelezi

Taarifa za kipelelezi zilikuwa na mambo muhimu ya kusaidia nchi za Ulaya kuitawala Afrika ikiwemo Tanganyika. Baadhi ya taarifa hizo ni;

(i) Utajiri wa maliasili zilizokuwepo.
(ii) Ardhi yenye rutuba.
(iii) Hali ya hewa inayofaa kwa makazi ya Wazungu.
(iv) Tamaduni na tabia za wenyeji, pamoja na uimara wa tawala zao.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Taarifa hizi za wapelelezi zilisaidia mataifa ya Ulaya kufanya uamuzi wa kuvamia na kuchukua maeneo mbalimbali Barani Afrika. Pia, kutumia taarifa hizi ilikuwa rahisi kwa wafanyabiashara kuamua aina ya bidhaa na masoko yanayoweza kuwatajirisha kwa haraka zaidi. Kwa muktadha huu, walowezi na wafanyabiashara walianza kuja kwa wingi mwanzoni mwa miaka ya 1880 kwa nia ya kuzitumia fursa zilizoonekana.

**(b) Wamisionari**

Wamisionari walianza kuingia Tanganyika mwaka 1844 kupitia Zanzibar baada ya kupata vibali na vitambulisho kutoka kwa Sultani. Wamisionari waligharamiwa na vyama mbalimbali vya kidini kutoka Ulaya. Kwa mfano Johann Ludwig Krapf na Johannes Rebmann waligharamiwa na chama cha Church Missionary Society (C.M.S) kwenda Zanzibar na baadaye kuelekea Bara. Mwaka 1863 mapadre wa Shirika la Roho Mtakatifu walifuatia na kujenga kituo Zanzibar na baadaye Bagamoyo. Mwaka 1968 wamisionari wa chama cha Universities Mission to Central Africa (UMCA) walijenga vituo. Vituo hivyo vilijengwa Zanzibar, Magila katika mkoa wa Tanga na Masasi. Wamisionari wa White Fathers walifika mwaka 1870 ambao walijenga vituo vya Ujiji, Unyanyembe, Karema na Mwanza.

Wamisionari walipinga na kukomesha biashara ya watumwa. Waliamini kwamba, biashara ya utumwa ilikuwa kipingamizi kikubwa kwa maendeleo ya ubepari wakati huo. Hivyo, ilikuwa ni lazima kukomesha biashara hiyo ili wazalishaji mali wabaki nchini mwao. Walianza kuzalisha mazao yaliyohitajika katika nchi za kibepari. Malengo mengine ya Wamisionari yalikuwa ni:

(i) Kueneza dini ya Kikristo na kutoa elimu iliyojikita katika ufundishaji wa kusoma, kuandika na kuhesabu.

(ii) Kueneza utamaduni wao. Waliamini kwamba utamaduni wao ulikuwa bora kuliko ule wa Waafrika.

(iii) Kushawishi wafanyabiashara kutoka Ulaya kuja kufanya biashara Tanganyika.

(iv) Kuanzisha kilimo cha mazao muhimu.

(v) Kuwaandaa Waafrika kupokea mfumo wa uchumi wa kibepari.

**(c) Wafanyabiashara**

Nchi za Ujerumani, Ufaransa, na Uingereza zilidhamiria kueneza biashara mbadala wa ile ya utumwa ambayo ilikinzana na malengo yao ya muda mrefu baada ya mapinduzi ya viwanda. Wafanyabiashara hawa waliingia mikataba mbalimbali ya biashara na Sultani wa Zanzibar Seyyid Said.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mikataba hii iliwapa nafasi nzuri ya kuendesha biashara katika nchi hii. Miongoni mwa wafanyabiashara maarufu waliofanya biashara na jamii za Kitanzania ni Mwingereza aliyejulikana kwa jina la William Mackinnon. Hata hivyo, mfanyabiashara huyu hakufanikiwa sana kibiashara kwa kuwa alikosa ushirikiano kutoka kwa serikali yake ya Uingereza. Mfanyabiashara mwingine alikuwa ni Charles Stokes kutoka Uingereza. Huyu alifanya biashara maeneo ya Unyanyembe. Aidha, Charles Stokes alifanikiwa zaidi kibiashara kwa sababu alijiepusha na migogoro na Waarabu. Pia, alitengeneza urafiki na Wanyamwezi wa Unyanyembe.

Wafanyabiashara wa Kijerumani walikuja kuanzia mwaka 1884. Mjumbe wao wa kwanza aliyetumwa kuja kufanya mikataba na machifu alikuwa Carl Peters. Huyu alitumwa na kampuni yake ya biashara iliyoitwa Kampuni ya Wajerumani ya Afrika Mashariki. Miongoni mwa machifu aliofanya nao mkataba ni Chifu Mangungo wa Msovero, Usagara. Mkataba huu ni mfano wa mikataba ya kilaghai ambayo wafanyabiashara walifanya na viongozi wa jamii za Kitanganyika ili kuhalalisha ukoloni. Kwa mfano katika mkataba huu, Carl Peters alimhonga Chifu Mangungo kwa kumpa nguo na vitu vingine. Akamwahidi kumpa vitu vingi vya anasa ili akubali kuiuza nchi yake. Kwa kuwa chifu Mangungo hakujua lugha ya kigeni hakuelewa hila na ubaya wa mikataba hiyo hivyo alikubali.

**Kazi ya kufanya**

Jadili na wanafunzi wenzako athari mbalimbali zilizojitokeza kutokana na ujio wa wapelelezi, wafanyabiashara na wamisionari.

## Matokeo ya uhusiano kati ya jamii za Ulaya na Asia na Tanzania kabla ya ukoloni

(a) Kukomeshwa kwa biashara ya utumwa iliyokuwa inaendeshwa na Waarabu.

(b) Kueneza dini ya kikristo na kuanzisha shule kwa ajili ya kuwafundisha Waafrika kusoma, kuandika na kuhesabu kwa madhumuni ya kupata watumishi wa ngazi za chini ili kusaidia kuendesha shughuli za kiofisi na serikali kwa ujumla.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 49 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Kuanzisha kilimo cha mazao ya biashara kama pamba na kahawa.

(d) Ujio wa ukoloni. Uhusiano huu ulipelekea Wazungu kuanzisha mfumo wa ukoloni ili kufaidi zaidi mali zetu.

## Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja faida tatu na hasara tatu za biashara zilizotokana na uhusiano baina ya jamii za Pwani ya Afrika Mashariki na nchi za Ulaya na Asia kabla ya ukoloni.
2. Orodhesha watu kutoka Ulaya kuja Pwani ya Afrika Masharikii karne ya 19 kabla ya ukoloni.
3. Taja wapelelezi wawili waliofika Pwani ya Afrika Mashariki.
4. Kwa nini William Mackinnon hakufanikiwa katika biashara?

## Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja mashirika mawili ya kimisionari yaliyotuma wawakilishi wao kuja Tanganyika.
2. Orodhesha bidhaa zilizochukuliwa na Wareno kutoka jamii za Pwani ya Afrika Mashariki kabla ya ukoloni.
3. Ni kwa namna gani uhusiano kati ya Sultani wa Zanzibar na jamii za bara uliwanufaisha wafanyabiashara wa Ulaya?
4. Eleza kazi tatu walizofanya wapelelezi.
5. Eleza uwiano wa thamani kati ya bidhaa zilizotoka Pwani ya Afrika Mashariki na zile zilizotoka Ulaya na Asia.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Ukoloni | mtindo wa nchi au Taifa kuitawala nchi nyingine kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni |
| Ujima | ni mfumo wa maisha ya watu wanaoishi na kumiliki rasilimali kwa pamoja |
| Ukabaila | ni mfumo wa kiuchumi ambao watu wachache humiliki mali kama vile ardhi/wanyama kwa manufaa yao binafsi |
| Mkataba | makubaliano yanayofikiwa kwa maandishi kati ya pande mbili au zaidi ambayo yanatekelezwa na pande husika kwa mujibu wa taratibu na sheria |



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 50 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Sita

## Jinsi wakoloni walivyogawana Afrika

Katika sura ya tano, umejifunza uhusiano wa Tanzania na nchi za Ulaya na Asia kabla ya ukoloni. Katika sura hii, utajifunza jinsi wakoloni walivyogawana Afrika. Vilevile, utajifunza sababu za kugawana makoloni, maeneo yaliyogombewa zaidi na mgawanyo wa Afrika Mashariki.

### Sababu za kugawana makoloni

Maendeleo ya viwanda katika nchi za Ulaya yalisababisha ushindani miongoni mwa mataifa ya kibeberu katika robo ya mwisho ya karne ya 19. Ushindani na mgogoro mkubwa miongoni mwao ulikuwa katika namna ya kupata masoko ya bidhaa za viwandani. Vilevile kupata malighafi, vibarua wa gharama nafuu na maeneo ya kuwekeza vitega uchumi. Ushindani katika kupata mahitaji haya ulisababisha wasiwasi mkubwa baina ya mataifa ya Ulaya. Hali hii ilitishia amani na kuonesha hatari ya kutokea vita baina yao. Kutokana na hali hiyo kiongozi wa Ujerumani Kansela Otto von Bismark aliamua kuitisha mkutano haraka huko Berlin ili kuepusha janga la vita.



**Kielelezo namba 1:** Kansela Otto von Bismark



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 51 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mkutano wa Berlin ulianza mwezi Novemba 1884 na kumalizika mwezi Februari 1885. Mataifa yaliohudhuria mkutano huo ni Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Ubelgiji, Hispania, Ureno, Italia, Marekani, Denmark, Uholanzi, Urusi, Uturuki, Austria-Hungary na Uswisi. Mataifa haya ya kibeberu yalikubaliana na kuweka masharti kuhusu jinsi ya kuigawa Afrika. Masharti hayo yalikuwa:

(a) Taifa lolote lililoshika sehemu yoyote ya pwani ya Afrika kama ilivyo kwa Afrika Mashariki ya Wajerumani, ni lazima litoe taarifa kwa nchi nyingine za Ulaya.

(b) Taifa la Ulaya lazima lioneshe uwezo wa kutawala sehemu inayolimiliki. Hivyo lilitakiwa liwe na jeshi imara lenye uwezo wa kuzuia upinzani wa wenyeji katika shughuli zao na ulinzi wa walowezi.

(c) Mfalme Leopold wa Ubelgiji alitambuliwa kuwa mtawala wa Kongo na Waingereza walitambuliwa kuwa watawala katika eneo la mto Niger. Lakini mataifa yalikubaliana kuwa mito mikubwa kama Niger, Kongo, Senegal na Zambezi itumike kwa usafiri na iwe wazi kwa mataifa yote.

(d) Kukomesha biashara ya utumwa ndani ya makoloni yao.

Kumalizika kwa Mkutano wa Berlin mwaka 1885, kulianzisha mapambano na uvamizi wa Bara la Afrika ikiwemo Afrika Mashariki ya Wajerumani. Mabeberu walianza kuchukua maeneo yaliyokuwa chini ya Waafrika. Uchukuaji huo ulifanyika katika maeneo ambayo Wamisionari, Wapelelezi na Wafanyabiashara walikuwepo na kusaini mikataba.

## Mbinu zilizotumiwa na Mabeberu

Mabeberu walitumia makampuni ya kibiashara katika kueneza na kusimamia utawala wa kikoloni. Mfano mojawapo wa makampuni hayo ni Kampuni ya Wajerumani ya Afrika Mashariki iliyokuwa chini ya Carl Peters na Kampuni ya Waingereza ya Afrika Mashariki iliyokuwa chini ya William Mackinnon.

Mabeberu na makampuni yao mwanzoni walitumia ulaghai wa mikataba. Wananchi walipogundua ulaghai huo, walikataa kuheshimu mikataba hiyo. Ndipo mabeberu walipoanzisha vita vya uvamizi dhidi ya upinzani huo. Vita hivyo, vililenga katika maeneo ambayo yalikuwa hayajaingiliwa na mabeberu wengine pamoja na kuimarisha tawala zao.



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 52 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Mkutano wa Berlini ulifanyika mwaka gani?
2. Mtawala wa Kongo alijulikana kwa jina gani?
3. Taja mito mitatu iliyoamuliwa kutumika kwa usafiri kwenye mkutano wa Berlin.
4. Eleza mbinu zilizotumika na mabeberu kuvamia Afrika Mashariki.
5. Taja mataifa matatu ambayo hayakupata makoloni Afrika.

## Mapambano katika mgawanyo wa makoloni

Mapambano ya kuligawa Bara la Afrika yaliendelea hadi mwaka 1900. Kufikia mwaka huo, mgawanyo wa Bara la Afrika ulikuwa umekamilika. Uingereza ilikuwa imechukua nchi zifuatazo: Gambia, Sierra Leone, Gold Coast (Ghana), Nigeria, Afrika ya Kusini, Bechuanaland (Botswana) Rhodesia ya Kusini (Zimbabwe) Rhodesia ya Kaskazini (Zambia), Basoto (Lesotho) Swaziland, Nyasaland (Malawi), Zanzibar, British East Africa (Kenya), Uganda, sehemu ya Somalia, Sudan na Misri.

Ufaransa nayo ilipata makoloni yafuatayo: Tunisia, Algeria, Morocco, Kongo Brazaville, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Gabon na koloni la Afrika ya Magharibi ambalo baadaye liligawanywa katika makoloni ya Mauritania, Senegal, Guinea, Mali, Burkina Fasso, Ivory Coast, Niger, Dahomey na Chad. Wafaransa pia waliichukua sehemu ya Somalia.

Wabelgiji walichukua Kongo. Wajerumani walinyakua Kameruni, Togo, Namibia na Afrika ya Mashariki ya Wajerumani (Tanganyika, Burundi na Rwanda). Waitaliano walichukua Libya na sehemu ya Somalia. Wareno walipata Angola, Msumbiji, Guinea Bissau, visiwa vya Cape Verde, Sao Thome na Principe. Hispania ilishika Sahara ya Magharibi na Ikweta ya Guinea.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 53 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 2:** Ramani ya Afrika kuonesha ilivyokuwa imegawanywa kufikia mwaka 1914



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 54 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Maeneo yaliyogombewa zaidi

Baadhi ya maeneo yaligombewa zaidi na mataifa ya Ulaya kutokana na fursa zilizokuwepo katika maeneo hayo ambazo ni pamoja na:

(a) Ukanda wa pwani ambao ulikuwa na vituo muhimu vya kibiashara.

(b) Maeneo yenye rutuba na hali ya hewa nzuri kwa ajili ya kilimo na makazi. Maeneo hayo ni kwenye miteremko ya mlima Kilimanjaro na nyanda za juu Kusini. Maeneo mengine ni mto Kongo, mto Nile, delta ya Niger na mfereji wa Suez.

(c) Sehemu zenye maziwa makubwa na mito kwa ajili ya urahisi wa usafirishaji wa malighafi na bidhaa zao za viwandani. Katika Tanganyika walivutiwa zaidi na maeneo ya Ziwa Tanganyika, Nyasa na Ziwa Victoria.

(d) Ardhi yenye madini na rasilimali nyingine kama misitu na wanyama.

## Mgawanyo wa Afrika Mashariki

Baada ya makubaliano ya mkutano wa Berlin, hatua iliyofuata ilikuwa ni kugawana makoloni ya Afrika Mashariki baina ya mataifa ya kibepari. Wahusika wakuu waliogombania Afrika Mashariki walikuwa ni Wajerumani na Waingereza. Mgawanyo huo ulifanyika mwaka 1886 na 1890. Katika kugawa Afrika Mashariki, mikataba miwili ilitumika kati ya Wajerumani na Waingereza.

### (a) Mkataba wa mwaka 1886

Mwaka 1886 serikali ya Ujerumani, Uingereza na Zanzibar chini ya Sultani walikutana kwa lengo la kuigawa Afrika Mashariki kati ya mataifa hayo. Katika mkataba huo Wajerumani walipewa eneo la Tanganyika, Rwanda na Burundi ambalo liliitwa Afrika Mashariki ya Wajerumani. Pia, eneo la Witu hadi kaskazini mwa Mombasa lilitambuliwa kuwa chini ya Ujerumani. Waingereza wakapata Kenya. Sultani alibakiwa na eneo la Visiwa vya Pemba, Unguja na eneo la kilometa kumi na sita (16) Pwani ya Afrika Mashariki. Katika makubaliano hayo mataifa haya yalikubaliana kuwa hakuna kuingiliana tena katika maeneo yao waliyogawana.



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 55 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 3:** Ramani ya Afrika Mashariki baada ya mkataba wa 1886

## (b) Mkataba wa Heligoland wa mwaka 1890

Mkataba wa mwaka 1890 ulijulikana kuwa mkataba wa Heligoland ambao ulikuwa na lengo la kurekebisha ule wa mwaka 1886. Mkataba huu ulifanyika kati ya serikali ya Uingereza na Ujerumani. Madhumuni yake ilikuwa ni kurekebisha mipaka ya mwaka 1886 na kugawana upya sehemu zilizokuwa hazijagawiwa, mfano Uganda. Mkataba wa Heligoland ulihitimishwa na kuweka makubaliano kadhaa ili kuepuka mgogoro uliokuwepo. Makubaliano hayo yalikuwa:



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 56 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(i) Maeneo ya utawala kutoka mashariki mpaka magharibi mwa Ziwa Victoria yaliongezwa. Hivyo, Uganda ikawa chini ya Uingereza.

(ii) Ujerumani ilikubali Uingereza itawale Witu, Zanzibar na eneo lote lililokuwa chini ya himaya ya Sultani.

(iii) Uingereza ilikubali kuachia kisiwa cha Heligoland kilichopo Ujerumani katika bahari ya Kaskazini. Wajerumani walihitaji kisiwa hicho kwa sababu kilikuwa kituo muhimu cha jeshi la majini.




**Kielelezo namba 4:** Ramani ya Afrika Mashariki baada ya mkataba wa Heligoland mwaka 1890



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 57 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Kwa nini Kansela Otto Von Bismark wa Ujerumani aliitisha mkutano wa Berlin?
2. Mataifa matano yaliyohudhuria mkutano wa Berlin ni __________, __________, __________, __________ na __________.
3. Orodhesha makubaliano manne yaliyofikiwa katika mkutano wa Berlin.
4. Taja sifa za maeneo yaliyogombewa zaidi na mataifa ya kibepari.

**Zoezi la 3**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Mkutano wa Berlin ulikuwa na umuhimu gani kwa mataifa ya kibepari?
2. Toa sababu iliyofanya sehemu zenye maziwa na mito mikubwa kugombewa zaidi na wakoloni.
3. Tofauti na mkutano wa Berlin, taja mikataba miwili iliyohusika kuiweka Tanganyika chini ya utawala wa Kijerumani.

## Msamiati

Walowezi ni wavamizi katika nchi au taifa fulani katika nyanja za siasa, uchumi na utamaduni

Ubeberu mfumo wa kimataifa wa siasa uchumi wa uzalishaji mali wa kiwango cha juu kabisa cha ubepari ambapo mataifa tajiri huvuka mipaka yake na kwenda kunyonya uchumi wa nchi maskini

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 58 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Saba

## Mashujaa wa Afrika waliopinga uvamizi wa kikoloni

Katika sura hii utajifunza juu ya mashujaa wa Afrika, jinsi walivyopinga uvamizi wa kikoloni na sifa za mashujaa. Vilevile, utajifunza sababu za kupinga uvamizi wa Bara la Afrika na njia walizotumia mashujaa kupinga uvamizi huo. Mwisho utajifunza mchango wa mashujaa wetu katika kupinga uvamizi.

### Mashujaa wa Afrika

Mashujaa wa Afrika walikuwa viongozi wa mwanzo wa Bara la Afrika, waliopinga uvamizi wa wakoloni katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Wakoloni waliovamia Bara la Afrika ni baadhi ya mataifa ya Ulaya. Mataifa hayo yalikuwa ni Waingereza, Wajerumani, Wafaransa, Wabelgiji, Wareno, Waitaliano na Wahispania. Mashujaa wa Afrika walipinga uvamizi wa wageni kwa sababu hawakutaka kutawaliwa katika nchi zao. Pia, walipinga uvamizi huo kwa sababu, waliona kwamba wageni watakapovamia nchi zao watapora mali zao. Hivyo, mashujaa hawakukubaliana na hali hiyo na kuamua kutumia jitihada zao zote kupinga uvamizi wa wakoloni.

Baadhi ya mashujaa hao ni Urabi Pasha wa Misri dhidi ya Waingereza mwaka 1882 na Muhammad Ahmad wa Sudan dhidi ya Waingereza na Waturuki mwaka 1881. Halikadhalika Msiri wa Kongo (Zaire) dhidi ya Wabelgiji mwaka 1878, Mullah wa Somalia dhidi ya Waingereza mwaka 1885 na Mfalme Menelik wa II wa Ethiopia aliyewapiga Waitaliano mwaka 1893. Vilevile, Mkwawa mwaka 1891 na Machemba mwaka 1893 katika Afrika Mashariki ya Wajerumani dhidi ya Wajerumani. Mashujaa wengine katika Afrika Mashariki ya Wajerumani waliopinga uvamizi wa Wajerumani ni Abushiri na Bwana Heri katika maeneo ya Pwani mwaka 1888 hadi 1889, Mangi Sina wa Kilimanjaro mwaka 1891 na Mtemi Isike wa Tabora mwaka 1891.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 59 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Soma habari hii, kisha jibu maswali

Uvamizi wa wakoloni katika Bara la Afrika ulianza miaka ya 1870. Uvamizi huo ulifanywa na wageni kutoka mataifa ya Ulaya waliokuja Afrika kutafuta malighafi ya viwanda vyao. Hii ilitokana na kasi ya ukuaji wa viwanda huko Ulaya. Kukua kwa viwanda katika mataifa ya Ulaya kuliongeza uzalishaji mali kwa kiasi kikubwa.

Kutokana na ukuaji huo wa viwanda, wazungu walihitaji soko la kuuza bidhaa zao. Hivyo waliamua kuwa, sehemu mojawapo ya kupata malighafi za kutosha na kuuza bidhaa zao ni Barani Afrika.

Kati ya mwaka 1884 hadi mwaka 1885, mataifa ya Ulaya yaliamua kufanya mkutano uliolenga kuligawa Bara la Afrika. Mkutano huo ulifanyika nchini Ujerumani katika mji mkuu wa nchi hiyo yaani Berlin. Lengo la mkutano huo, lilikuwa ni kugawana makoloni katika Bara la Afrika, ambapo ingekuwa rahisi kwao kujipatia malighafi na masoko ya bidhaa zao. Miongoni mwa mataifa yaliyohudhuria mkutano wa Berlin ni Ubelgiji, Ufaransa, Hispania, Italia, Uingereza, Ujerumani na Ureno. Otto von Bismack aliyekuwa Kansela wa kwanza wa Ujerumani ndiye aliyeitisha mkutano wa Berlin.

Maeneo waliyovamia zaidi na kugawana yalikuwa ni: Kanda za Pwani ya Mashariki na Magharibi ya Afrika kwa sababu waliona ni rahisi kufanya biashara. Mfano wa maeneo hayo ni Zanzibar, Sofala nchini Msumbiji, Pate nchini Somalia, Lamu na Mombasa nchini Kenya. Maeneo mengine ni yale yenye rutuba na hali ya hewa nzuri. Maeneo haya yaliwafaa kwa kuishi, kulima na kufuga ili kupata malighafi kwa ajili ya viwanda vyao. Pia, walivamia maeneo yenye maziwa makubwa na mito ili waweze kusafirisha malighafi na bidhaa za viwandani. Miongoni mwa maeneo ya maziwa na mito yaliyovamiwa yalikuwa ni maeneo ya mto Niger huko Nigeria, maeneo yaliyopitiwa na mto Nile hasa nchini Misri na eneo la mto Kongo. Vilevile, maeneo yote ya maziwa makuu ya Afrika ya Mashariki, mfano Ziwa Victoria, Tanganyika na Ziwa Nyasa magharibi na kusini mwa Tanzania na Ziwa Edward na Albert nchini Uganda. Maeneo hayo yote yalikuwa na rutuba ya kutosha na madini mengi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo kulingana na habari uliyosoma.**

1. Toa sababu mbili zilizowafanya wakoloni kuvamia Bara la Afrika.
2. Orodhesha mataifa yaliyohudhuria mkutano wa Berlin mwaka 1884 hadi 1885.

**Kazi ya kufanya**

Chora Jedwali likionesha mashujaa wa Afrika waliopinga uvamizi, mwaka na maeneo yao ya utawala.

**Mfano:**

| Shujaa | Mwaka | Eneo |
|---|---|---|
| Urabi Pasha | 1882 | Misri |
| | | |

## Sifa za mashujaa wa Afrika waliopinga uvamizi

Mashujaa wa Afrika waliopinga uvamizi wa kikoloni walikuwa na sifa nyingi zilizodhihirisha ushujaa wao. Miongoni mwa sifa za mashujaa ni kuwa na moyo wa uzalendo. Walipenda amani, upendo na maendeleo. Pia, walikataa kutawaliwa, walipinga ukabila na walikuwa wanasiasa, hawakupenda dhuluma, walipenda amani na upendo. Aidha, hawakupenda unyonyaji, unyanyasaji, utegemezi na dhuluma.

Mashujaa wa Afrika walipinga uvamizi kwa sababu walipenda nchi zao, watu wao na rasilimali zilizokuwepo nchini mwao ili zisichukuliwe. Kwa kuwa mashujaa hao walikuwa na sifa hizo walijitoa muhanga kupinga uvamizi wa namna zote kutoka mataifa ya Ulaya.

## Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Toa sifa tano walizokuwa nazo mashujaa wa Afrika waliopinga uvamizi wa nchi zao.
2. Taja lengo la mkutano wa Berlin wa mwaka 1884 hadi mwaka 1885.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 61 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Jadili na wenzako katika kikundi athari za uvamizi wa wakoloni, kisha wasilisha darasani.

## Sababu za kupinga uvamizi katika Bara la Afrika

Zipo sababu mbalimbali zilizowafanya mashujaa kupinga uvamizi wa wakoloni katika nchi za Afrika, ambazo ni:

**(a) Kulinda uhuru**

Wavamizi walipokuja Barani Afrika, waliwatawala Waafrika katika nyanja kuu za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa kuwa kutawaliwa huku kuliwanyima uhuru wa kuendesha maisha yao katika nyanja hizo, hivyo mashujaa wa Afrika wakaona ni vyema kupambana na uvamizi huo ili kulinda uhuru wao ili wasitawaliwe na mataifa ya Ulaya.

**(b) Kupinga unyonyaji**

Viongozi wa Afrika walipinga unyonyaji uliofanywa na wavamizi. Hii ina maana kwamba, wavamizi walinunua bidhaa kutoka nchi za Afrika kwa bei ndogo, lakini waliuza bidhaa hizo kwa bei kubwa. Hii ilisababisha mashujaa wa Afrika kuamua kupambana nao na kuwaondoa Barani Afrika ili kulinda rasilimali za nchi zao na kuzuia unyonyaji.

**(c) Kupinga wavamizi waliopora na kumiliki rasilimali**

Wavamizi walipokuja Afrika walikuwa na tamaa ya kupora na kumiliki mali walizozikuta katika nchi za Afrika. Kutokana na tamaa zao, walimiliki rasilimali nyingi hasa ardhi kwa ajili ya kilimo cha mazao ya biashara kama vile chai, mkonge, kahawa na pamba ili waweze kupata malighafi kwa ajili ya viwanda vyao huko Ulaya. Wavamizi waliwatumia wananchi (manamba) kulima mashamba yao kwa ujira mdogo hasa katika mashamba ya mkonge.

**(d) Kupinga kutozwa kodi iliyoanzishwa na wavamizi**

Wavamizi walianzisha kodi katika makoloni ya Afrika pamoja na Afrika Mashariki. Wavamizi waliweka sheria kwamba, kila mwanaume mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea alitakiwa kulipa kodi ya kichwa, walioshindwa kulipa kodi walitumikishwa kufanya kazi katika mashamba na miundombinu.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 62 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(e) Kupinga uvamizi katika miliki ya biashara.**

Baadhi ya mashujaa kama vile Abushiri na Bwana Kheri walipinga Wajerumani kuhodhi biashara katika ukanda wa pwani ya Tanzania.

**Zoezi la 3**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja mambo matatu yaliyosababisha mashujaa wa Afrika kupinga uvamizi wa wakoloni.
2. Eleza ni kwa nini wavamizi kutoka mataifa ya Ulaya walipora na kumiliki ardhi kubwa Afrika.
3. Taja aina ya kodi iliyotozwa na wavamizi Afrika.

**Kazi ya kufanya**

Fikiria kwamba eneo mnaloishi na kuendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo, viwanda na biashara linavamiwa na wageni kutoka mataifa ya kigeni. Je, utakubaliana na hali hiyo? Kwa nini?

## Njia walizozitumia mashujaa kupinga uvamizi Barani Afrika

Njia zifuatazo zilitumika katika harakati za kupinga uvamizi wa wakoloni katika Bara la Afrika.

### Umoja

Ili wawe na nguvu ya kupambana na wavamizi, jamii za Afrika ziliungana ili kupinga uvamizi wa wakoloni. Mfano, nchini Kenya Mazrui aliweza kuwaunganisha makabila mbalimbali kupingana na uvamizi wa Waingereza katika eneo la Mombasa.

### Vita

Hii ni njia iliyotumiwa na mashujaa wa Afrika kuwapinga wakoloni. Mashujaa wa Afrika walipigana kwa kutumia silaha za jadi kama mikuki, ngao na mishale. Sehemu nyingine kama Ethiopia na Pwani ya Afrika Mashariki walitumia bunduki. Kiongozi wa Ethiopia kwa wakati ule alikuwa Mfalme Menelik wa II. Kiongozi huyu alikuwa imara kwa kuunganisha jeshi

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

lake kupigana na wavamizi Waitaliano na mwaka 1893 walishinda vita. Hii ilikuwa sababu iliyowafanya Waethiopia wasitawaliwe na wakoloni.

**Zoezi la 4**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja maeneo matano katika Afrika yaliyopigana kupinga uvamizi wa wakoloni.
2. Eleza njia moja iliyowasaidia mashujaa wa Afrika kupinga uvamizi.

**Kazi ya kufanya**

Wewe kama shujaa katika eneo unaloishi, eleza njia tano utakazozitumia kupinga uvamizi katika eneo unaloishi.

## Mchango wa mashujaa wa Afrika kupinga uvamizi

Mashujaa wa Afrika walifanya juhudi kubwa sana kupinga uvamizi wa wakoloni ili kulinda uhuru na kutetea maslahi ya nchi za Afrika. Katika harakati hizo za kupambana na wavamizi, mashujaa wa Afrika walifanya mambo mengi ili kufanikisha upinzani huo kama vile, kuleta umoja kwa kuunganisha jamii za Kiafrika kuwa kitu kimoja. Baadhi ya mashujaa walioweza kuunganisha jamii zao ni Mfalme Menelik wa II wa Ethiopia, Mkwawa wa Afrika Mashariki ya Wajerumani na Urabi Pasha wa Misri.

**Kazi ya kufanya**

Chora jedwali linaloonesha mashujaa waliosaidia kupinga uvamizi wa Mabeberu, mwaka/miaka na sehemu zao.

**Mfano**

| Kiongozi/ Shujaa | Sehemu | Mwaka |
|---|---|---|
| Mfalme Menelik wa II | Ethiopia | 1893 |
| Mkwawa | Tanganyika | 1891-1898 |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 5

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Katika kupambana na wavamizi, viongozi wa jamii za Afrika walifanya mambo kadhaa kuwang'oa wavamizi. Yataje
2. Ni kitu gani kiliwasaidia mashujaa wa Afrika kupinga uvamizi katika jamii zao?

## Zoezi la 6

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Ni kwa nini mkutano wa kuligawa Bara la Afrika uliitwa mkutano wa Berlin?
2. Wakoloni walipendelea zaidi maeneo ya namna gani? kwa nini?
3. Kama wewe ungekuwa ni miongoni mwa mashujaa wa Afrika ungetumia mbinu gani kupambana na wavamizi?

**Andika Ndiyo kama sentensi ni sahihi na Hapana kama sentensi si sahihi.**

4. Wavamizi kutoka mataifa ya Ulaya walikuja Afrika kuwasaidia Waafrika kukuza sekta ya kilimo, viwanda na biashara. ________
5. Patrice Lumumba alipinga uvamizi katika nchi ya Kongo. ____________
6. Tanganyika, Victoria, Nyasa, Edward na Albert ni maziwa makubwa yanayopatikana Afrika Magharibi. ____________
7. Mkutano wa Berlin uliitishwa na Kansela wa kwanza wa Ujerumani Otto von Bismark. ____________
8. Mashujaa wa Afrika waliopinga uvamizi walikuwa na sifa ya ujasiri, upendo, uzalendo, wapenda amani, wapenda maendeleo na kutopenda unyonyaji. ____________
9. Kodi iliyotozwa na Wajerumani Afrika Mashariki iliitwa kodi ya wanaume. ____________
10. Njia zilizotumiwa na wakoloni kuvamia Bara la Afrika ilikuwa njia ya amani. ____________
11. Msiri alipigana na Wabelgiji katika nchi ya Tanganyika. _______

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 65 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

12. Katika harakati za kupinga uvamizi Afrika mashujaa waliwezesha nchi za Afrika kuwa na umoja. ___________

**Chagua herufi ya jibu sahihi.**

13. Muhammad Ahmad alikuwa ni kiongozi wa nchi ya:
    (a) Rwanda
    (b) Burundi ( )
    (c) Sudan
    (d) Niger
14. Sababu ya wakoloni kuvamia ukanda wa pwani katika Afrika ilikuwa ni:
    (a) urahisi wa kufanya biashara
    (b) urahisi wa kuwasaidia watu ( )
    (c) urahisi wa kuendesha shughuli za kilimo
    (d) kurahisisha uchimbaji wa madini
15. Miongoni mwa mashujaa wa Afrika waliopinga uvamizi ni:
    (a) Agostino Neto, Kwame Nkrumah na Otto Von Bismack
    (b) Kwame Nkurumah, Isike, Seyyid Said ( )
    (c) Otto Von Bismack, Isike na Agostino Neto
    (d) Mfalme Menelik wa II, Msiri na Mkwawa.
16. Mkutano wa kuigawa Afrika ulifanyika katika nchi ya:
    (a) Uingereza
    (b) Marekani ( )
    (c) Ujerumani
    (d) Ufaransa

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Koloni | nchi inayotawaliwa na wageni |
| Mstari wa mbele | kuwa na bidii katika kufanya jambo fulani |
| Pora | chukua kwa nguvu bila ruhusa |
| Uzalendo | hali ya kupenda na kulinda nchi na mali zake |
| Mashujaa | viongozi Waafrika waliowaongoza wananchi wao kupambana kupinga uvamizi wa wakoloni |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Nane

## Utawala wa kikoloni

Katika sura ya saba, umejifunza jinsi mashujaa wa Afrika walivyopinga uvamizi wa kikoloni. Katika sura hii, utajifunza juu ya utawala wa kikoloni, Afrika Mashariki ya Wajerumani chini ya ukoloni wa Wajerumani, mgawanyo wa utawala wa Kijerumani, uchumi wa kikoloni katika utawala wa Kijerumani na vita vya Maji Maji vilivyoanza mwaka 1905 hadi 1907. Vilevile utajifunza ukoloni wa Waingereza na uchumi wa kikoloni chini ya Waingereza. Mwisho utajifunza harakati za ukombozi wa jamii za Watanganyika na ukombozi wa Zanzibar.

### Maana ya ukoloni

Ukoloni ni hali ambayo nchi moja huitawala nchi nyingine, kiuchumi, kisiasa na kijamii. Tanganyika ilitawaliwa na Wajerumani na Waingereza katika vipindi viwili tofauti. Utawala wa Afrika Mashariki uliwezeshwa na mikataba miwili baina ya Wajerumani na Waingereza kama tulivyoona huko nyuma.

### Afrika Mashariki ya Wajerumani chini ya ukoloni wa Wajerumani

Uvamizi wa Wajerumani katika Afrika Mashariki ya Wajerumani ulipitia hatua kuu tatu:

(a) Hatua ya kwanza ya uvamizi kati ya mwaka 1884 hadi 1887. Katika hatua hii ilisimamiwa na chama cha Kijerumani cha kutafuta makoloni.

(b) Hatua ya pili ilianza mwaka 1887. Katika hatua hii uvamizi ulisimamiwa na kampuni ya Kijerumani ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, kampuni hii ilipambana na matatizo makubwa ya upungufu wa fedha na upinzani kutoka kwa wenyeji.

(c) Katika hatua ya tatu uvamizi ulisimamiwa na serikali ya Kijerumani. Katika hatua hii serikali ya kijerumani ilimteua Gavana wa kwanza kusimamia utawala wa kikoloni. Gavana huyo aliitwa Julius Von Soden. Aliendeleza uvamizi na kufikia mwaka wa 1903 karibu sehemu zote za Tanganyika, Rwana na Burundi zilikuwa zimewekwa



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 67 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

chini ya utawala wa Kijerumani. Gavana alikuwa kiongozi mkuu wa koloni. Alikuwa mtawala mkuu na Amiri jeshi mkuu wa koloni. Alikuwa na baraza la kumshauri lililokuwa na wajumbe wa Kijerumani tu.

## Mgawanyo wa utawala wa Kijerumani

Wajerumani waligawanya koloni la Afrika Mashariki ya Wajerumani katika wilaya mbalimbali ili kurahisisha utawala. Ilipofika mwaka 1914 Afrika Mashariki ya Wajerumani ilikuwa imegawanywa katika wilaya ishirini na nne (24). Angalia kielelezo namba 1. Wilaya hizi zilikuwa chini ya Makamishna waliokuwa wakiishi makao makuu ya wilaya. Miongoni mwa majukumu ya Kamishna yalikuwa ni kutawala eneo husika lililokuwa chini yake.




**Kielelezo namba 1:** Ramani ya Afrika Mashariki ya Wajerumani kuonesha wilaya zote 24



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 68 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Aidha, wilaya hizo ziligawanywa katika sehemu ndogondogo za kiutawala chini ya uongozi wa Maakida au Maliwali. Wengi wao walikuwa Waarabu na Waswahili wachache kutoka Pwani waliopata nafasi za kuwa Maakida au Maliwali. Watawala wa jadi waliokuwa wenye nguvu waliendelea kuwa machifu wa Wajerumani. Wajumbe ambao walikuwa chini ya Maakida na Maliwali walisimamia vijiji. Kila Jumbe alitawala kijiji kati ya vijiji kadhaa vilivyokuwa chini ya Akida au Liwali.

Majukumu ya Maakida, Maliwali na Machifu yalikuwa kama ifuatavyo:

(a) Kukusanya kodi.

(b) Kuandikisha manamba na vibarua.

(c) Kutoa taarifa juu ya jambo lolote lisilo la kawaida au lililohatarisha usalama wa serikali ya kikoloni.




**Kielelezo namba 2:** Chati ya muundo wa utawala wa Wajerumani

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Kwa kushirikiana na wenzako, chora muundo wa uongozi wa Serikali ya Kijerumani kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Kijiji na muundo wa serikali wa sasa kuanzia ngazi ya wilaya hadi Kijiji/Mtaa.

## Uchumi wa kikoloni katika utawala wa Kijerumani

Madhumuni ya uvamizi wa Wajerumani yalikuwa ni kujinufaisha kiuchumi. Walilenga kupata masoko ya bidhaa zao za viwandani. Bidhaa hizo ni kama nguo, bunduki, mvinyo na vyombo vya nyumbani. Vilevile, kupata malighafi kwa gharama nafuu. Bidhaa walizochukua kutoka Tanganyika ni ngozi, mpira, nta, asali, pembe za ndovu, almasi na dhahabu.

Mwaka 1890 Wajerumani walianza kujenga njia za uchukuzi na mawasiliano chini ya idara ya ujenzi ambapo bandari za Tanga na Dar es Salaam zilianza kujengwa. Reli ya Tanga hadi Moshi ilianza kujengwa mwaka 1893 hadi 1911 wakati reli ya Dar es Salaam hadi Kigoma ilianza kujengwa mwaka 1905 hadi 1914.

## Kilimo

Wajerumani walianzisha shughuli za kilimo cha mazao ya biashara kama pamba, kahawa, mpira na mkonge. Mwaka 1902 kilijengwa kituo cha utafiti wa mazao Amani Usambara. Mwaka 1905 wakoloni walianzisha kilimo cha pamba Mwanza, Rufiji, Morogoro na Lindi. Baada ya vita vya Maji Maji mwaka 1905-1907 wananchi waliruhusiwa kulima mazao ya biashara. Mpira ulilimwa Bagamoyo, mkonge ulilimwa Tanga, Morogoro, Kilosa, Lindi na Mikindani, wakati kahawa ililimwa Kagera na Kilimanjaro.



**Kielelezo namba 3:** Mnyapara akisimamia vibarua wakati wa kukata mkonge

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 70 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja jina la Gavana wa Wajerumani aliyesimamia utawala wa kikoloni Afrika Mashariki ya Wajerumani.
2. Taja mazao yaliyolimwa katika mikoa ifuatayo katika kipindi cha ukoloni wa Wajerumani:
   (a) Morogoro ___________
   (b) Kagera na Kilimanjaro ___________
   (c) Mwanza ___________
   (d) Bagamoyo ___________
3. Reli ya Tanga hadi Moshi ilianza kujengwa mwaka gani?
4. Unafikiri ni kwa nini Wajerumani walitoza kodi?

## Elimu

Serikali ya kikoloni ya kijerumani ilidhamiria kukuza elimu katika Afrika Mashariki ya Wajerumani kwa kuelimisha Waafrika wachache baada ya vita vya Maji Maji ili wawasaidie katika shughuli zao za utawala. Shule ya kwanza ilianzishwa Tanga darasa la kwanza hadi la nne. Wengi wao walikuwa ni watoto wa machifu. Wale wote waliojua kusoma, kuandika na kuhesabu waliajiriwa katika ngazi za chini katika serikali ya kikoloni. Hadi ilipofika mwaka 1914 Wajerumani walikuwa na vituo 89 vyenye wanafunzi 8494. Wamisionari pia walipewa jukumu la kutoa elimu. Hadi kufikia mwaka 1914 Wamisionari walikuwa na vituo 1852 vyenye wanafunzi 108,550. Lugha ya kufundishia ilikuwa Kiswahili. Wazungu na Wahindi walipewa elimu iliyowatayarisha katika madaraka ya juu zaidi ya Waafrika serikalini. Wahindi waliandaliwa pia katika uendeshaji wa biashara. Katika shule nyingi elimu iliishia darasa la nne. Katika shule ya Tanga liliongezwa darasa la tano na sita ambako lugha ya Kijerumani ilifundishwa.

### Kazi ya kufanya

Jadili na wenzako kuhusu lengo la elimu ya kikoloni, kisha uandike katika daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 71 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mapambano dhidi ya ukoloni wa Kijerumani

Wajerumani walitumia zaidi ya miaka 15 kueneza na kuimarisha utawala wao Tanganyika. Katika kipindi chote hicho vikundi mbalimbali vya wenyeji vilipinga vikali utawala wa Wajerumani. Mifano michache kutoka sehemu za Tanganyika ni:

(a) Kanda ya Pwani

Maeneo ya ukanda wa Pwani, mapambano yaliongozwa na wafanyabiashara. Baadhi ya wafanyabiashara hao ni Abushiri bin Sultani wa Pangani na Bwana Heri wa Uzigua. Huyu alikuwa tishio kubwa kwa Wajerumani. Meja Von Wissmann alitumwa kutoka Ujerumani ili kuzuia upinzani huu. Kadiri vita ilivyozidi Abushiri aliishiwa wapiganaji na silaha na kukimbilia maeneo ya Usagara. Baadaye alishikwa na kunyongwa hadharani katika mji wa Bagamoyo. Bwana Heri pia aliwapinga Wajerumani lakini baada ya miezi sita tu alishindwa.

(b) Kanda ya Kaskazini

Sehemu ya ukanda wa Kaskazini, Wajerumani walipingwa na viongozi wa jamii ya Kichaga. Viongozi hao ni Mangi Sina wa Kibosho na Mangi Meli wa Moshi. Mangi Meli alipambana na majeshi ya Wajerumani kuanzia mwaka 1892. Alikamatwa na kunyongwa mwaka 1893 baada ya yeye kumuua kamanda wa Kijerumani Von Bullow.

(c) Kanda ya Magharibi

Jamii ya Kinyamwezi ilipinga uvamizi wa Wajerumani chini ya viongozi wao Mtemi Isike au Mwana Kiyungi na Mtemi Mirambo kuanzia mwaka 1886. Wajerumani walifanikiwa kuvunja ngome ya Isike. Mtemi huyu alijilipua yeye pamoja na familia yake kwa kutumia baruti.

(d) Kanda ya Kati

Kanda hii, Wagogo walipigana na Wajerumani chini ya watemi Kigole wa Kilimatinde na Sinyangaro katika mwaka 1893.

(e) Kanda ya Kusini

Katika kanda hii, Wahehe walitoa upinzani mkubwa dhidi ya Wajerumani. Kiongozi wa Wahehe alikuwa Mtwa Mkwavinyika

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 72 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mkwawa, tazama kielelezo namba 5. Chini ya uongozi wake, Wahehe walipigana na Wajerumani kuanzia mwaka 1891 hadi 1898. Mapigano ya kwanza yalitokea mwaka 1891 katika eneo lililoitwa Lugalo. Katika mapigano hayo Wajerumani walishindwa vibaya. Pambano la pili lilifanyika mwaka 1894, katika pambano hili, jeshi la Wajerumani lilishambulia ngome ya Mkwawa katika eneo la Kalenga. Aidha, katika pambano hilo Mkwawa na jeshi lake walishindwa hivyo aliamua kukimbilia porini na huko aliendeleza vita vya msituni. Mkwawa alipoona kuwa amezidiwa na kuwa alikaribia kutekwa na Wajerumani aliamua kujiua kwa kujipiga risasi mwaka 1898.

Mtawala mwingine wa jadi katika kanda ya kusini ni Mwene Machemba aliongoza Wayao katika mapambano na Wajerumani mwaka 1890. Wajerumani walimshinda Machemba katika mapambano ya mwaka 1899.



**Kielelezo namba 4:** Kiongozi wa Wahehe Mtwa Mkwavinyika Mkwawa

## Vita vya Maji Maji 1905-1907

Vita vya Maji Maji vilianza mwaka 1905 na kumalizika 1907. Vita hii iliitwa Maji Maji kutokana na imani kwamba risasi za Wajerumani zingebadilika na kuwa maji kama alivyofundisha Bwana Kinjekitile Ngwale. Kinjekitile alikuwa mganga wa jadi wa kabila la Wamatumbi lililoishi Ngarambe Kilwa mkoani Lindi. Vita vya Maji Maji vilienea hadi Kusini mwa Afrika Mashariki ya Wajerumani vikihusisha makabila ya Wangoni, Wamatengo,



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 73 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Wangindo, Wamatumbi, Wayao na Wabena. Vita hivi vilienea hadi Kaskazini Mashariki mwa Pwani ya Afrika Mashariki ya Wajerumani. Pia, maeneo ya Nandete huko Kilwa, Rufiji, Kilosa hadi Morogoro ambapo Waluguru, Wambunga na Wapogoro walishiriki. Wazaramo waliokuwepo Dar es Salaam nao waliingia katika mapigano. Vilevile, vilienea Songea hadi Njombe.




**Kielelezo namba 5:** Maeneo yaliyoathirika na Vita vya Maji Maji

## Sababu za kutokea kwa vita vya Maji Maji

(a) Kutokana na utawala wa mabavu na utumiaji wa nguvu kupita kiasi. Hata Machifu, Jumbe na Maakida walipigwa viboko hadharani kwa kutotimiza amri za wakoloni na walowezi.

(b) Unyanyasaji na ukandamizaji uliokithiri ambapo wenyeji walilazimishwa kuanzisha na kulima mashamba ya pamba. Pamba hiyo iliuzwa kwa Wajerumani kwa fedha kidogo sana. Wilaya ya Kilwa Wamatumbi walilazimishwa kufanya kazi ngumu katika



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 74 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mashamba ya pamba ya serikali majumbe na maakida walitumia mabavu na viboko katika kusimamia kazi hizo.

(c) Kulipa kodi kubwa ambapo wenyeji walilazimishwa kulipa kodi ya rupia tatu kwa mwaka. Mwanaume aliyeshindwa kulipa kodi hii, aliadhibiwa vikali kwa kupigwa viboko hadharani, kufungwa na kufanyishwa kazi ngumu.

(d) Ukatili wa Maakida na Jumbe katika usimamizi wa shughuli za Wajerumani.

(e) Unyang'anyi wa ardhi hasa zenye rutuba kutoka kwa wenyeji.

(f) Wajerumani kudharau utamaduni wa wenyeji, mfano ngoma za jadi, jando na unyago.

(g) Wajerumani kuruhusu Wamisionari kuchoma nyumba zilizokuwa zinatumiwa na waganga wa jadi kwa ajili ya matibabu.

(h) Tabia za majeshi ya Wajerumani na vijana wa kazi wa Wajerumani kuchukua wake za wenyeji.

(i) Ujira mdogo usiofanana na uzito wa kazi. Vibarua walilipwa fedha kidogo sana baada ya kufanyishwa kazi za sulubu. Vilevile, wenyeji walilazimishwa kufanya kazi kwa vipindi virefu katika mashamba ya walowezi.

Ingawa vita ilichukua miaka miwili (2) mwisho wake jamii za Afrika Mashariki ya Wajerumani zote zilishindwa.

## Sababu za kushindwa vita vya Maji Maji

(a) Silaha duni za wenyeji.

(b) Kukosekana kwa umoja imara baina ya wenyeji.

(c) Mawasiliano hafifu baina ya wapiganaji na wananchi.

(d) Tofauti baina ya viongozi wa vikosi vya wenyeji. Baadhi ya viongozi walikuwa vibaraka wa serikali ya Wajerumani.

(e) Uchumi hafifu.

## Matokeo ya vita vya Maji Maji

(a) Inaaminika kuwa, takribani watu kati ya 75,000 na 120,000 walipoteza maisha yao.

(b) Njaa ilienea maeneo yote yaliyoshiriki katika vita na watu wengi walikufa kwa njaa.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 75 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(c) Tawala nyingi za jadi zilisambaratika.

(d) Wajerumani walijifunza madhara ya ukatili na utawala wa mabavu.

(e) Vijana wengi walipoteza maisha hivyo, kupoteza nguvu kazi ya Taifa.

(f) Wajerumani walibadili sera na kuruhusu wenyeji kulima mazao ya biashara.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Orodhesha bidhaa zilizoletwa na Wajerumani nchini Tanzania.
2. Vita vya Maji Maji vilianza mwaka __________.
3. Wagogo walipinga uvamizi chini ya uongozi wa mtemi _______.
4. Mtwa Mkwavinyika Mkwawa alianza mapigano dhidi ya Wajerumani mwaka __________ katika eneo la __________.
5. Toa sababu za mapigano ya vita vya Maji Maji.

## Ukoloni wa Waingereza

Utawala wa Uingereza dhidi ya jamii za Watanganyika ulianza mwaka 1918, baada ya Wajerumani kushindwa vibaya katika vita kuu vya kwanza vya dunia iliyopiganwa kati ya mwaka 1914 hadi 1918. Vita hivi vilikuwa baina ya mataifa ya kibepari ya Ulaya ambayo yalisababisha ubeberu katika nchi zao na makoloni yaliyo chini ya utawala wao. Baada ya kushindwa huko, Ujerumani ilinyang'anywa makoloni yake yote. Eneo la Tanganyika liliwekwa chini ya utawala wa Waingereza kwa udhamini wa Umoja wa Mataifa uliofahamika kwa jina la League of Nations. Sir. Horace Byatt aliteuliwa kuwa Gavana wa kwanza Mwingereza mwaka 1920 akifuatiwa na Sir. Donald Cameroon mwaka 1925, Sir. Edward Twining mwaka 1948 na Sir. Richard Turnbul mwaka 1959 ambaye ndiye aliyekabidhi nchi ya Tanganyika kwa wananchi wake mwaka 1961 nchi ilipopata uhuru. Miaka ya mwanzoni ya utawala wa Waingereza walifuata utaratibu na mfumo wa Wajerumani lakini baadaye walibadilisha mfumo wa utawala.

Kwa ujumla Waingereza walitumia mfumo wa utawala tofauti na ule wa Wajerumani. Waingereza walitumia mfumo wa utawala wa kutumia utawala wa jadi wa Machifu wakati Wajerumani walitumia zaidi mfumo wa utawala wa moja kwa moja, yaani kwa kutumia Maafisa, Waarabu, Waswahili na Waafrika wachache wa pwani kama Maakida na Maliwali.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 76 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Waingereza




**Kielelezo namba 6:** Chati ya muundo wa Serikali ya Waingereza

Baada ya Malkia wa Uingereza, waziri wa makoloni ndiye aliyefuatia kimadaraka akisaidiwa na magavana wa makoloni. Koloni liligawanywa katika majimbo ambayo nayo yaligawanywa katika wilaya. Makamishna walioteuliwa na gavana ndiyo walikuwa watawala wa wilaya. Hadi ngazi ya wilaya uongozi wa Serikali ya kikoloni ulishikwa na Waingereza.

Ili kurahisisha utawala wa kikoloni, wilaya nazo ziligawanywa katika tawala za makabila zilizokuwa chini ya utawala wa jadi wa machifu. Watawala hawa wa jadi ambao walikuwa machifu walitofautiana majina kama Mtemi, Mangi, Mtwa, Nkosi au Mwene kulingana na tamaduni za kabila husika. Kazi kubwa ya watawala wa jadi ilikuwa ni kusimamia maagizo yote kutoka ngazi za juu kiutawala.



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 77 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Jadili na wenzako kazi za viongozi wa kikoloni katika serikali ya Waingereza kisha andika kwenye daftari lako la mazoezi.

## Elimu ya kikoloni wakati wa Waingereza

Kama ilivyokuwa wakati wa Wajerumani, elimu wakati wa ukoloni wa Mwingereza ilitolewa kwa wananchi wachache. Baadhi ya watoto walitoka katika familia za machifu na makarani wa ngazi ya chini walipewa kipaumbele. Madhehebu ya dini pia yalihusika katika jukumu la kutoa elimu kwa baadhi ya wananchi. Shule na vyuo vilijengwa na Serikali au Wamisionari katika maeneo yaliyokuwa yanazalisha malighafi. Elimu hii ya kikoloni ilikuwa mbadala wa elimu ya jadi iliyokuwa inatolewa kabla ya ukoloni. Kiwango cha elimu wakati wa Waingereza kilipanda hadi darasa la nane, kisha darasa la kumi na mwisho darasa la kumi na mbili kwa shule chache za sekondari.

## Malengo ya elimu ya kikoloni

(a) Kutoa ujuzi mdogo ili kuwezesha uzalishaji mali mashambani na usimamizi wa kilimo.

(b) Kupata watumishi watakaofanya kazi za maofisini kama makarani, matarishi na wasimamizi wa kazi.

(c) Kusomesha watu wachache hususani watoto wa machifu ili kuwasaidia wakoloni katika utawala wao.

Elimu ya kikoloni ilitolewa kwa lugha ya Kiswahili kuanzia darasa la kwanza hadi la tano. Darasa la sita hadi elimu ya vyuo ilifundishwa kwa lugha ya Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili. Watoto wa watawala wa jadi walitayarishwa kuwa waaminifu kwa serikali ya kikoloni.

Hata hivyo, elimu hii ilitolewa kibaguzi ambapo wazungu walipewa elimu bora zaidi wakifuatiwa na Wahindi na Waarabu, wakati Waafrika walipata elimu ya hadhi ya chini zaidi kuliko wote. Pia, elimu ya kikoloni iliwafanya Waafrika wachache waliopata elimu hiyo kuwadharau wale ambao hawakuipata. Vilevile, walipuuza mila na desturi za kiafrika na kuiga za kigeni kama vile mavazi, majina yao, lugha, burudani na tabia.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 78 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Uchumi wa kikoloni chini ya Waingereza

Uchumi wa kikoloni ulihusisha uzalishaji wa mazao ya biashara, ufugaji, madini na uuzaji wa bidhaa za viwandani kutoka nchi za Ulaya tangu miaka ya 1880. Madhumuni makuu ya uchumi wa kikoloni yalikuwa ni upatikanaji wa soko la bidhaa zao kutoka viwanda vya Ulaya, maeneo ya makazi kutokana na ongezeko la watu barani Ulaya na kupata maeneo mapya ya uwekezaji na uzalishaji usio na gharama kubwa.

## Njia zilizotumika kueneza uchumi wa kikoloni chini ya Mwingereza

Ili kueneza uchumi wa kikoloni chini ya Mwingereza, njia zifuatazo zilitumika:

(a) Kuharibu njia za uchumi wa asili, kwa mfano Waingereza waliua na kutokomeza biashara ya kubadilishana bidhaa miongoni mwa jamii za kitanzania. Pia, baadhi ya maeneo walikatazwa kufanya aina yoyote ya kilimo kwa wakulima wadogowadogo. Sababu ilikuwa ni kuwalazimisha kufanya kazi katika mashamba ya kikoloni ili walipwe fedha zitakazowasaidia kupata mahitaji muhimu kama vile chakula, malazi, mavazi na kulipa kodi. Pia, waliua viwanda vya asili kwa kupiga marufuku uzalishaji wa bidhaa kama vile mikuki, sime na majembe.

(b) Kuanzisha mfumo mpya wa uchumi, kwa mfano kuwa na mashamba makubwa ya mazao kulisaidia kujengwa kwa njia za usafirishaji na mawasiliano ambazo hazikuwepo kabla ya ukoloni. Hadi mwaka 1928, Waingereza walijenga kipande cha reli kutoka Tabora hadi Mwanza.

**Kazi ya kufanya**

Jadili na wenzako katika kikundi njia zilizotumika kueneza uchumi wa Waingereza kisha wasilisheni darasani.

## Sekta za uchumi wa kikoloni wa Waingereza

### Kilimo

Utawala wa Waingereza ulishurutisha kilimo cha mazao ya biashara kwa ajili ya malighafi katika viwanda vyao huko Ulaya. Wakoloni walisisitiza kilimo cha pamba maeneo ya Mwanza, Shinyanga, Tabora na Morogoro, kahawa maeneo ya Kilimanjaro, Tukuyu, Kagera na Mbinga. Korosho



FOR ONLINE USE ONLY

MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 79 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

ililimwa maeneo ya Mtwara, Lindi na Tunduru na tumbaku maeneo ya Urambo, Tabora, Songea na Iringa. Ufugaji na uvuvi pia ulifanyika katika maeneo mbalimbali ya koloni la Tanganyika.

Aidha, Walowezi walimiliki mashamba makubwa ya mkonge. Zao la mkonge lililimwa kandokando ya reli maeneo ya Tanga, Morogoro, Lindi na baadhi ya maeneo ya Kilimanjaro kama Makanya, Lembeni, Kisangara na Kiruru ili kurahisisha usafirishaji wa zao hilo. Miwa na chai ililimwa katika mikoa ya Morogoro, Arusha na Kagera.

Nguvukazi katika mashamba haya ilikuwa vibarua au manamba. Baadhi ya makabila yaliyofanya kazi kama vibarua katika mashamba haya ni Wasukuma, Wangoni, Wanyamwezi, Waha, Wafipa, Wamakonde, Wanyiramba, Wanyaturu na Warundi. Ilipofika mwaka 1948 maeneo kadhaa kama Kigoma, Ruvuma na Rukwa yalitengwa maalumu kama maeneo ya vibarua. Wakoloni waliunda mashirika kadhaa ya kutafuta vibarua. Manamba au vibarua walilipwa ujira mdogo ili wasijitosheleze na waendelee kufanya kazi kila siku ili kukidhi mahitaji yao.

**Viwanda**

Waingereza walianzisha viwanda vichache vya kuzalisha na kuongeza thamani ya bidhaa kwa mahitaji ya Wazungu, Wahindi na Waafrika wachache. Bidhaa hizo ni kama vile sigara, sabuni, nyama za kusindika na vinywaji kama soda na bia. Pia walianzisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ya biashara kama vile pamba, kahawa na tumbaku kwa ajili ya kuyaandaa kwa kusafirisha kwenda Ulaya. Lengo kuu la viwanda hivi lilikuwa kupunguza uzito wa malighafi hizo.

**Madini**

Shughuli za uchimbaji wa madini katika koloni la Tanganyika zilifanyika katika sehemu mbalimbali, kwa mfano uchimbaji wa almasi huko Mwadui, dhahabu huko Chunya na chumvi huko Bagamoyo. Makampuni ya madini yalimilikiwa na Wazungu.

**Biashara**

Biashara katika serikali ya kikoloni ilifanywa na Waasia kutoka India. Aidha, serikali ya kikoloni iliruhusu jamii ya kihindi kujishughulisha na biashara za rejareja na jumla.

Hata hivyo, kuna makampuni kadhaa ya Uingereza na Amerika kama BAT (British and America Tobacco) na Smith Mackenzie zilifungua matawi



FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

nchini Tanganyika. BAT ilijihusisha na biashara ya tumbaku wakati Smith Mackenzie ilijihusisha na usambazaji wa bidhaa kutoka viwanda vya Uingereza.

## Mbinu zilizotumika kujenga utawala katika kipindi cha ukoloni

Katika kujenga na kuimarisha utawala wa kikoloni mbinu zifuatazo zilitumika:

**Nguvu za kijeshi**: Matumizi ya nguvu za kijeshi yalitumika kueneza utawala wa kikoloni. Njia hii ilitumika baada ya wenyeji kugoma kusaini mikataba ya kilaghai au kutotii matakwa ya ukoloni.

**Kutumia viongozi wa jadi**: Wazungu waliamua kufanya urafiki na machifu wa jadi kwa kisingizio cha kuwalinda dhidi ya maadui. Viongozi wasaliti walirubuniwa na mabepari ili washirikiane nao kuwavamia na kuwatawala wenzao walioonesha upinzani mkali dhidi ya uvamizi wa kikoloni.

**Kwa kutumia vitisho**: Wakoloni waliwatisha wenyeji kwa kuzunguka zunguka na wanajeshi karibu na maeneo yao. Pia, waliwatisha kwa kuanzisha kambi za kijeshi, magereza na mahakama.

**Kwa kutumia elimu ya kikoloni:** Elimu ya kikoloni ilisaidia sana kujenga utawala wa kikoloni kwa kuwabadilisha au kupumbaza Waafrika kuona utawala wa kikoloni si mbaya. Na wale waliosoma kuwa sehemu ya utawala huo.

## Harakati za ukombozi wa jamii za Watanganyika

Harakati ya ukombozi ilikuwa dhamira ya jamii za Watanganyika kujitawala zenyewe na kutokomeza aina zote za ukandamizaji na unyonyaji wa kibepari.

## Harakati za mwanzo

Tangu awali katika kipindi cha uvamizi, jamii za Tanganyika zilipinga utawala wa wakoloni kwa njia mbalimbali kama tulivyoona katika kipindi cha vita vya Maji Maji. Njia nyingine ni pamoja na uanzishaji wa vyama vya wakulima sehemu za uzalishaji kama:

(a) Bukoba Buhaya Union (BBU) mwaka 1924

(b) Kilimanjaro Native Cooperative Union (KNCU) mwaka 1925

(c) Usambara Native Growers Association (UNGA) mwaka 1931

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 81 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Nyanza Cooperative Union (NCU) mwaka 1954

(e) Meru Growers Cooperative Union (MGCU) mwaka 1954

(f) Ngaka Coffee Growers (NCG) mwaka 1934

(g) Ushirika wa Wangoni na Wamatengo (Ngoni Matengo Co-operative Union) mwaka 1936

(h) Victoria Federation of Cooperative Union (VFCU) mwaka 1954

(i) Lake Province Growers Association (LPGA) mwaka 1949

(j) Bugufi Coffee Cooperative Society (BCCS) mwaka 1936

Lengo kuu la vyama hivi ilikuwa kupigania maslahi bora katika bei ya mazao wanayozalisha.

## Vyama vya wafanyakazi

Kulikuwa na baadhi ya makundi kama walimu, makarani, madereva, matarishi, wafanyakazi wa reli na wasomi mijini ambayo yalianzisha vyama kupigania maslahi bora kutoka kwa waajiri wao. Pia, walipigania elimu bora, bei bora ya mazao na kupinga ubaguzi katika maeneo ya kazi. Mfano, mwaka 1922, chini ya uongozi wa Bwana Martin Kayamba kilianzishwa chama cha watumishi wa serikali Tanganyika Territory African Civil Servant Association (TTACSA). Chama kingine cha Ushirikiano wa Waafrika (The African Association),kiliundwa mwaka 1929, mjini Dar es salaam.

Mwaka 1955 vyama vyote vya wafanyakazi viliunda chama kimoja cha wafanyakazi ili kuwa na umoja wa kitaifa. Shirikisho hilo lilipewa jina la Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi Tanganyika (Tanganyika Federation of Labour (TFL)) ambapo Bwana Rashidi Mfaume Kawawa alikuwa Katibu Mkuu.

## Vyama vya siasa

Kukithiri kwa unyonyaji hasa baada ya vita vya pili vya dunia kulisababisha kuzuka kwa harakati kadhaa za ukombozi wa nchi kwa kudai kupata uhuru. Katika mwaka 1929 chama cha Waafrika yaani African Association kilianzishwa. Chama hiki kilidai na kutetea haki za Waafrika. Mwaka 1948 kilibadili jina na kujiita Tanganyika African Association (TAA). Chama hiki kilikuwa na mchango mkubwa sana katika kukua kwa harakati za kudai uhuru hapa nchini. Tarehe 7 Julai



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 82 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mwaka 1954, TAA iliitisha mkutano mkuu kujadili katiba na muundo wake. Katika mkutano huo TAA ikazaa chama kipya cha siasa kilichojulikana kama Tanganyika African National Union (TANU) chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kama Rais wake. Kwa hiyo TANU ilizaliwa tarehe 7.7.1954. TANU ilijizatiti kuwaunganisha wananchi wa Tanganyika katika kupigania Uhuru wao.

Vyama vingine vilianzishwa vilikuwa African National Congress (ANC) chini ya uongozi wa Bwana Zuberi Mtemvu mwaka 1958 baada ya kutokea kutoelewana ndani ya TANU. Vilevile United Tanganyika Party (UTP) kilichoanzishwa mwaka 1959 na Wazungu.

Katika kuelekea kupata uhuru, vyama vya siasa vilishiriki kwenye chaguzi ili kupata kile kitakachoshinda ili kuongoza nchi huru. Katika chaguzi kuu za miaka ya 1958, 1959 na 1960 TANU ilishinda kwa kishindo. Na ule wa mwisho yaani wa mwaka 1960, ulipelekea Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kuteuliwa kuwa Waziri Kiongozi katika serikali ya mpito. Mwezi mei 1961 iliundwa serikali ya madaraka ya ndani na Mwalimu Jullius Nyerere aliteuliwa kuwa Waziri Mkuu. Na ilipofika tarehe 9.12.1961 Tanganyika ilipata uhuru kamili.

Katika kipindi cha mwaka mmoja serikali ya Tanganyika ilikuwa chini ya Malkia wa Uingereza kama mkuu wa nchi na Gavana wa Kiingereza. Ilipofika tarehe 9.12.1962 Tanganyika ilikuwa Jamhuri chini ya uongozi wa Rais Julius Kambarage Nyerere kama mkuu wa nchi.

## Ukombozi wa Zanzibar

Harakati za ukombozi wa Zanzibar zilianza katikati ya miaka ya 1950. Kabla ya hapo ilikuwa ni makundi kadhaa yenye mrengo wa ubaguzi wa rangi yaliyopigania maslahi yao katika Visiwa vya Zanzibar. Waafrika hawakuwa na namna yoyote ya kuwa huru isipokuwa kupambana na uovu wa Waingereza na serikali ya Mamwinyi iliyoongozwa na Waarabu kutoka Oman chini ya Sultani. Kwa ujumla, harakati za ukombozi Zanzibar ziligubikwa na ubaguzi wa rangi.

Katika harakati hizi, Mamwinyi na Waarabu walianzisha chama chao kiitwacho Zanzibar Nationalist Party (ZNP). Madhumuni yake yakiwa ni kunyakua madaraka na kuhakikisha kuwa Mamwinyi wanakabidhiwa madaraka ya kuiongoza Zanzibar huru.

Waafrika waliunda Chama cha Ushirikiano wa Waafrika yaani African Association (AA) ndani ya Zanzibar. Chama kiliundwa kwa lengo kubwa la



FOR ONLINE USE ONLY

MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 83 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kupinga ubaguzi wa rangi na unyonyaji wa mtu mweusi. Pamoja na utetezi dhidi ya unyonyaji wa wakulima na wakwezi, chama kilijishughulisha na michezo pamoja na burudani. Mwaka 1939 Washirazi walianzisha chama chao wakati Waafrika nao walijidhatiti kutokomeza ukoloni wa wageni kupitia chama cha Zanzibar African Association (ZAA) kilichoundwa mwaka 1948. Ilipofika Februari 5, 1957 Washirazi na Waafrika waliunganisha vyama vyao na kuunda chama cha Afro Shiraz Party (ASP).

Ndugu Abeid Aman Karume alichaguliwa kuwa Rais wa ASP na katibu wake alikuwa ndugu Thabit Kombo. Lengo kubwa la ASP lilikuwa kudai uhuru na kuhakikisha kuwa Wazanzibar wana haki ya kumiliki ardhi. Katika harakati hizi, uchaguzi wa kwanza ulifanyika mwaka 1957 na ushindani ulikuwa kati ya ASP na ZNP. ASP ilishinda kwa kupata viti 5 kati ya 6 vya Baraza la Kutunga Sheria (LEGCO).

Muungano huu kati ya Waafrika na Washirazi ulikuwa tishio kubwa kwa Mamwinyi wa kiarabu na Waingereza pia. Hivyo Waingereza na Waarabu walibuni mbinu kadhaa ikiwemo kuwashawishi Washirazi wajitenge ili kuidhoofisha ASP. Baadhi ya Washirazi walikubali na hivyo waliunda chama chao cha Zanzibar and Pemba Peoples Party (ZPPP) mwaka 1959.

Mwaka 1961 mwezi Januari na Juni ulifanyika uchaguzi mwingine ulioipa ASP kura na viti vingi kuliko Zanzibar Nationalist Party (ZNP) na Zanzibar and Pemba People's Party (ZPPP), lakini haikukabidhiwa Serikali kwa vile ZNP na ZPPP waliungana. Uchaguzi mwingine ulifanyika Julai 1963. Mbinu za kuungana ZNP na ZPPP zilirudiwa tena katika uchaguzi huo. Mbinu hizi zilisaidia kuvipa ushindi ZNP na ZPPP vyama hivi vilishawishiwa kuungana ili kuunda serikali moja ya mpito itakayolinda maslahi ya Waingereza. Mohamed Shamte wa ZPPP alipewa madaraka ya kuunda serikali tarehe 10 mwezi Desemba mwaka 1963. Uhuru huu ulifahamika kama uhuru wa Waarabu Sultan ndiye aliyefanywa kuwa mkuu wa nchi.

Hata baada ya kupokonywa haki yao ya uchaguzi, Waafrika chini ya uratibu wa ASP walidhamiria kuendeleza mapambano hadi watakapopata uhuru wao kutokana na unyonyaji uliokithiri kuendelea. Ilipofika tarehe 12 Januari mwaka 1964 ASP waliipindua Serikali ya vibaraka iliyoongozwa na Mohamed Shamte. Sheikh Abeid Aman Karume ndiye aliyekuwa Rais wa kwanza wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya kuwapindua vibaraka wa ZPPP na ZNP.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 84 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Matokeo ya utawala wa kikoloni

Matokeo ya utawala wa kikoloni yamegawanyika katika makundi matatu ambayo ni kiuchumi, kisiasa na kijamii kama ifuatavyo:

**(a) Kiuchumi**

(i) Kuingia kwa matumizi ya fedha, kulisababisha kufa kwa mfumo wa kubadilishana bidhaa baina ya jamii moja na jamii nyingine.

(ii) Wananchi walilazimishwa kulipa kodi, kwa hiyo iliwalazimu kwenda kulima kwenye mashamba makubwa ya Wazungu ili wapate ujira na kwenda kulipa kodi, mfano kodi ya kichwa.

(iii) Kuingia kwa mazao ya biashara kama vile mkonge, kahawa na chai, hivyo wananchi kulazimishwa na Wazungu kwenda kufanya kazi kwenye mashamba hayo.

(iv) Ujenzi wa miundo mbinu, kama vile reli na barabara kwa ajili ya usafirishaji wa malighafi.

(v) Biashara zilifanywa kibaguzi, wazungu walifanya biashara za makampuni makubwa, Waarabu na Wahindi walifanya biashara za rejareja na Waafrika walizuiliwa kufanya biashara yoyote.

(vi) Kunyang'anywa kwa ardhi yenye rutuba kwa wazawa, kwa mfano Wameru.

(vii) Unyonywaji mkubwa wa rasilimali za Tanganyika kama vile madini na wanyama.

**(b) Kijamii**

(i) Kuanzishwa kwa huduma za kijamii, kwa mfano elimu na afya ambavyo vilitolewa kwa misingi ya ubaguzi wa rangi.

(ii) Kutetereka kwa baadhi ya familia, hii ilisababishwa na watu hususani wanaume kwenda kufanya kazi kwenye mashamba makubwa.

(iii) Lishe kuwa duni na upungufu wa chakula, kwa sababu wakoloni walisisitiza kulima mazao ya biashara kuliko mazao ya chakula.

(iv) Kukua kwa matabaka miongoni mwa Watanganyika; kwa mfano waliosoma na wasiosoma, wa mjini na wa vijijini.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 85 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**(c) Kisiasa**

(i) Waafrika hawakuruhusiwa kuwa na nyadhifa za juu za uongozi.

(ii) Wafanyakazi wa serikali ya kikoloni hawakuruhusiwa kujishughulisha na siasa.

(iii) Viongozi wa jadi waliongoza kwa mujibu wa maagizo au maelekezo kutoka kwa wakoloni.

(iv) Utawala wa kikoloni ulikuwa wa kibabe na ukandamizaji.

**Kazi ya kufanya**

Jadili katika vikundi harakati zilizotumiwa na Wazanzibar katika kujiletea ukombozi wao, kisha uziandike kwenye daftari lako.

## Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Je, Zanzibar ilipata uhuru mwaka gani?
2. Elezea sekta tofauti za uchumi katika kipindi cha ukoloni wa Waingereza.
3. Eleza sababu za uanzishwaji wa vyama vya wafanyakazi.
4. Eleza njia zilizotumika kueneza uchumi wa kikoloni.
5. Unafikiri kwanini chama cha ASP kilifanya mapinduzi Zanzibar?

## Zoezi la 4

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Ni yapi yalikuwa majukumu ya Kamishna wa wilaya katika kipindi cha utawala wa Kijerumani?
2. Upinzani wa Mtwa Mkwavinyika Mkwawa ulianza mwaka gani?
3. Tanganyika ilikuwa chini ya utawala wa Uingereza kuanzia mwaka gani?
4. Bwana Rashidi Mfaume Kawawa aliongoza chama gani?
5. Orodhesha matokeo ya utawala wa kikoloni.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 86 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Manamba | wafanyakazi wa kiafrika wa wakoloni katika mashamba makubwa |
| Kibaraka | ni kiongozi wa Taifa fulani anayetumiwa na mabeberu kwa manufaa yao bila kujali madhara yanayowapata wananchi wenzake |
| Walowezi | ni wavamizi katika nchi au taifa fulani katika nyanja za siasa, uchumi na utamaduni |
| Ubeberu | mfumo wa kimataifa wa siasa-uchumi wa uzalishaji mali wa kiwango cha juu kabisa cha ubepari ambapo mataifa tajiri huvuka mipaka yake na kwenda kunyonya uchumi wa nchi maskini |
| Mrengo | mwelekeo au msimamo wa itikadi ya kisiasa unaoamini kuwa ni sharti kuwe na mgawanyo sawa wa mali na madaraka kwa watu wote katika jamii |

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 87 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Tisa

## Mashujaa wa Afrika dhidi ya uvamizi mpya

Ulipokuwa darasa la nne, ulijifunza tabia za kishujaa na namna ya kuwatambua mashujaa wetu. Pia, uliwafahamu mashujaa wa zamani waliopinga uvamizi wa taifa letu, sababu zilizowafanya mashujaa hao kupinga uvamizi wa taifa letu na mchango wao na namna ya kuwaenzi katika taifa letu. Katika sura hii, utajifunza kuhusu uvamizi mpya katika nchi za Afrika na sababu za uvamizi huo kiuchumi, kisiasa na kijamii. Vilevile, utajifunza njia wanazozitumia wageni kuvamia Bara la Afrika na njia wanazozitumia Waafrika kupinga uvamizi huo.

### Dhana ya shujaa

Shujaa ni mtu yeyote anayeweza kukabiliana na matatizo ya jamii yake kwa moyo, nia na nguvu thabiti. Shujaa katika jamii anaweza kuwa mwanaume au mwanamke na anaweza kutoka mahali popote. Pia, anaweza kuwa na michango mbalimbali, kwa mfano anaweza kutoa mchango katika kutoa msaada au kutatua jambo lolote gumu katika jamii inayomzunguka.

Bara letu la Afrika limewahi kuwa na mashujaa wengi waliopambana na uvamizi mbalimbali wa kiuchumi, kisiasa na kijamii miaka mingi kabla na baada ya ukoloni. Baadhi ya mashujaa hawa ni pamoja na Baba wa Taifa hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa Tanzania, aliyekuwa Rais wa Ghana hayati Kwame Nkrumah, Rais wa kwanza wa Afrika ya Kusini baada ya kukomeshwa ubaguzi wa rangi hayati Nelson Mandela, Rais wa kwanza wa Kenya hayati Jomo Kenyatta, hayati Patrice Lumumba wa Kongo (Kinshasa), hayati Samora Machel wa Msumbiji na Keneth Kaunda wa Zambia. Hawa wote na wengine wengi kwa ujumla walipinga uvamizi mpya katika nchi zao kwa kudai haki na usawa, uhuru, fursa sawa za kijamii, kiuchumi, kupinga ubaguzi wa rangi na kuonewa kwa Waafrika kulikotokana na ujio wa wageni hao walowezi.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 88 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE


Julius K. Nyerere


Kwame Nkurumah


Jomo Kenyatta


Patrice Lumumba

**Kielelezo namba 1:** Baadhi ya mashujaa wa Afrika

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza maana ya shujaa.
2. Taja mashujaa watano wa Afrika waliopambana na uvamizi baada ya ukoloni.

## Uvamizi mpya katika nchi za Afrika

Ingawa ukoloni mkongwe uliisha karibu katika nchi zote za Afrika hadi kufikia mwaka 1990, wakoloni walioondoka walianza kurejea kwa njia mpya na namna mbalimbali. Mfumo huo mpya wa kikandamizaji na kinyonyaji uliitwa ukoloni mamboleo. Mfumo huu wa ukoloni ulilenga kuendelea kuzitawala nchi za Kiafrika kwa njia mpya ambayo ilikuwa tofauti na mfumo wa ukoloni mkongwe. Nchi kama Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Italia, Ureno, Ubelgiji na Marekani zilianza kujielekeza kutafuta uhusiano mpya na nchi huru za Kiafrika. Kihistoria, ukoloni mamboleo ulianza kushamiri na kuota mizizi kuanzia miaka ya 1950. Kuanzia wakati huo, makampuni ya Kimarekani yalianza kujijengea ukaribu na mataifa huru na hata yale yaliyokuwa yakielekea kupata uhuru.

Baada ya mwaka 1960, nchi nyingi za Afrika zilikuwa huru, isipokuwa Libya ambayo ilikuwa huru tangu mwaka 1951, Tunisia na Sudani mwaka 1956 na Ghana iliyopata uhuru wake mwaka 1957. Miongoni mwa nchi za Afrika zilizopata uhuru baada ya mwaka 1960 ni pamoja na Tanganyika

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 89 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

mwaka 1961, Uganda mwaka 1962 na Kenya mwaka 1963. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (Kinshasa), Nigeria, Somalia na Togo zilipata uhuru mwaka 1960, Burundi na Rwanda zilipata uhuru mwaka 1962 na mwaka 1964 nchi za Malawi (Nyasaland) na Zambia (Rhodesia ya Kaskazini) zilipata uhuru.

Baadhi ya nchi za Kusini mwa Afrika zilichelewa kupata uhuru kwa vile zililazimika kupigana vita vya ukombozi. Nchi hizo ni Msumbiji 1975, Namibia 1990, Angola 1975, Zimbabwe 1980 na Afrika ya Kusini ambayo ilitokomeza ubaguzi wa rangi na kuunda mfumo wa demokrasia 1994.




**Kielelezo namba 2:** Ramani ya Afrika huru.



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 90 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Soma vitabu mbalimbali vya historia ili ubainishe nchi nyingine zilizopata uhuru kabla ya miaka ya 1960 na baada ya mwaka 1960, kisha jadiliana na wenzako darasani.

## Njia za uvamizi mpya

### (a) Njia ya kisiasa

Njia ya kwanza iliyodhihirisha uvamizi mpya wa kikoloni ni ya kisiasa. Ukoloni mamboleo uliota mizizi zaidi kwa njia ya kupindua na kupandikiza serikali za vibaraka barani Afrika. Kuanzia miaka ya 1950 nchi za Afrika zilipoanza kupata uhuru, mabeberu hawakufurahishwa na serikali mpya za kizalendo. Hali hii ilichangiwa na kupanuka kwa vita baridi iliyokuwapo kati ya ubepari na ujamaa zilizougawa ulimwengu katika pande mbili pinzani. Kambi hizo ni ile ya kibepari ikiongozwa na Marekani na ile ya kijamaa ikiongozwa na Jamhuri za Kisoshalisti za Kisovieti (Urusi).

Mfano wa kwanza ni wa Kongo (Kinshasa). Baada ya Kongo kupata uhuru chini ya Waziri Mkuu Patrice Lumumba mwaka 1960, miezi michache baadaye, nchi hiyo ilishuhudia uasi katika majimbo yake ya Kasai na Katanga. Uasi huo uliongozwa na Moses Tshombe aliyeungwa mkono na serikali za kibaraka za Ubelgiji, Marekani, Ufaransa na mataifa mengine ya kibepari. Serikali ya Kongo iliungwa mkono na Urusi, Cuba na hata baadhi ya nchi huru za Kiafrika kama Ghana. Uasi huo ulisababisha Kongo kuzama katika mauaji ya wenyewe kwa wenyewe na mwaka 1961 Patrice Lumumba aliuawa na vikosi vilivyoungwa mkono na mabeberu na kuiondoa serikali yake mpya madarakani. Badala yake, Wabelgiji na mabeberu wengine walimuunga mkono mtawala mpya aliyeitwa Mobutu Seseseko ambaye alikuwa kibaraka wao.

Baada ya kupata uhuru 1975 chama cha MPLA kilishika madaraka na kilikuwa cha kizalendo. Nchi za kibeberu zilitaka chama cha UNITA kishike madaraka ili kiwe kibaraka wao. Hivyo wakakiunga mkono kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe kati ya serikali ya MPLA na UNITA ili kupindua serikali ya kizalendo ya MPLA.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 91 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

### (b) Njia za kiuchumi

Namna ya pili ambayo imeukomaza ukoloni mamboleo ni njia ya kiuchumi. Misaada ya kifedha na utu inayotoka katika nchi za kibepari ni njia mojawapo ya kuimarisha ukoloni mamboleo. Japo misaada ya kifedha na utu ina michango mbalimbali kiuchumi na kisiasa, baadhi ya misaada hiyo imechochea ukoloni mamboleo. Misaada hasa kutoka Benki ya Dunia na Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) yenye sura ya kuisaidia Afrika kifedha, imekuwa mojawapo ya njia zinazotumiwa na wakoloni kujipenyeza katika nchi huru za Afrika. Mikopo kutoka taasisi hizi huambatana na masharti magumu ya urejeshaji pamoja na riba kubwa kwa mataifa yenye uchumi mdogo.

Njia hizo za kiuchumi wanazozitumia waenezaji wa ukoloni mamboleo zimegawanyika katika sehemu mbili.

#### (i) Soko huria

Ukoloni mamboleo kwa njia za kiuchumi ulianza kujitokeza zaidi mwishoni mwa mwaka 1980. Kuanza kwa uchumi wa soko huria katika nchi nyingi za Kiafrika ulichagizwa na msukumo kutoka mataifa ya kibepari. Nchi za Kiafrika zililazimishwa kufungua milango kwa bidhaa na huduma kutoka mataifa ya Magharibi. Soko huria kwa namna nyingine lilifungua fursa kwa wachuuzi wadogo kununua na kuuza bidhaa, kulisaidia kukua kwa miji na kuhamia mijini kwa wakazi wengi wa vijijini. Soko huria lilienda sambamba na sera ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma, kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta za madini, kilimo na viwanda. Njia hii japo ilileta manufaa lakini baadhi ya mabepari walitumia mwanya huu kujipenyeza kwa njia ya mikataba mibovu katika sekta za madini na sekta nyingine na hivyo kuendelea kupora rasilimali za mataifa ya Afrika. Njia nyingine zilizotumika na wageni zilikuwa ni kukwepa kodi au kupata misamaha ya kodi isiyofaa na hivyo kujinufaisha zaidi na utajiri wa Afrika. Mbinu zote hizi ziliwezekana kutokana na tatizo kubwa la uongozi lililozikumba nchi nyingi za kiafrika kutokana na miongo mingi ya vita na migogoro mingine ya kisiasa na kiuchumi.

#### (ii) Biashara za kimataifa

Biashara za kimataifa ni uuzaji na ununuzi wa bidhaa au malighafi baina ya mataifa. Hivyo, ukoloni mambaoleo ni unyonyaji kupitia biashara za kimataifa. Biashara kati ya Afrika na mataifa ya Magharibi bado ni ile ya uuzaji malighafi kutoka Afrika na ununuzi wa bidhaa za viwandani kutoka Ulaya, Asia na kwingineko. Aina hii ya uhusiano huipa Afrika hasara kubwa kiuchumi, kwa kuwa biashara na mikataba yake bado



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 92 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

inasimamiwa na mabepari, kwani wao hupanga bei za mazao kutoka Afrika. Mazao ya wakulima yananunuliwa kwa bei ya chini wakati bidhaa zao za viwanda ni ghali, aina hii ya uhusiano wa kibiashara ni ya kinyonyaji.

**(c) Njia ya kiutamaduni**

Njia ya tatu ya uvamizi ni kupitia utamaduni na mila za Waafrika. Tatizo hili pia limekuza na kuendeleza ukoloni mamboleo. Mila na utamaduni wa Mwafrika ulianza kuzoroteshwa tangu karne ya 19 baada ya kuingia kwa ukoloni mkongwe. Wakoloni kupitia Wamisionari Wazungu na Waarabu walileta dini na mila za mataifa yao. Kwa njia hiyo, walishawishi Waafrika kupokea utamaduni na lugha zao. Utamaduni wa Mwafrika ulionekana wa kishenzi na usio na ustaarabu. Kwa sababu hii, dini na tamaduni za kiafrika zilianza kudhoofu na kufifia. Baada ya uhuru na hasa kuingia kwa utandawazi na kuenea kwa televisheni na mitandao mbalimbali ya mawasiliano, uvamizi wa kiutamaduni umeongezeka zaidi. Kumekuwa na mwingiliano wa mila nyingi za kigeni kama matumizi ya lugha zao, muziki, mavazi yasiofaa na matumizi ya madawa ya kulevya yanayadhoofisha kwa kiasi kikubwa nguvu kazi ya Bara la Afrika.

**Kazi ya kufanya**

Jadili njia za uvamizi mpya zilizotumika katika maeneo mbalimbali ya Afrika, kisha ziandike kwenye daftari lako.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja njia tatu zinazotumiwa na wageni kuendeleza ukoloni mamboleo barani Afrika.
2. Kama ungekuwa kiongozi ungetumia mbinu zipi kupambana na ukoloni mamboleo?

## Njia wanazotumia Waafrika kupinga uvamizi

### Kuimarisha Umoja wa Nchi za Afrika

Umoja wa Afrika unaunganisha nguvu za Waafrika, ili waweze kujitegemea kiuchumi, kisiasa na kijamii. Viongozi wa nchi za Afrika wanapaswa kufanya jitihada za kuhakikisha kwamba umoja wa nchi za



FOR ONLINE USE ONLY

MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 93 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kiafrika unaimarishwa zaidi. Pamoja na umoja huo wa Afrika, jumuiya za kiuchumi za kikanda kama Jumuiya ya Maendeleo ya Kiuchumi Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki(EAC), Jumuiya ya Afrika Magharibi (ECOWAS) na Jumuiya ya Kiuchumi, nchi za Afrika ya Kati zinapaswa kuimarishwa. Kanda hizi zikiimarishwa zitasukuma zaidi maendeleo ya Afrika kiuchumi kwa kuimarisha biashara za pamoja na kupunguza unyonyaji wa ukoloni mamboleo. Uimara wa jumuiya za kikanda, utaimarisha ulinzi na usalama na kupunguza utegemezi kwa jumuiya za kimataifa kiuchumi, kisiasa, kiulinzi na usalama.

**Kuimarisha Benki ya Afrika**

Nchi za Afrika zinafanya jitihada ya kuimarisha Benki ya Afrika ili kuweza kujitegemea kiuchumi. Benki ya Maendeleo ya Afrika imekuwa kitovu kikubwa cha ujenzi wa Afrika mpya kwa kufadhili ujenzi wa miundombinu kama reli na barabara. Pia, inaweza kusimamia ujenzi wa taasisi imara za kiserikali kwa kuzipa fedha mamlaka za miji ili kujijengea uwezo zaidi. Kwa kufanya hivi, kutapunguza sana kutegemea wakoloni mamboleo na wanyonyaji wa kimagharibi na wengineo.

**Kuimarisha sera za kupinga ukoloni mamboleo**

Tangu uhuru, nchi nyingi zilijitahidi kupinga ukoloni mamboleo kwa namna mbalimbali. Mwaka 1959, mkutano wa Bandung huko Indonesia uliunda kwa mara ya kwanza sauti ya pamoja ya nchi za dunia ya Tatu dhidi ya ukoloni mamboleo na mivutano ya vita baridi. Njia nyingine katika kujenga sera imara dhidi ya ukoloni mamboleo zilikuwa kujenga siasa ya ujamaa na kujitegemea. Nchi kama Tanzania kupitia Azimio la Arusha mwaka 1967 ilitangaza sera thabiti za kujitegemea kama Taifa. Azimio hilo liliunda misingi imara ya kuheshimu utu na kupinga unyonyaji. Pia, lilisisitiza uhuru wa nchi na utekelezaji wa siasa za ujamaa na kujitegemea. Mataifa mengine ya Kiafrika kama Ghana, Zambia, Senegal, Msumbiji na Misri yaliimarisha ujamaa kwa namna mbalimbali yakiwa na dhamira ya kujenga uafrika, kujitegemea na kujiamini.

**Kupunguza utegemezi**

Baada ya nchi nyingi za Kiafrika kupata uhuru, zimeendelea kutegemea misaada kutoka mataifa yaliyozitawala. Hali hii imesababisha nchi nyingi



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 94 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

za Afrika kuendelea kuwa tegemezi katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mataifa yaliyozitawala nchi za Afrika yameendelea kuyanyonya yaliyokuwa makoloni yao kupitia rasilimali zao, kwa mfano, misitu, madini na wanyama pori. Afrika inahitaji kujitegemea na kuimarisha uwekezaji kutoka kwa wazawa na kuimarisha elimu ili kujenga nguvu kazi imara na inayojitosheleza.

### Serikali kuimarisha uchumi

Serikali za nchi za Afrika zinajitahidi kuimarisha uchumi wa nchi zao kwa kupambana na mambo yanayoathiri uchumi kama vile ufisadi, rushwa, na upendeleo. Tanzania ni mfano mzuri wa nchi zinazopinga mambo hayo. Serikali za Afrika zinapaswa kuvutia wawekezaji halali wataoweza kulipa kodi na kuheshimu mikataba waliyoiingia.

### Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

**Andika Ndiyo kwa sentensi sahihi na Hapana kwa sentensi zisizo sahihi.**

1. Uvamizi mpya kutoka nchi za kigeni hutumia vita kuvamia Bara la Afrika. ____________
2. Malighafi ni muhimu katika viwanda vya wavamizi wanaokuja Bara la Afrika. ____________
3. Misaada ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kutoka Ulaya ni njia pekee za kujikomboa. ____________
4. Mikataba mizuri ya biashara ni njia ya kuwasaidia Waafrika kupambana na uvamizi. ____________

### Kazi ya kufanya

Jadiliana na wenzako kubaini njia mbalimbali ambazo Waafrika wanaweza kuzitumia kupinga uvamizi mpya, kisha andika kwenye daftari lako.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 95 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 4

**Jibu maswali yafuatayo:**

**Chagua herufi ya jibu lililo sahihi.**

1. Nchi nyingi za Afrika zilipata uhuru kuanzia mwaka:

   (a) 1961 (b) 1972 ( )

   (c) 1960 (d) 1964

2. Sababu mojawapo ya kiuchumi iliyotumika kuvamia Bara la Afrika ni:

   (a) kilimo (b) kupata elimu ( )

   (c) biashara (d) uchukuzi

**Andika herufi ya jibu sahihi kutoka kifungu B kwa kuoanisha na kifungu A.**

| Na. | Fungu A | Fungu B |
|---|---|---|
| 3. | Sierra Leone na Tanganyika zilipata uhuru mwaka ______ | (a) Nkrumah, Lumumba, Kenyata, Nyerere na Mandela |
| 4. | Nchi ya Tanzania ni mfano bora katika ______ | (b) Uvamizi mpya<br>(c) 1964 |
| 5. | Njia ya kupinga uvamizi Afrika ______ | (d) kupinga rushwa na ufisadi |
| 6. | Mashujaa waliopinga uvamizi Afrika ______ | (e) Kuondoa utegemezi, kuimarisha mikataba, kusitisha misaada na mikopo |
| | | (f) Somalia, Sudan na DRC Kongo (Kongo Kinshasa)<br>(g) 1961 |

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 96 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

7. Taja mambo matano yanayosababisha wavamizi (wakoloni mamboleo) kuja barani Afrika.
8. Eleza kazi inayofanywa na Benki ya Maendeleo ya Afrika.
9. Bainisha njia tatu zinazoweza kutumiwa na nchi za Afrika ili kupinga hali ya uvamizi mpya.

**Andika Ndiyo kwa sentensi sahihi na Hapana kwa sentensi zisizo sahihi.**

10. Mashujaa wa Afrika hufanya kazi ya kuwaelekeza wavamizi sehemu zenye rasilimali. ____________
11. Uvamizi mpya katika nchi za Afrika ulitokea kabla ya nchi hizo kupata uhuru. ____________
12. Nchi za Burundi, Rwanda na Uganda zilipata uhuru mwaka 1962. ____________
13. Soko huria ni mfumo wa uchumi ambao bei ya bidhaa zake na huduma zinazotolewa, hupangwa na serikali. ____________
14. Misaada na mikopo inayotolewa na mataifa ya Ulaya, Marekani na Asia husaidia nchi za Afrika kupambana na uvamizi. ________
15. Wavamizi wanapokuja Afrika huwafundisha Waafrika kutengeneza bidhaa mbalimbali. _________
16. Mataifa ya Ulaya na Marekani hutuma majeshi yao Afrika kusaidia ulinzi wa amani kwa lengo la kutaka kunufaika na rasilimali zilizopo Afrika. ____________
17. Wavamizi kutoka nchi za nje huja Afrika kununua malighafi kwa bei ndogo na kutuuzia bidhaa zao kwa bei kubwa. ____________
18. Nchi za Afrika zinajitahidi kuimarisha uchumi wa nchi zao kwa kupambana na rushwa, ufisadi na viongozi. ____________

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 97 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Malighafi | vitu vinavyotumika kuzalisha au kutengeneza vitu vingine |
| Mathalani | kwa mfano |
| Nadharia | maelezo yanayotolewa bila vitendo |
| Riba | ziada ya pesa au vitu anayopata mtu aliyekopesha kama faida ya kile alichokopesha. Au ni fedha ya ziada anazopata mtu aliyeweka fedha zake benki kama faida ya kuwekeza |
| Rasilimali | mali au nguvu kazi |
| Sera | maelekezo yanayotoa mwongozo wa kufanya jambo fulani |
| Soko huria | uendeshaji wa biashara pasipo mamlaka ya serikali kuingilia |
| Ufisadi | tendo la kufanya ubadhirifu au wizi wa mali zilizopo katika dhamana yako |
| Unyonyaji | tabia ya mtu au watu kujipatia vitu bila kuvifanyia kazi |
| Uwekezaji | kutumia fedha au rasilimali kwa kuanzisha kitega uchumi kwa madhumuni ya kupata kipato zaidi |

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

## Ramani

Ulipokuwa darasa la nne, ulijifunza alama za ramani na namna ya kuchora ramani ya shule. Pia, ulijifunza kuchora pande kuu nne za dunia. Halikadhalika, ulijifunza kusoma uelekeo wa vitu katika mazingira kwa kutumia pande kuu nne za dunia. Katika sura hii, utajifunza dhana ya ramani, aina za ramani, matumizi ya ramani na pande kuu nane za dunia. Vilevile, utajifunza kuchora ramani ya kijiji/mtaa au wilaya.

### Dhana ya ramani

Ramani ni taswira ya nchi au sehemu ya nchi inayooneshwa kwenye karatasi, kipande cha ubao au ardhini kwa vipimo maalumu. Ramani zote huchorwa kwa kutumia kipimio na taarifa zote katika ramani hutafsiriwa kwa kutumia ufunguo.

Ramani ni kifaa kizuri hasa kwa wasafiri katika nchi kavu, baharini na angani. Wajenzi, walimu, marubani, manahodha, watafiti, watalii, wanajeshi na watu wengine wa kada mbalimbali wanahitaji kutumia ramani katika kutimiza majukumu yao. Katika dunia ya leo yenye mabadiliko mengi na mwingiliano mkubwa wa watu, kila mtu anatakiwa kujifunza kutumia ramani. Ramani itamwezesha mtu kufanya shughuli zake bila kusubiri kuuliza maswali mengi yanayohusu unakotoka, ulipo na unakokwenda.

### Aina za ramani

Kuna aina mbili za ramani ambazo ni:

(a) Ramani za topografia. Ramani hizi huonesha sura ya asili ya nchi kama bahari, mito, maziwa na milima. Pia, ramani hizi huonesha vitu viliyotengenezwa na binadamu, mfano barabara, reli, mazao na majengo.

**Kazi ya kufanya**

Chora ramani ya shule yako kuonesha vitu vya asili na vitu vilivyotengenezwa na binadamu katika daftari lako, kisha muoneshe mwalimu wako akusahihishie.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 99 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(b) Ramani za takwimu. Hizi ni ramani zinazoonesha idadi ya watu au vitu katika eneo fulani. Ramani hizi, huonesha mtawanyiko wa wakazi katika nchi, shughuli, mvua, jotoridi na mgandamizo wa hewa.

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Ramani ni nini?
2. Taja aina mbili za ramani.

## Matumizi ya ramani

Ramani hutumika kwa madhumuni mbalimbali. Matumizi hayo ni kama yafuatayo:

(a) Ramani hutumika kuonesha mahali au sehemu vitu vilipo.

(b) Ramani hutumika katika shughuli za kijeshi kwa mfano, wakati wa vita ili kujua uelekeo wa maadui na maeneo muhimu ili wasipotezane.

(c) Ramani hutumiwa na wasafiri, manahodha na marubani katika kuongoza meli au eropleni.

(d) Ramani hutumiwa na watu wa upimaji wa ardhi katika kuandaa mipango miji, ujenzi wa barabara, nyumba na njia za reli.

(e) Ramani hutumika kuelezea maeneo na tabianchi.

## Sifa za ramani

Ramani inakuwa kamili kama itakuwa na vitu vifuatavyo:

(a) **Kichwa cha ramani**, hutambulisha ramani ni ya eneo gani au inahusu nini. Kwa mfano, ramani ya Tanzania kuonesha mikoa inayolima mazao ya biashara.

(b) **Dira**, huonesha mwelekeo wa mahali katika ramani. Dira ina pande kuu nne ambazo ni Kaskazini, Kusini, Magharibi na Mashariki. Kwa kawaida kila ramani huonesha uelekeo wa Kaskazini. Upande wa juu wa ramani ndio uelekeo wa Kaskazini.

(c) **Fremu**, huonesha mwisho au mpaka wa ramani.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 100 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) **Ufunguo**, ni kielelezo kinachofafanua alama au rangi zilizotumika katika ramani.

(e) **Kipimio**, huonesha uwiano kati ya umbali uliopo katika ramani na umbali halisi kwenye ardhi. Matumizi ya kipimio ni kupunguza umbali uliopo ardhini ili uweze kuenea kwenye karatasi inayochorwa ramani. Kwa mfano, huwezi kuchora kilomita moja kwenye karatasi lakini unaweza kutumia sentimita moja kuwakilisha kilomita moja kwenye karatasi. Pia, kipimio humfanya msomaji wa ramani kujua umbali halisi toka sehemu moja hadi nyingine kwenye ardhi kwa kupima umbali huo katika ramani kwa kutumia kipimio.




**Kielelezo namba 1:** Ramani ya wilaya ya Kongwa



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 101 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja sifa tano za ramani.
2. Orodhesha matumizi ya ramani unayoyafahamu.
3. Ufunguo katika ramani huonesha nini?
4. Kwa nini tunatumia kipimio kuchora ramani?

## Pande nane za dunia

Katika darasa la nne, ulijifunza pande kuu nne za dunia. Pande nane za dunia zinatokana na pande kuu nne za dunia ambazo ni Kaskazini, Mashariki, Kusini na Magharibi. Ukichora mstari katikati ya Kaskazini na Mashariki tunapata Kaskazini – Mashariki, vivyo hivyo tunapata Kusini – Mashariki ambayo iko kati ya Kusini na Mashariki. Kusini – Magharibi iko kati ya Kusini na Magharibi. Kaskazini – Magharibi ni upande ulioko kati ya Kaskazini na Magharibi.




**Kielelezo namba 2:** Pande nane za Dunia



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 102 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza maana ya kipimio cha ramani.
2. Eleza umuhimu wa kichwa cha ramani .

**Katika sentensi zifuatazo andika Ndiyo kwa sentensi sahihi na Hapana kwa sentensi zisizo sahihi.**

3. Ramani ni uwakilishi wa sehemu ya eneo la uso wa nchi katika karatasi. ___________
4. Ramani za topografia huonesha sura ya nchi. ___________
5. Dira ya ramani ni utambulisho wa ramani. ___________
6. Ukichora mstari katikati ya Kaskazini na Mashariki tunapata Kaskazini Magharibi. ___________
7. Ramani hutumiwa na wapimaji ardhi katika kuandaa mipango miji. ___________
8. Kusini Magharibi iko katikati ya Kusini na Mashariki. ___________

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi.**

9. Sura ya nchi huoneshwa katika ramani ya aina ya ___________.
10. Dira wakati wote huonesha upande wa ___________.
11. Ramani hutambulishwa na ___________.
12. Alama zilizotumika katika ramani hutafsiriwa kwa kutumia _____________.
13. Ramani za _____________ huonesha takwimu, watu, mvua na joto.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Kada | taaluma mbalimbali |
| Topografia | sura ya nchi |

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 103 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Moja

## Mfumo wa jua

Ulipokuwa darasa la nne, ulijifunza kuhusu mfumo wa jua. Ulijifunza sayari nane katika mfumo wa jua na vitu vinavyopatikana katika sayari dunia. Pia, ulijifunza tofauti kati ya mwanga wa jua na mwanga wa mwezi. Katika sura hii, utajifunza juu ya mfumo wa jua, sifa za sayari dunia, mizunguko ya dunia na matokeo ya dunia kujizungusha kwenye mhimili wake. Vilevile, utajifunza matokeo ya dunia kulizunguka jua, kupwa na kujaa kwa maji, sababu zake na matokeo ya kupwa na kujaa kwa maji.

### Maana ya mfumo wa jua

Jua ni nyota. Nyota hii ipo karibu na dunia kuliko nyota nyingine zote. Kwa sababu ya kuwa karibu na dunia, nuru ya jua ni kali kuliko nyota nyingine tunazoziona. Jua liko katikati ya sayari ambazo hulizunguka. Mfumo wa jua ni mpangilio wa jua, mwezi na sayari zinazolizunguka.

Katika mfumo wa jua kuna sayari nane ambazo ni Zebaki, Zuhura, Dunia, Mirihi, Sumbula, Sarateni, Zohali na Kausi. Kila sayari hulizunguka jua katika njia yake maalumu iitwayo obiti. Muda wa sayari kulizunguka jua unatofautiana kutegemeana na umbali uliopo kati ya jua na sayari yenyewe. Kwa mfano, sayari ya Zebaki humaliza mzunguko wake kwa siku 88 tu, wakati sayari Dunia hulizunguka jua kwa siku $365\frac{1}{4}$ au 366. Sayari zote zilizoko katika mfumo wa jua zina sifa tofauti.

### Sifa za sayari Dunia

Katika kujifunza mfumo wa jua, tumeona kuwa sayari ziko kwenye mpangilio maalumu. Sayari dunia ni ya tatu kutoka kwenye jua. Sayari dunia ina sifa zifuatazo: Ndiyo sayari pekee ambamo viumbe hai vyote vinaishi. Aidha, robo tatu ya eneo la sayari dunia imefunikwa na maji. Pia, sayari dunia ina hewa ya oksijeni na kabonidioksaidi ambazo ni muhimu kwa viumbe hai wanaoishi humo. Halikadhalika, sayari dunia hupata mwanga kutoka kwenye jua.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 104 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi la 1

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza maana ya mfumo wa jua.
2. Obiti ni nini?
3. Kwa nini sayari hutumia muda tofauti kulizunguka jua?
4. Taja sayari nane zilizoko katika mfumo wa jua.
5. Taja sifa nne za sayari dunia.

## Mizunguko ya dunia

Dunia ina mizunguko miwili. Mzunguko wa kwanza ni dunia kujizungusha yenyewe kwenye mhimili wake na mzunguko wa pili ni dunia kulizunguka jua. Mizunguko hii, hutokea kwa wakati mmoja. Dunia hukamilisha mzunguko mmoja wa kujizungusha yenyewe katika mhimili wake kutoka Magharibi kuelekea Mashariki kwa saa 24 yaani siku moja. Dunia hulizunguka jua kwa siku $365\frac{1}{4}$ au siku 366 kamili, sawa na mwaka mmoja.




**Kielelezo namba 1:** Dunia inajizungusha kwenye mhimili wake



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 105 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Matokeo ya dunia kujizungusha kwenye mhimili wake

Dunia inapojizungusha kwenye mhimili wake tunapata usiku na mchana, kupwa na kujaa kwa maji, mabadiliko ya uelekeo wa upepo na mikondo ya bahari. Pia, tunapata tofauti ya muda kati ya longitudo moja na nyingine. Dunia hutumia dakika nne kujizungusha kutoka nyuzi moja ya longitudo hadi nyingine, hivyo hutumia dakika 60 ambazo ni sawa na saa moja kujizungusha nyuzi 15 za longitudo. Kwa hiyo tofauti ya muda kati ya kila nyuzi 15 za longitudo ni saa moja.

## Matokeo ya dunia kulizunguka jua

Mzunguko wa pili wa dunia, ni ule wa dunia kulizunguka jua. Matokeo ya mzunguko huu ni majira ya mwaka ambayo ni kiangazi, masika, kipupwe na vuli. Vilevile, dunia inapolizunguka jua tunapata tofauti ya urefu wa usiku na mchana katika kipindi fulani cha mwaka. Kwa mfano, mwezi Novemba hadi Januari katika nchi yetu jua huchelewa kuzama kuliko inavyokuwa kwa miezi ya Juni na Julai. Katika mzunguko wake dunia huwa karibu zaidi na jua Januari 3 kila mwaka kipindi ambacho hujulikana kama Perihelioni. Julai 6 kila mwaka dunia huwa mbali zaidi na jua na hujulikana kama Afelioni. Pia, dunia inapolizunguka jua tunapata tofauti ya kimo cha jua la utosi kwa vipindi tofauti vya mwaka. Kadhalika, dunia inapolizunguka jua husababisha kupatwa kwa jua na kupatwa kwa mwezi.




**Kielelezo namba 2:** Dunia inalizunguka jua

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 106 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na wenzako darasani kuhusu majira ya mwaka, kisha taja miezi ya masika, kiangazi, vuli na kipupwe kulingana na sehemu ya nchi uliyopo.

**Zoezi la 2**

**Jibu maswali yafuatayo:**

**Andika Ndiyo kwa sentensi sahihi au Hapana kwa sentensi zisizo sahihi.**

1. Dunia ina mizunguko miwili. ________
2. Dunia inapolizunguka jua tunapata usiku na mchana. ________
3. Usiku na mchana huwa na urefu sawa kipindi chote cha mwaka. ________
4. Dunia inapolizunguka jua tunapata majira ya mwaka. ________

## Kupwa na kujaa kwa maji

Katika sehemu za pwani kuna wakati maji husogea mbali na kingo za bahari na kuna wakati maji yanarudi mpaka kwenye kingo za bahari. Kitendo hiki ndicho huitwa kupwa na kujaa kwa maji. Maji yanaposogea mbali na kingo za bahari hali hiyo huitwa kupwa na maji yanaporudi mpaka kwenye kingo za bahari huitwa kujaa kwa maji.

## Sababu za kujaa na kupwa kwa maji

Kujaa na kupwa kwa maji hutokea baharini na matokeo yake huonekana ufukweni. Hii hutokana na mabadiliko yanayosababishwa na nguvu ya uvutano kati ya dunia na mwezi.

Sehemu ya dunia inayotazamana na mwezi huathiriwa zaidi na nguvu hizi za uvutano. Maji ya bahari huvutwa kuelekea upande mwezi ulipo wakati unapoizunguka dunia kwa muda wa siku moja.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 107 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Matokeo ya kupwa na kujaa kwa maji

Maji yanapokupwa na kujaa huleta matokeo yafuatayo:

Kupwa na kujaa kwa maji husababisha mmomonyoko wa ardhi katika fukwe za bahari hasa bahari inapokuwa na mawimbi makubwa wakati wa kujaa kwa maji. Kupwa na kujaa kwa maji huleta mazao ya wanyama wa baharini kwenye nchi kavu. Mazao hayo ni kama kauri, koa, kombe na simbi ambayo huokotwa na watumiaji wakati maji yanapokupwa. Mazao hayo ya baharini hutumiwa na watu kama mapambo.



Muonekano wa mazao ya bahari baada ya maji kupwa



Simbi



Kauri



Kombe



Koa

**Kielezo namba 3**: Baadhi ya mazao kutoka baharini

FOR ONLINE USE ONLY

### Zoezi la 3

**Chagua herufi ya jibu sahihi.**

1. Dunia hulizunguka jua kwa muda wa:

   (a) saa 24 (b) siku $365\frac{1}{4}$ au 366 ( )

   (c) usiku na mchana (d) siku 300

2. Dunia hutumia muda wa dakika ___________ kujizungusha kati ya longitudo moja hadi nyingine:

   (a) 15 (b) 24 ( )

   (c) 4 (d) 60

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

3. Mabadiliko ya maji kupwa na kujaa hutokea mara mbili:

   (a) kila siku (b) kwa wiki ( )

   (c) kwa mwaka (d) baada ya mwezi mmoja

4. Sayari yenye viumbe hai ni:

   (a) Sumbura (b) Mihiri

   (c) Zuhura (d) Dunia ( )

**Weka alama ya vema (✓) mbele ya sentensi sahihi na alama ya kosa (×) kwa sentensi zisizo sahihi.**

5. Dunia hulizunguka jua.

6. Dunia hujizungusha kwenye mhimili wake kwa saa 24.

7. Dunia hulizunguka jua kwa siku $365\frac{1}{4}$

8. Dunia hulizunguka jua kwa saa 24.

9. Usiku na mchana hutokana na jua kuizunguka dunia.

**Jibu maswali yafuatayo kwa kuandika Ndiyo kwa sentensi sahihi au Hapana kwa sentensi zisizo sahihi.**

10. Mzunguko wa dunia katika mhimili wake hausababishi usiku na mchana. ____________

11. Baadhi ya mazao yanayopatikana baharini ni kauri, koa, kombe na simbi. ____________

12. Tofauti ya muda kati ya kila nyuzi 15 za longitudo ni saa moja. ____________

13. Kupwa na kujaa kwa maji husababishwa na nguvu ya mvutano kati ya mwezi na jua. ____________

14. Dunia hujizungusha katika mhimili wake kutoka Mashariki kwenda Magharibi. ____________

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Afelioni | kipindi cha mwaka ambapo dunia huwa mbali zaidi na jua |
| Kiangazi | msimu wa jua usio na mvua |
| Kimondo | nyota ipitayo kasi angani |
| Kipupwe | msimu wa baridi wenye upepo, unyevu kidogo na ukungu |
| Masika | majira ya mvua nyingi inayonyesha mfululizo |
| Mzingo (obiti) | njia ya sayari kulizunguka jua |
| Perihelioni | kipindi cha mwaka ambapo dunia huwa karibu zaidi na jua |
| Vuli | msimu wa mvua za muda mfupi |

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 110 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Mbili

## Rasilimali zetu

Darasa la nne, ulijifunza rasilimali zilizoko katika kijiji au mtaa na kata. Pia, ulijifunza rasilimali zilizoko katika Wilaya yako. Katika sura hii utajifunza aina za rasilimali zinazopatikana katika mkoa unaoishi, ulinzi wa rasilimali hizo na mchango wake katika maendeleo ya mkoa. Vilevile, utajifunza vitendo vya uharibifu wa rasilimali zilizoko katika mkoa na njia za kulinda rasilimali hizo.

### Maana ya rasilimali

Rasilimali ni jumla ya mali alizonazo mtu, jamii au taifa. Rasilimali za nchi zikitumika ipasavyo zinaweza kulifanya taifa kupata mabadiliko chanya kuelekea kwenye maendeleo. Rasilimali zinazopatikana katika mkoa wako zimegawanyika katika makundi makuu mawili ambayo ni rasilimali za asili na rasilimali za kutengenezwa au kuundwa. Rasilimali zote zinaweza kuharibiwa zisipotunzwa vizuri. Jukumu la utunzaji wa rasilimali hizo ni la kila mwananchi.

**Rasilimali za asili:** ni mali za asili ambazo mtu, jamii, au nchi huwa nazo. Rasilimali hizo hazitengenezwi na mtu. Baadhi ya rasilimali hizo ni ardhi, gesi, maji, madini, uoto wa asili, na mbuga za wanyama.

**Rasilimali za kutengenezwa:** ni mali ambazo mtu, jamii au taifa huwa nazo kutokana na ubunifu na kazi za binadamu. Rasilimali hizi ni kama vile miundombinu mfano barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na majengo. Katika kundi hili pia kuna makumbusho ya kihistoria kwa mfano michoro ya kale ya Kondoa Irangi, magofu ya Kaole Bagamoyo, Kilwa Kivinje kwenye boma la Wajerumani na Mji mkongwe Zanzibar. Pia, kuna vivutio vya kiutamaduni kwa mfano mavazi, ngoma na nyimbo. Hizi zote ni rasilimali zetu.

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Rasilimali ni nini?
2. Taja makundi mawili ya aina za rasilimali.
3. Kwa kila aina ya rasilimali ulizotaja katika swali la pili, toa mifano ya rasilimali zinazopatikana katika mkoa wako.



FOR ONLINE USE ONLY

MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 111 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Ardhi ni sehemu ya dunia ambayo haijafunikwa na maji, ambako mimea huweza kuota. Ardhi ni rasilimali muhimu inayobeba rasilimali nyingine. Ni sehemu ambayo shughuli mbalimbali hufanyika kwa ajili ya maendeleo ya mtu binafsi, jamii na nchi kwa ujumla.

## Mchango wa rasilimali ardhi

Katika maendeleo ya mkoa, ardhi hutumika kwa shughuli za kilimo cha mazao ya chakula na biashara, kujenga miundombinu, kama vile barabara, reli na viwanja vya ndege. Vilevile, ardhi huhifadhi aina mbalimbali za madini. Katika ardhi hupatikana udongo unaotumika kwa kilimo, kufinyanga vitu mbalimbali kama vyungu, sanamu na kutengeneza matofali kwa ajili ya kujengea. Ardhi ni rasilimali muhimu, ikitumiwa vizuri huongeza pato la mkoa na taifa kwa ujumla.

## Vitendo vinavyochangia kuharibu rasilimali ardhi

Uharibifu wa rasilimali hii, huweza kusababishwa na vitendo mbalimbali vikiwemo vile vilivyojadiliwa katika sura ya kwanza ya kitabu hiki. Baadhi ya vitendo hivyo ni:

Kilimo kisichozingatia kanuni na njia bora za kuhifadhi ardhi. Kwa mfano kukata miti ovyo, kuchoma moto wakati wa kuandaa mashamba kwa ajili ya kilimo na kulima shamba kwa muda mrefu bila kulipumzisha. Pia, kupanda zao la aina moja katika shamba kwa muda mrefu, huchangia kuharibu ardhi. Vitendo vingine vinavyoharibu ardhi ni kutumia kemikali zinazoua wadudu katika kilimo. Vitendo hivi husababisha ardhi ichakae upesi na kushindwa kutoa mazao bora ya kilimo.

Uharibifu mwingine wa rasilimali ardhi unatokana na ufugaji wa mifugo mingi inayozidi uwezo wa malisho na ufugaji wa kuhamahama kwa ajili ya kufuata malisho. Kuhamahama kwa mifugo, husababisha mgandamizo wa udongo na kuharibu unamu wake. Aidha, husababisha mmomonyoko wa udongo katika sehemu inakopitia mifugo mara kwa mara. Pia, utupaji wa taka ngumu zisizooza kwa mfano mifuko ya plastiki nayo husababisha uharibifu wa rasilimali ardhi.

## Njia za kulinda rasilimali ardhi

Ili kulinda rasilimali ardhi za mkoa hatuna budi kuzingatia njia zifuatazo:

Kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa rasilimali ardhi. Kuzingatia kanuni za kilimo bora kwa kupumzisha shamba ili lirudishe rutuba yake ya asili,

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kulima kwa kubadilisha mazao ili ardhi isichoke haraka, kutumia mbolea za asili na kulima kwa kukingama mteremko. Kupanda miti ili kutunza rutuba na viumbe hai vinavyopatikana katika ardhi. Kupunguza idadi ya mifugo ili iendane na uwezo wa malisho. Kutotupa taka ovyo hasa zile zisizooza mfano mifuko ya plastiki.



**Kielelzo namba 1:** Wanafunzi wakipanda miti

## Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza umuhimu wa ardhi.
2. Orodhesha vitendo vinavyochangia uharibifu wa ardhi.
3. Taja njia za kuzuia uharibifu wa ardhi.

## Maji

Maji ni rasilimali ya asili inayojumuisha mito, maziwa, bahari, mabwawa na yale yaliyoko chini ya ardhi. Baada ya mvua kunyesha, sehemu ya maji yanaingia ardhini na mengine huingia kwenye mito, mabwawa, maziwa na bahari. Maji yanayoingia ardhini huweza kupatikana kwenye chemchemi na visima.



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 113 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mchango wa rasilimali maji

Maji ni rasilimali muhimu sana katika maisha ya viumbe hai. Maji husaidia kuzalisha umeme unaotumika viwandani na nyumbani. Pia, husaidia katika usafirishaji na hutumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Pia, maji hutumika kwa matumizi ya shughuli za nyumbani, viwandani na shughuli za uvuvi. Maji ya bahari na baadhi ya maziwa mfano ziwa Kindai na Singidani mkoani Singida hutupatia chumvi kwa matumizi ya nyumbani na viwandani. Maziwa mengine mfano Ziwa Natron hutupatia magadi soda inayotumika katika utengenezaji wa vyakula vya kuoka kama vile keki, mikate na maandazi. Pia, hutumika kulainisha vyakula ambavyo ni vigumu kuiva.

## Vitendo vinavyochangia kuharibu rasilimali maji

Uharibifu wa rasilimali maji, husababishwa na vitendo vifuatavyo: Shughuli za kilimo katika vyanzo vya maji, kuchoma moto na ukataji miti na misitu ovyo inayozunguka vyanzo vya maji. Vitendo hivi, husababisha mmomonyoko wa udongo kwenye vyanzo vya maji na kuviharibu. Pia, husababisha kukauka kwa vyanzo vya maji. Vitendo vingine ni umwagaji taka za kemikali toka viwandani katika mito, maziwa na bahari. Pia, uvuvi haramu kwa kutumia sumu na baruti huharibu rasilimali maji. Vitendo hivi huua viumbe hai vinavyoishi katika maji na kuharibu ikolojia ya bahari, ziwa au mto.

## Njia za kulinda rasilimali maji

Ili kulinda rasilimali maji hatuna budi kuzingatia mambo yafuatayo:

Kuweka sheria zinazozuia shughuli za kilimo katika vyanzo vya maji na kuepuka kukata miti ovyo katika maeneo yanayozunguka vyanzo vya maji. Njia nyingine ni kuyatibu maji yenye kemikali kutoka viwandani kabla ya kuyatiririsha kwenye bahari, maziwa au mito. Pia, kuzuia vitendo vyote vya uvuvi haramu wa kutumia sumu na baruti, kwani husababisha uchafuzi wa maji. Pili, ili tuwe na maji ya kutosha, uvunaji wa maji ya mvua usisitizwe.

### Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza umuhimu wa maji.
2. Taja matumizi ya rasilimali maji katika mkoa wako.
3. Orodhesha sababu zinazochangia uharibifu wa rasilimali maji.
4. Taja njia za kutunza rasilimali maji.



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 114 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Uoto wa asili

Uoto wa asili ni mimea yote inayoota bila kupandwa katika eneo fulani. Mimea hii ni tofauti na ile inayooteshwa na binadamu. Aina za uoto wa asili zinazopatikana Tanzania ni misitu, mbuga vichaka na nyasi. Uoto wa asili huhusiana moja kwa moja na tabianchi. Kwa mfano, sehemu zenye mvua nyingi huwa na misitu minene, na sehemu zenye mvua kidogo zina mbuga za vichaka na nyasi.

## Mchango wa uoto wa asili katika maendeleo ya mkoa

Uoto wa asili husaidia kutupatia mvua ambazo huhitajika katika shughuli za uzalishaji mali mfano, kilimo na ufugaji. Misitu pia inasaidia kukua kwa viwanda ambavyo hutumia malighafi kutokana na misitu, mfano mbao kwa ajili ya ujenzi, kutengeneza samani na karatasi. Pia, inatusaidia kupata mazao kama asali na dawa za asili. Misitu pia hutupatia nishati ya kuni na mkaa.

## Vitendo vinavyochangia uharibifu wa uoto wa asili

Uharibifu wa uoto wa asili husababishwa na shughuli za kilimo, kukata na kuchoma moto misitu au mbuga. Vilevile, kilimo cha kuhamahama na uchomaji wa mkaa, husababisha uharibifu wa rasilimali misitu.

## Njia za kulinda uoto wa asili

Ili kulinda rasilimali hii, hatuna budi kuzingatia njia zifuatazo: Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa uoto wa asili. Kuzuia shughuli za kiuchumi kwa kuweka sheria na kanuni za usimamizi wa misitu. Kuhimiza wananchi kupanda miti kabla ya kukata miti. Pia, kuacha vitendo vya kuchoma moto misitu na mbuga.

### Zoezi la 4

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza maana ya uoto wa asili.
2. Taja aina ya uoto wa asili unaopatikana katika mkoa wako.
3. Taja vitendo vinavyochangia kuharibu uoto wa asili katika mkoa wako.
4. Elezea njia za kulinda uoto wa asili.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 115 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Mbuga za wanyama

Mbuga ya wanyama ni eneo lililotengwa maalumu kwa ajili ya kuhifadhi wanyamapori. Tanzania kuna mbuga na hifadhi nyingi za wanyamapori kama vile Serengeti, Katavi, Manyara, Mikumi, Ruaha, Tarangire na Selous. Pia, wanyamapori hupatikana katika eneo la Mamlaka ya hifadhi Ngorongoro. Baadhi ya wanyama wakubwa wanaopatikana katika hifadhi hizi ni tembo, nyati, kifaru, twiga, chui, simba, nyumbu, tandala na pundamilia.



**Kielelezo namba 2:** Wanyamapori wakiwa katika hifadhi

## Mchango wa mbuga za wanyama

Mbuga za wanyama huliingizia taifa kipato kupitia utalii wa ndani na wa nje. Vilevile huleta maendeleo ya miundombinu kama vile barabara, mawasiliano na hoteli. Aidha, husaidia kukuza kipato cha mtu mmojammoja kwa kutoa ajira mbalimbali. Uwepo wa mbuga za wanyama husaidia katika kutoa elimu kwa kufanya ziara za kielimu na kufanya tafiti za kisayansi.

## Vitendo vinavyochangia kuharibu mbuga za wanyamapori

Uharibifu wa rasilimali hii husababishwa na vitendo mbalimbali, kama vile kufanya shughuli za ufugaji na kilimo ndani ya hifadhi. Vilevile, kuchoma moto maeneo yaliyo karibu na mbuga za wanyama ambao huweza kusababisha moto kuenea hadi kwenye hifadhi na kusababisha madhara kwa wanyama, miundombinu na uoto wa asili. Pia, vitendo vya ujangili, mfano uuaji wa wanyama kama vile tembo na vifaru.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 116 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Njia za kulinda mbuga za wanyama

Ili kulinda rasilimali hii hatuna budi kufanya mambo yafuatayo: Kuweka sheria zinazozuia kufanya shughuli za binadamu kama vile kilimo na ufugaji katika mbuga za wanyama, na kuwaelimisha watu kuhusu kuyalinda maeneo ya hifadhi dhidi ya moto. Pia, kuweka ulinzi ili kudhibiti ujangili na uwindaji holela. Kuimarisha mipaka ya maeneo ya hifadhi ili kudhibiti uvamizi wa maeneo hayo kwa shughuli za binadamu kama vile ujenzi, kilimo na ufugaji.

**Kazi ya kufanya**

Jadiliana na wenzako kubainisha aina za wanyamapori wanaopatikana katika mbuga za wanyama na faida zinazotokana na mbuga hizo.

**Zoezi la 5**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja mbuga tatu za wanyama unazozifahamu.
2. Eleza umuhimu wa mbuga za wanyama.
3. Taja aina mbili za utalii.

## Madini

Madini ni rasilimali ambayo huchimbwa ardhini. Madini yapo ya aina mbalimbali hapa nchini. Mifano ya madini ni almasi, bati, chuma, gesi, shaba, dhahabu, Tanzanite, magadi, ulanga na makaa ya mawe.

## Mchango wa madini kwa maendeleo ya mkoa

Madini hutupatia faida kubwa ikiwa ni pamoja na fedha. Kipato hicho hutumika kwa ajili ya kuimarisha miundombinu kwa mfano, umeme, barabara, maji na njia za mawasiliano. Aidha, sehemu zinazozunguka migodi hujengwa miundombinu na huduma muhimu za kijamii kama vile hospitali, shule na soko ambapo watu hupata ajira. Vilevile, huchangia katika kukua kwa makazi kutokana na kuwepo kwa watu wengi kutoka sehemu mbalimbali ambao wamekuja kufanya kazi kwenye migodi.

## Njia za kulinda madini

Ili kulinda rasilimali hii hatuna budi kuzingatia njia zifuatazo:
Kusisitiza matumizi ya teknolojia sahihi katika uchimbaji wa madini, usimamizi mzuri wa madini kwa kuweka sheria zinazosimamia uchimbaji,

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 117 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

uuzaji, ununuzi na usafirishaji wa madini na uhifadhi wa mazingira. Pia, kutoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya kemikali zinazotumika kusafisha madini.

**Kazi ya kufanya**

Jadili katika vikundi faida za madini, kisha andika kwenye daftari lako.

## Zoezi la 6

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Madini ni nini?
2. Orodhesha madini yanayopatikana katika mkoa wako.
3. Eleza umuhimu wa madini.
4. Eleza njia za kulinda madini.

## Zoezi la 7

**Jibu maswali yafuatayo:**

**Andika Ndiyo kwa sentensi zilizo sahihi na Hapana kwa sentensi zisizo sahihi.**

1. Madini, milima, maji na ardhi ni mifano ya rasilimali za asili. ___________
2. Simba, tembo, nyati, nyoka, mbuzi, ng'ombe ni baadhi ya wanyama wanaoishi mbugani. ___________
3. Ni muhimu kutunza rasilimali zetu ili zisiharibiwe. ___________
4. Bila vyanzo vya maji hatuwezi kupata maji safi na salama. ___________
5. Serikali ndiyo pekee yenye wajibu wa kulinda rasilimali za Taifa. ___________
6. Mmomonyoko wa udongo ni matokeo ya matumizi yasiyofaa ya rasilimali za ardhi. ___________

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 118 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Jibu maswali yafuatayo:**

7. Taja rasilimali za asili zinazopatikana kwenye mkoa wako.
8. Eleza juhudi zinazofanywa na serikali ya mkoa kuhakikisha inazuia vitendo vya uharibifu wa rasilimali maji.
9. Taja aina za uoto wa asili zilizopo katika eneo lako.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Ikolojia | ni uhusinao wa viumbe na mazingira yao pamoja na viumbe wengine |
| Kemikali | kitu chochote chenye uwezo wa kuathiri taratibu afya ya kiumbe |
| Magadi | madini aina ya chumvi ambayo hutumiwa kutengeneza sabuni au kulainisha chakula |
| Samani | vifaa kama viti, meza au kabati vilivyotengenezwa kwa mbao |
| Ujangili | uwindaji wanyamapori bila idhini kwa lengo la kupata mazao ya wanyamapori kama vile, pembe za ndovu, nyama na ngozi |
| Unamu | jinsi chembechembe za udongo au mchanga zilivyokaa au kufanana |

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 119 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Tatu

## Uzalishaji mali

Ulipokuwa darasa la nne, ulijifunza shughuli mbalimbali za uzalishaji mali katika kijiji, mtaa na kata. Vilevile, ulijifunza vikwazo vinavyoweza kujitokeza katika shughuli za uzalishaji mali.

Katika sura hii, utajifunza shughuli za uzalishaji mali kabla na baada ya uhuru na mapato yatokanayo na uzalishaji mali. Vilevile, utajifunza njia za kuboresha shughuli za uzalishaji mali.

### Shughuli za uzalishaji mali

Shughuli za uzalishaji mali ni kazi anazofanya binadamu ili kujipatia kipato. Shughuli za uzalishaji mali zina manufaa kwa mtu na kwa taifa. Binadamu anaweza kuzalisha mali kwa kufuga, kulima, kuchimba madini, kufanya biashara, kuvua samaki, kufanya kazi viwandani na shughuli za utalii.

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza maana ya shughuli za uzalishaji mali.
2. Taja njia nne za uzalishaji mali.

### Shughuli za uzalishaji mali kabla ya uhuru

Kabla ya uhuru, shughuli kuu za uzalishaji mali zilikuwa ni kilimo, ufugaji na uvuvi. Jamii zilifanya shughuli mbalimbali kutokana na hali ya kijiografia ya sehemu husika. Wakulima wengi walipatikana sehemu zenye udongo wenye rutuba na mvua nyingi. Mashamba waliyolima yalikuwa madogo kwa ajili ya mazao ya chakula na walilima kwa kutumia jembe la mkono. Pia, wageni walipofika walifanya shughuli za kilimo kwa kuwatumia Waafrika kama vibarua. Kilimo hicho, kilikuwa cha mashamba makubwa ya mazao ya biashara kama vile mkonge, chai, pareto na kahawa. Wageni walitumia mashine kama trekta katika shughuli za kilimo. Kilimo cha mazao ya biashara kilifanyika katika mikoa ya Morogoro na Tanga

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 120 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwa zao la mkonge, kahawa katika mikoa ya Kagera na Kilimanjaro na chai katika mikoa ya Iringa, Mbeya na Tanga.

Wafugaji wengi walipatikana katika sehemu zenye maji na malisho ya mifugo ambazo hazikuwa na mbung'o. Walifuga ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na bata ili kupata nyama, maziwa, ngozi na mayai. Pia, walifuga punda kwa ajili ya kubeba mizigo.

Shughuli za uvuvi zilifanyika sehemu zenye bahari, maziwa, mito na mabwawa. Katika uvuvi, wavuvi walitumia vifaa kama vile mgono, ndoana, upindo na jarife.

### Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja shughuli kuu mbili za uzalishaji mali kabla ya uhuru.
2. Nini faida ya kilimo katika jamii?
3. Taja mahitaji makuu mawili yanayowezesha shughuli ya ufugaji.
4. Taja vifaa viwili vya uvuvi vilivyotumika kabla ya uhuru.
5. Mazao gani matatu ya biashara yaliyolimwa na wageni?

## Shughuli za uzalishaji mali baada ya uhuru

Shughuli za uzalishaji mali zilizofanywa baada ya uhuru ni mwendelezo wa shughuli za uzalishaji mali zilizofanywa kabla ya uhuru. Shughuli hizo ni kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara, utalii na viwanda.

## Kilimo

Baada ya uhuru kilimo kimeendelea kuwa shughuli kuu ya uzalishaji mali inayofanywa na watu wengi na ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu. Kilimo kinafanyika na mtu mmojammoja na katika mashamba makubwa ambayo mengi yanamilikiwa na wawekezaji.

Kilimo kinachofanyika ni cha mazao ya chakula, mfano maharage, mahindi na mpunga, huko Mbarali Mbeya eneo la Kapunga na Ifakara Morogoro. Mazao ya biashara ni pamba, mkonge, chai, kahawa, korosho, tumbaku na alizeti.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufugaji

Shughuli nyingine ya uzalishaji mali ambayo imeendelea kufanyika baada ya uhuru ni ufugaji. Shughuli ya ufugaji hufanyika katika sehemu ambazo hazina mbung'o ili kuepusha mifugo isishambuliwe na ugonjwa wa malale unaosababishwa na mbung'o. Aidha, ufugaji wa samaki na kuku wa nyama na mayai hufanywa katika maeneo mbalimbali ya nchi. Ufugaji unafanywa na mfugaji mmojammoja na pia hufanywa na mashirika au makampuni katika mashamba makubwa ya kufugia wanyama yaani ranchi za taifa. Baadhi ya ranchi hizi zipo maeneo ya Kongwa mkoani Dodoma, Handeni mkoani Tanga na Ruvu mkoani Pwani. Vilevile, kuna mashamba ya ng'ombe wa maziwa katika chuo cha utafiti wa kilimo na mifugo Mpwapwa mkoani Dodoma.

Katika kuhakikisha mifugo inakuwa na malisho ya kutosha kwa mwaka mzima, hata wakati wa kiangazi, serikali imetenga mashamba ya nyasi ambapo nyasi hizo zikishakua hukatwa na kufungwa kwa mashine maalumu na kuhifadhiwa kwa ajili ya kulisha wanyama wakati wa kiangazi. Mfano wa mashamba hayo ni shamba la Kiboriani lililoko wilaya ya Kongwa na shamba la Kafoi lililoko Sanya juu, Kilimanjaro.

**Kazi ya kufanya**

Tembelea eneo au sehemu yoyote yenye shughuli za ufugaji iliyo karibu na shule yako ili kujifunza namna wanyama wanavyotunzwa.

## Uvuvi

Shughuli nyingine ya uzalishaji mali ni uvuvi. Baada ya uhuru, wavuvi wameendelea kuvua samaki katika bahari, maziwa, mito na mabwawa kwa lengo la kujipatia kipato na chakula. Njia zinazotumika katika uvuvi ni njia za asili na njia za kisasa. Baadhi ya njia za asili ni kuvua kwa kutumia mgono, dema, na mkuki. Njia za uvuvi za kisasa hutumia vyombo vikubwa vya uvuvi pamoja na vifaa kama vile nyavu na ndoana.

## Biashara

Biashara ni shughuli nyingine ya uzalishaji mali ambayo inaendelea kufanyika hadi sasa. Kuna wafanyabiashara wakubwa wenye makampuni kama Independent Power Producer (IPP), Bakhresa na Mohamed



FOR ONLINE USE ONLY

MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 122 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Enterprises. Kampuni hizi na nyingine nyingi huzalisha bidhaa mbalimbali na kuziuza nje ya nchi na kwa wafanyabiashara wadogowadogo ambao huwauzia walaji. Wafanyabiashara wadogowadogo humiliki maduka ya kuuza bidhaa mbalimbali kama sukari, unga (sembe, dona na ngano), sabuni na mchele. Wafanyabiashara wadogowadogo ni pamoja na wamachinga ambao huuza bidhaa zao kwa kutembeza, yaani huwafuata wateja majumbani au mahali popote walipo.

## Viwanda

Viwanda ni mojawapo ya shughuli ya uzalishaji mali nchini Tanzania. Baadhi ya viwanda tulivyo navyo ni viwanda vya sukari, nguo na viwanda vya kubangua korosho. Viwanda vingi vimeendelea kujengwa tangu nchi yetu ilipopata uhuru. Baada ya uhuru viwanda vingi vilimilikiwa na umma. Hata hivyo sera ya ubinafsishaji ya mwaka 1992, ilisababisha viwanda vingi kuuzwa. Baadhi ya wawekezaji hawakuviendeleza viwanda walivyonunua na hivyo kusababisha viwanda vingi kufungwa. Kuanzia mwaka 2015 serikali iliweka mikakati ya kufufua uzalishaji wa viwanda mbalimbali.

Shughuli za viwanda husaidia upatikanaji wa ajira na imekuwa ni sehemu muhimu ya kuwawezesha watu kujipatia kipato. Pia, viwanda huingizia serikali mapato kwa njia ya kodi. Vilevile, viwanda huwezesha shughuli nyingine za uzalishaji mali kama vile kukua kwa kilimo, kwani wakulima huweza kuyauza mazao viwandani kama malighafi. Upatikanaji wa umeme, malighafi na uwepo wa wataalamu waliohitimu kutoka vyuo mbalimbali umesaidia kukua kwa sekta ya viwanda.

## Utalii

Sekta ya utalii imekuwa ni miongoni mwa shughuli za uzalishaji mali. Serikali, makampuni na watu binafsi wanajishughulisha na sekta ya utalii. Sekta hii, imeajiri watu katika nyanja mbalimbali. Kwa mfano, watu wamejiajiri kwa kazi za kutoa huduma hotelini, kuongoza watalii, udereva na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali za asili kwa ajili ya watalii. Baadhi ya shughuli za utengenezaji wa bidhaa hizi ni uchongaji vinyago au uchoraji, bidhaa za ususi mfano vikapu, mikoba na mikeka, nguo za kudarizi kama batiki na utengenezaji wa viatu vya kimasai kwa kutumia ngozi za wanyama na shanga.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 123 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 3**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Shughuli za uzalishaji mali zinazoendelea kufanyika tangu tulipopata uhuru ni (i) __________ (ii) __________ (iii) __________ (iv) __________
2. Mashirika ya umma yana mashamba makubwa ya kufugia mifugo yanayoitwa __________.
3. Taja mikoa miwili ambayo ina ranchi za taifa.
4. Vitu vinavyotengenezwa na Watanzania kwa ajili ya kuwauzia watalii ni __________, __________, __________, __________ na __________.
5. Taja faida tatu zinazotokana na sekta ya utalii hapa nchini.

## Njia za kuboresha shughuli za uzalishaji mali

Tumeona kwamba, kuna shughuli za aina nyingi za uzalishaji mali zinafanywa na mtu mmojammoja au familia au vikundi vya watu. Kwa mfano, kwenye migodi, viwanda na mashamba makubwa. Ili kuweza kupata manufaa makubwa na yenye faida kubwa, kuna umuhimu wa kuboresha shughuli hizi.

## Kilimo

Shughuli za kilimo zinaweza kuwa bora zaidi kama wakulima watatumia pembejeo sahihi, yaani mbolea na mbegu zilizo bora na kulima kwa majira. Pia, maofisa ugani wanatakiwa kufanya kazi zao kwa ukaribu zaidi na wakulima ili kuwapa elimu na maelekezo sahihi na ya kutosha. Aidha, badala ya kutegemea kilimo cha mvua, wakulima wahimizwe kulima kilimo cha umwagiliaji. Wawe tayari kuhifadhi mazao yao vizuri ili yasiharibike. Pia, wakulima watumie zana bora za kilimo kama vile plau na matrekta ili kurahisisha ulimaji na pia kulima eneo kubwa zaidi na kupata mazao ya kutosha.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 124 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Ufugaji

Mfugaji ili aweze kupata faida kutokana na shughuli ya ufugaji. Ni vizuri mfugaji kuwa na idadi ndogo ya mifugo, kuchagua mifugo bora itakayotoa mazao mengi na bora. Aidha, mfugaji apate ushauri kutoka kwa wataalamu wa mifugo na vituo vya utafiti vya mifugo. Halikadhalika, mfugaji ashauriwe kupanda nyasi ili kuipatia mifugo malisho bora wakati wote na pia apewe elimu juu ya kuhifadhi nyasi vizuri ili kuhakikisha mifugo inapata malisho wakati wote.

## Uvuvi

Ili uvuvi uwe na matokeo mazuri ni lazima uboreshwe kwa kufanya uvuvi unaozingatia njia bora. Katika kuboresha shughuli ya uvuvi, wavuvi wanashauriwa kutumia zana bora na zinazolenga kutunza mazingira ya majini na kulinda mazalia ya samaki. Aidha, wavuvi waelimishwe juu ya madhara ya uvuvi haramu ili waweze kuacha njia haramu za uvuvi, mfano kutumia sumu na baruti na vilevile kuacha matumizi ya kokoro.

## Viwanda

Ili viwanda viweze kuzalisha bidhaa bora zenye kukidhi mahitaji ya watu, vinahitaji mashine za kisasa, malighafi za kutosha, maji, nishati na soko ili uzalishaji bidhaa uwe endelevu. Ili kuboresha uzalishaji, viwanda vinatakiwa kuzingatia uzalishaji wa bidhaa bora na halisi kwa ajili ya kulinda soko la bidhaa hizo. Vilevile, viwanda vitilie mkazo urejelezaji wa takataka zinazozalishwa kwa lengo la kutunza mazingira.

## Biashara

Biashara ni shughuli muhimu katika uzalishaji mali. Ili kuboresha shughuli za kibiashara ni vema kuwe na miundo mbinu ya uchukuzi iliyo bora kama vile bandari, barabara, reli na usafiri wa anga kwa ajili ya usafirishaji wa malighafi na bidhaa. Ni muhimu pia kuwa na mawasiliano mazuri ya simu, mtandao wa kimataifa, huduma bora za kisasa za kibenki, uhusiano mzuri na mataifa mbalimbali duniani na mtaji wa kutosha.

## Utalii

Utalii kama shughuli ya uzalishaji mali ni muhimu sana. Sekta ya utalii inaweza kuboreshwa ili kupata kipato zaidi. Ni muhimu kuendeleza na kudumisha ukarimu, amani na utulivu katika nchi yetu ili kuwavutia watalii

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 125 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kuja kutembea Tanzania. Pia, sehemu wanazotembelea watalii kama vile mlima Kilimanjaro, mbuga za wanyama mfano Serengeti na Mikumi na sehemu zenye kumbukumbu za kihistoria ziboreshwe na kuwa na huduma muhimu.

### Zoezi la 4

**Jibu maswali yafuatayo:**

**Oanisha sentensi katika sehemu A na sentensi kutoka sehemu B ili kupata maana sahihi.**

| Na. | Sehemu A | Majibu | Sehemu B |
|---|---|---|---|
| 1. | Mbuga za wanyama ________ | (   ) | (a) Fedha za kigeni<br>(b) Kwenda shuleni |
| 2. | Shughuli za uzalishaji mali ________ | (   ) | (c) Hutoka Ulaya, Marekani na sehemu nyingine duniani |
| 3. | Wawekezaji ________ | (   ) | (d) Serengeti, Mikumi na katavi |
| 4. | Watalii kutoka nchi za nje ________ | (   ) | (e) Watu wenye mitaji mikubwa |
| 5. | Ranchi za Taifa ________ | (   ) | (f) Kilimo ,ufugaji, uvuvi na shughuli za viwandani |
| | | | (g) Mashamba makubwa ya kufugia mifugo |

## Mapato na matumizi yanayotokana na shughuli za uzalishaji mali

Lengo kubwa la uzalishaji mali ni kupata kipato. Kipato hicho kinaweza kutokana na mazao ya kilimo, madini, bidhaa za viwandani, mazao ya baharini, mazao ya mifugo kama ngozi na mapato kutokana shughuli za utalii. Kwa kiasi kikubwa kipato hicho kinamfikia moja kwa moja mzalishaji mali baada ya kuuza mazao yake na mfanyakazi baada ya kulipwa mshahara. Serikali hupata mapato kutokana na kutoza kodi zitokanazo na mauzo ya bidhaa na mishahara ya wafanyakazi.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Mapato yatokanayo na shughuli za uzalishaji mali kwa mtu binafsi hutumika kwa matumizi mbalimbali, mfano kukidhi mahitaji makuu ya familia kama vile mavazi, malazi na chakula. Matumizi ya mapato ya serikali ni kutoa huduma muhimu za kijamii kama vile hospitali, maji safi na salama na elimu. Pia, mapato haya hutumika kujenga miundombinu kama barabara, umeme na kulipa mishahara ya wafanyakazi.

Vilevile, serikali hupata fedha za kigeni kutokana na mauzo ya bidhaa nje ya nchi na ujio wa watalii nchini mwetu kuona vivutio mbalimbali kama vile mbuga za wanyama, kuona na kupanda milima Meru na Kilimanjaro. Sehemu nyingine muhimu za vivutio ni mambo ya kale na majengo ya kale, kwa mfano Mji Mkongwe Zanzibar na magofu ya Kaole Bagamoyo.

## Zoezi la 5

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja shughuli moja kuu ya uzalishaji mali iliyoanzishwa nchini Tanzania baada ya uhuru ___________.
2. Nini kifanyike ili kilimo kiwe bora zaidi?
3. Taja njia zinazoiwezesha serikali kujipatia fedha kwa matumizi mbalimbali.
4. Mapato yanayopatikana kutokana na shughuli ya uzalishaji mali katika familia yenu hutumika kwa ajili ya nini?

**Andika Ndiyo kwa sentensi sahihi na Hapana kwa sentensi isiyo sahihi.**

5. Kilimo katika Tanzania hufanywa na wakulima wadogowadogo tu. ___________
6. Kokoro hupunguza kiasi cha samaki baharini. ___________
7. Shughuli ya uchongaji vinyago huvutia watalii. ___________
8. Shamba la Kapunga ni kwa ajili ya kilimo cha mtama. ___________
9. Shughuli ya uvuvi inahitaji maofisa ugani. ___________

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 127 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Jaza nafasi zilizoachwa wazi.**

10. Aina mbili za mazao yanayolimwa na wawekezaji ni __________ na __________.
11. Bidhaa mbili zitokanazo na ususi ni __________ na __________.
12. Ili viwanda viweze kuzalisha bidhaa kwa wingi zaidi vinahitaji __________ na __________.

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Jarife | wavu wenye matundu makubwa unaotegwa katika maji yenye kina cha wastani kwa ajili ya kuvulia samaki |
| Kokoro | nyavu zenye matundu madogo sana zinazotumika kuvulia samaki wadogo kinyume cha sheria |
| Ndoana | mtego wa chuma chembamba ulioviringwa sehemu ya nchani na hufungwa kwenye mshipi maalumu, unaotumiwa kuvulia samaki na viumbe wengine majini |
| Ranchi | shamba maalumu linalotumika kufuga na kuzalisha mifugo |
| Upindo | aina ya nguo kama shuka ambayo hutumiwa na wavuvi kuvulia dagaa au samaki wadogo |
| Malale | ugonjwa unaoenezwa na mbung'o |

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 128 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi na Nne

## Ujasiriamali

Katika sura hii, utajifunza maana ya ujasiriamali, jinsi ya kujenga tabia za kijasiriamali na aina za ujasiriamali. Vilevile utajifunza faida za ujasiriamali, fursa za kibiashara zinazopatikana katika sehemu zenye mito, mabwawa, maziwa na bahari. Aidha, utajifunza shughuli zinazofanyika mijini na vijijini, sehemu zenye ufugaji na sehemu zenye viwanda.

### Maana ya ujasiriamali

Ujasiriamali ni dhana pana yenye maana tofautitofauti. Baadhi ya maana hizo ni:

(a) Uwekezaji wa mtaji katika biashara kwa lengo la kujiajiri na kujipatia kipato.

(b) Ujuzi na maarifa ya mtu katika kutumia fursa zilizopo.

(c) Uwezo binafsi wa mtu wa kubadili mawazo na kuyaweka katika vitendo.

Mara nyingi neno ujasiriamali linahusishwa na kuanzisha na kuendesha mradi wa kibiashara. Lakini siyo wafanyabiashara wote ni wajasiriamali. Ili kuanzisha na kukuza biashara kwa mafanikio ni muhimu kuwa na tabia za kijasiriamali.

### Tabia za kijasiriamali

(a) Kujiwekea malengo makubwa

(b) Uthubutu

(c) Ubunifu wa kutumia mawazo na mbinu tofauti zilizopo

(d) Bidii na kutokata tamaa

(e) Kujitegemea na kujituma

(f) Uaminifu na uadilifu

Wako wafanyabiashara wengi ambao wanaanzisha miradi midogo ya kibiashara kwa mazoea au kwa kukosa kitu kingine cha kufanya na hawaoneshi tabia hizi za kijasiriamali. Wajasiriamali ni wale wanaoanzisha



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 129 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

shughuli za kibiashara wakiwa na malengo na kufanya juhudi za kuyafikia. Matokeo yake biashara zao hufanikiwa. Kwa hiyo, Mjasiriamali ni mtu anayefanya shughuli za Ujasiriamali.

## Kisa mafunzo: Soma kisa mafunzo cha mjasiriamali mfugaji, kisha ainisha tabia za kijasiriamali ambazo umezisoma

**Mjasiriamali mfugaji wa kuku**

Baada ya kumaliza elimu ya msingi katika shule ya Msingi Mbuyuni, mkoani Singida. Halima hakubahatika kuchaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari. Wazazi wake hawakuwa na uwezo wa kumpeleka shule ya sekondari ya binafsi. Hivyo, alidhamiria kufanya shughuli za kumuongezea kipato na kutamani watoto wake waje kupata elimu ya juu ambayo yeye hakuweza kuipata. Alidadisi kuhusu shughuli ambayo angeweza kufanya kwa faida. Aliongea na wafanyabiashara wa pale kijijini na wajomba zake ambao walikuwa na maduka Singida mjini.

Aligundua kwamba, wachuuzi walikuwa wakifika vijijini kununua mayai ya kuku wa kienyeji na kuyapeleka mjini kuyauza. Wachuuzi walikuwa hawapati mayai ya kutosha. Pia, walikuwa wakinunua mayai kwa bei ya chini sana, kwa sababu wafugaji waliyachanganya na mayai viza. Halima aliona hii ni fursa kubwa. Alimtafuta afisa ugani ili aweze kupata ushauri juu ya njia bora ya kufuga kuku ili wakue vizuri na kutaga mayai mengi. Afisa ugani alimshauri kuhusu mbegu nzuri ya kufuga na jinsi ya kutengeneza chakula cha kuku kutokana na vyakula na mimea inayopatikana kijijini. Aidha, alimfundisha dawa za asili za kuzuia na kutibu magonjwa ya kuku.

Halima alianza kufuga vifaranga watatu wa mayai ambao aliazima kwa majirani. Aliamua kwamba, angejitofautisha na wafugaji wengine kwa kulisha kuku wake vizuri ili kupata mayai mengi na makubwa. Vilevile, aliazimia kuwa mwaminifu kwa wateja wake. Alipoanza kuuza mayai, wafugaji wenzake walianza kumpiga vita, kwani wateja walikuwa wananunua mayai yake yote kabla ya kuchukua ya wengine. Wafugaji wengine walimwita Halima mchawi. Yeye hakujali na badala yake akawa anawahimiza watumie njia alizotumia kupata mafanikio. Baada ya miaka mitatu, Halima akawa ana mradi mkubwa wa kuku wa nyama na mayai. Halima, aliuza kuku wa nyama na kupata faida kubwa. Pia, alianza kununua mayai ya wafugaji waliokuwa waaminifu na kuchanganya na ya

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 130 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kwake. Kisha, alipeleka mjini kuyauza badala ya kuwasubiri wachuuzi. Aliamua kufungua shamba la ekari 50 ambazo alizitumia kufuga kuku na kustawisha mazao ambayo aliyatumia kuzalishia vyakula vya kuku.

## Aina za wajasiriamali

Neno ujasiriamali linatumika sana kwenye biashara. Hivyo, kuna aina tatu za wajasiriamali:

(a) Wajasiriamali wafanyabiashara: Wanaonesha tabia za kijasiriamali katika kuanzisha na kuendesha biashara.

(b) Wajasiriamali watumishi: Wanaonesha tabia za kijasiriamali katika kazi walizoajiriwa.

(c) Wajasiriamali jamii: Wanaonesha tabia za kijasiriamali katika kujenga uwezo wa jamii kutatua matatizo yake.

## Jinsi ya kujijengea tabia za kijasiriamali

Unaweza kujijengea tabia za kijasiriamali kwa kujitahidi kila wakati kufanya yafuatayo:

(a) Fanya kile kilicho ndani ya uwezo wako kujiendeleza na tafuta msaada pale uwezo wako unapoishia.

(b) Tumia fursa zilizoko karibu nawe hata kama ni kidogo kuanza safari ya kijasiriamali.

(c) Jiweke karibu na watu wenye mitizamo chanya, malengo na bidii.

(d) Jenga uaminifu kwa kutimiza ahadi na ukikopa lipa kwa wakati.

(e) Jiwekee malengo makubwa lakini unayoweza kuyafikia. Yaandike, yatekeleze na kuyafuatilia.

(f) Jenga mtazamo chanya na jifunze kuona mazuri kwenye kila hali.

(g) Weka kumbukumbu za mapato na matumizi yako.

**Tabia za kukwepa ili kuwa mjasiriamali mahiri:**

(a) Usiendekeze uvivu, uchukie kama ukoma.

(b) Usipoteze muda, kwani kila dakika inayopotea ni mali inapotea.

(c) Acha visingizio. Mafanikio yako yanakutegemea wewe kwa asilimia zaidi ya 90.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 131 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

(d) Usiwe tegemezi wa mawazo wala rasilimali.

(e) Usikate tamaa, mpaka upate unachokitafuta.

(f) Uwe mbunifu ili kuboresha shughuli zako za ujasiriamali.

**Maana ya ubunifu na faida zake**

Ubunifu maana yake ni kutekeleza wazo jipya ili kutengeneza ama kuboresha bidhaa, huduma au kuongeza tija. Ubunifu una faida mbalimbali kama vile, kuvutia wateja, kukabiliana na ushindani, kupanua na kuongeza faida. Pia, unaweza kutumia ubunifu kudhibiti mianya ya wizi.

## Fursa ya biashara

Fursa ya biashara ni uwezekano wa kufanya shughuli halali za biashara kwa faida. Uwezekano huo unakuwepo kama kuna watu wenye uhitaji na uwezo wa kununua bidhaa zinazouzwa. Aidha, kuwa na rasilimali unazoweza kuzitumia kukidhi mahitaji hayo kwa faida inayopatikana. Kwa mfano, kama wanakijiji wanahitaji maziwa na wana uwezo wa kuyanunua, unaweza kufuga ng'ombe na kuwauzia maziwa kwa faida.

## Sehemu zenye fursa za kibiashara

Fursa za kibiashara zipo katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano, sehemu za kandokando ya bahari, mito, maziwa na mabwawa, sehemu zenye wafugaji, viwanda, mijini na vijijini. Katika maeneo haya, kitu muhimu ni kwa mjasiriamali ni kuangalia fursa zilizopo na kuzitumia kwa tija.

## Fursa za kibiashara katika sehemu zenye mito, mabwawa, maziwa na bahari

Baadhi ya fursa zinazoweza kuwepo katika sehemu zenye mito, mabwawa, maziwa na bahari ni uvuvi, kilimo cha mwani na mashamba ya chumvi. Vilevile, usafirishaji, utalii wa majini na huduma za michezo ya kuogelea na kupiga mbizi. Shughuli nyingine ni huduma za kusafisha samaki, huduma za vyoo na maliwato. Shughuli hizi hufanyika kandokando ya bahari ya Hindi na maziwa kama Victoria, Tanganyika, Nyasa, Eyasi, Manyara, Jipe na Rukwa. Pia, kuna fursa ya shughuli za uvuvi na usafirishaji.

Fursa nyingine katika sehemu hizi, ni pamoja na biashara ya maduka ya vifaa vya uvuvi, kama vile nyuzi, ndoana na nyavu. Pia, kuna maduka ya



MAARIFA YA JAMII V KITABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 132 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

kawaida kwa ajili ya bidhaa ndogondogo, kama vile sukari, chumvi, mafuta ya kupikia na unga, ambazo hununuliwa na watu wanaofanya biashara ya kuuza na kununua samaki. Vilevile, kuna biashara za magenge ya chakula cha mama na baba lishe. Pia, wafanyabiashara wadogowadogo maarufu kama wamachinga wanaouza bidhaa zao katika mazingira hayo.



**Kielelezo namba 1:** Shughuli za ujasiriamali pembeni mwa bahari au ziwa

## Kazi ya kufanya

Jadiliana na wenzako juu ya fursa za kibiashara zilizoko katika maeneo yenu. Andika shughuli ulizojadili kwenye daftari lako.



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 133 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

**Zoezi la 1**

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza maana ya ujasiriamali.
2. Taja tabia tano za wajasiriamali.
3. Eleza tofauti kati ya mfanyabiashara mjasiriamali na anayefanya biashara kwa mazoea au kushikiza tu.
4. Taja fursa za kibiashara zilizoko katika maeneo ya pembezoni mwa bahari na maziwa.

## Fursa za biashara zilizoko mijini

Fursa za biashara sehemu za mijini zipo za aina nyingi. Hali hii, hutokana na idadi kubwa ya watu waishio mijini. Wakazi wa mijini wana mahitaji mengi ambayo yamesababisha watu wengine kubuni shughuli mbalimbali ili kutoa huduma kwa wakazi wa mijini na kujipatia kipato.

Fursa za kibiashara zilizoko mijini ni pamoja na udobi ambao ni kufua na kunyoosha nguo za watu mbalimbali kwa kutumia mikono au mashine. Aidha, kung'arisha viatu, huduma za chakula zinazofanywa na mama na baba lishe, kushona nguo, miradi ya usafirishaji kwa kutumia pikipiki (boda boda) na mikokoteni. Pia, vikundi vya akina mama vya kutengeneza bidhaa kama vile sabuni za kufanyia usafi majumbani na dawa za kuondoa madoa kwenye nguo. Vikundi vingine ni vile vya kutoa huduma katika shughuli mbalimbali kama vile kwenye harusi na matamasha mbalimbali. Huduma hizo ni kama vile, kupamba, kuburudisha kwa muziki na huduma za chakula. Shughuli nyingine ni ususi, kinyozi na huduma nyingine za saluni.

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE




**Kielelezo namba 2:** Baadhi ya shughuli za ujasiriamali mijini

## Fursa za kibiashara sehemu zenye wafugaji

Ufugaji ni shughuli ya kutunza wanyama kwa lengo la kupata mazao ya wanyama kama vile maziwa, nyama, mafuta, mayai na ngozi. Fursa za biashara kwenye maeneo yenye wafugaji ni kama vile: Uuzaji wa nyama na maziwa, utengenezaji mapambo kwa kutumia ngozi na shanga mfano, hereni, bangili na mikufu na utengenezaji wa mikanda ya ngozi na viatu kwa kutumia ngozi. Vilevile, silaha kama mishale, sime na mikuki hutengenezwa katika maeneo ya wafugaji. Shughuli nyingine inayopatikana kwenye maeneo yenye wafugaji ni kutengeneza mazao yanayotokana na maziwa, mfano samli na jibini. Pia, wajasiriamali wanaweza kufuga kuku na bata na hivyo kuuza nyama na mayai.

Fursa nyingine katika sehemu za ufugaji ni kuuza dawa za kutibu mifugo na kutengeneza vyakula vya mifugo kama kuku.



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 135 30/07/2021 09:33

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Fursa za kibiashara katika sehemu zenye viwanda

Viwanda ni mahali ambapo bidhaa mbalimbali huzalishwa kwa kutumia mashine, watu na malighafi. Katika viwanda kuna mkusanyiko wa watu wengi ambao ni wafanyakazi katika viwanda hivyo, huhitaji huduma mbalimbali. Huduma ambazo hutolewa na wajasiriamali ni kama maduka yanayouza bidhaa mbalimbali, migahawa, mama na baba lishe na huduma za kifedha. Pia, katika sehemu za viwanda kuna huduma za usafirishaji kama vile, huduma za usafiri kwa pikipiki na magari madogo na makubwa yanayobeba bidhaa kutoka viwandani kwenda kwa wauzaji na wasambazaji.

### Zoezi la 2

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja fursa za biashara zinazoweza kuwepo katika sehemu za wafugaji.
2. Kutokana na maziwa ya ng'ombe tunapata mazao kama ___________, ___________ na ___________.
3. Udobi ni nini?
4. Taja fursa mbili za biashara zinazoweza kufanywa zaidi na wajasiriamali wanawake.

### Zoezi la 3

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Eleza umuhimu wa kuwa na tabia za kijasiriamali.
2. Taja tabia nne ambazo unatakiwa kuziepuka ukitaka kuwa mjasiriamali mwenye mafanikio.
3. Orodhesha fursa za kibiashara zilizopo katika eneo unaloishi.
4. Wamasai hutengeneza hereni, mikufu na bangili kwa kutumia ___________.

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 136 30/07/2021 09:33

**Andika neno Ndiyo kwa sentensi ambazo ni sahihi na Hapana kwa sentensi ambazo si sahihi.**

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

5. Kila anayefanya biashara ndogondogo ni mjasiriamali.______
6. Ukiwa na tabia za kijasiriamali una uwezekano mkubwa wa kufanikiwa katika biashara. __________
7. Bila kuwepo na wanunuzi wenye uwezo wa kununua unachozalisha, hakuna fursa ya kibiashara. __________
8. Mahali penye viwanda huvutia wajasiriamali. __________
9. Mafanikio ya mtu yanamtegemea mtu mwenyewe zaidi kuliko serikali au watu wengine. __________
10. Mjasiriamali anaweza kutoa ajira kwa wanajamii. __________
11. Wako wafugaji, wakulima, wavuvi na wachuuzi ambao hawafanyi kazi zao kijasiriamali. __________
12. Kujiajiri mwenyewe ni kati ya mambo yanayochangia kukuza pato la Taifa. __________

**Chagua herufi ya jibu sahihi.**

13. Unapoanzisha mradi wa kufuga kuku, lengo kuu ni kupata:
    (a) kuku au mayai
    (b) faida ( )
    (c) kipato
    (d) kitoweo
14. Ili kuongeza kipato na kufaidi matunda ya ujasiriamali ni vyema:
    (a) kufanya kazi kwa bidii
    (b) kupumzika na kusubiri mapato ( )
    (c) kuomba msaada wa Mungu
    (d) kutafuta watumiaji

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Msamiati

| | |
|---|---|
| Jibini | aina ya chakula laini/kigumu kilichotengenezwa kutokana na maziwa mgando na ambacho kwa kawaida kina rangi nyeupe/manjano |
| Samli | mafuta ya kupikia yanayotokana na maziwa ya mnyama, kama vile ng'ombe na mbuzi |
| Ujasiriamali | ni uwekezaji wa mtaji katika biashara kwa lengo la kujiajiri na kujipatia kipato |
| Mjasiriamali | mtu anayefanya biashara kwa kufanya ubunifu, utafutaji wa fedha na kujishughulisha katika kutafuta faida kwa manufaa yake |

FOR ONLINE USE ONLY



MAARIFA YA JAMII V KiTABU CHA MWANAFUNZI 27/10/2018 FONT 12.indd 138 30/07/2021 09:33

Vitabu kutoka

Taasisi ya Elimu Tanzania

## Darasa la Tano




ISBN 978-9987-09-332-8

Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi

Maarifa ya Jamii   Kitabu cha Mwanafunzi   Darasa la Tano